# Nipashe

Jumatatu Desemba 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581157

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Samia** asamehe wafungwa 1,631 Siku ya Uhuru



UKURASA 2



NIPASHE JUMATATU DESEMBA 12, 2022

Nipashe Spotika

NUKUU 10 BORA KUHUSU RONALDO UK.16 - 17

ISIKUPITE

Harry Kane alifikia rekodi ya Wayne Rooney ya kufunga mabao 53 England baada ya bao lake la kwanza la kusawazisha dhidi ya Ufaransa kwenye mechi ya Robo Fainali ya Kombe la Dunia, lakini usiku wake juzi uliisha kwa huzuni baada ya kuchapwa 2-1 huku akikosa penalti ambayo ingeiwezesha timu yake kusawazisha. Hata hivyo, Kane amefikisha mabao hayo baada ya mechi 80 wakati Rooney alihitaji mechi 120 kufikisha idadi hiyo.

LA NUSU FAINALI...

Mshambuliaji wa Morocco, Youssef En-Nesyri (kulia), akiifungia timu yake kwa kichwa bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Ureno kwenye mechi ya Robo Fainali ya Kombe la Dunia la Fifa nchini Qatar juzi. Bao hilo limeiwezesha Morocco kufuzu nusu fainali ambapo sasa itakutana na Ufaransa Jumatano saa nne usiku. **PICHA: MTANDAO**

UKURASA 13



# Mbowe: Nilikamatwa, kufungwa kitambaa usoni kwa siku tatu

• **Afichua** kilichowakuta kina Lema, Lissu hadi kukimbilia ughaibuni... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**TUTAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WANACHAMA OACPS - MAJALIWA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Nchi...

UKURASA WA 7

**KAMPASI MPYA KUANZISHWA MAFUNZO YA USAFIRI WA RELI**

UONGOZI wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) umesema upo kwenye...

UKURASA WA 26

**WATOTO WA FAMILIA 1 WADAIWA KUKEKETWA**

WATOTO wawili wenye umri kati ya miaka 14 na 16 wa familia moja, wakazi wa kijiji...


## Dk. Mwinyi alivyopokewa kwa shangwe visiwani Z'bar

UKURASA 9



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Mama Siti Mwinyi na viongozi mbalimbali alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume jana, akitokea Dodoma alikoshiriki Mkutano Mkuu wa 10 uliomchagua kushika nafasi hiyo. Kulia ni mke wake, Mariam Mwinyi. **PICHA: IKULU**

## Abiria walia nauli za mabasi kupanda UK.26


**MICHEZO** KOCHA SIMBA QUEENS ATUA YANGA UK.28 **KATUNI** UK.6

# Samia asamehe wafungwa 1,600

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha kwa wafungwa 1,631 wenye makosa mbalimbali, wakiwamo wa kike walioingia na ujauzito gerezani.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, msahama huo umetolewa wakati wa kuadhimisha miaka 61 ya uhuru wa Tanzania Bara.

Waziri huyo alisema jana kuwa msamaha huo wa Rais umetolewa kwa kuzingatia kifungu cha 45(I)(d) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wafungwa wenye sifa stahiki wapunguziwe robo ya adhabu zao baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu.

Alisema kati yao, 101 wameachiwa huru kuanzia Desemba 10, mwaka huu na 1,530 watabaki gerezani kumalizia sehemu ya kifungo kilichobaki baada ya kupewa msamaha huo.

Pia alisema wengine waliopata msamaha ni wafungwa ambao ni wagonjwa wenye magonjwa sugu ambao wako katika hatua ya mwisho na wenye umri wa kuanzia miaka 70.

"Wafungwa wa kike walioingia na mimba gerezani au wenye watoto wanaonyonya na wasionyonya, wafungwa walemavu wa mwili na akili wasio na uwezo wa kufanya kazi na hali zao zithibitishwe na jopo la uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa na Wilaya.

"Pia wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 15 na wale waliohukumiwa kifungo cha maisha gerezani ambao wametumikia adhabu hiyo kwa miaka 20 au zaidi.

"Pia waliobadilishiwa adhabu ya kifo na kuwa maisha na wamekaa miaka 20 au zaidi kuanzia walipoanza kutumikia adhabu ya kifo," alifafanua.

Alitaja makundi yaliyokosa msamaha huo ni wafungwa waliopatikana na hatia kuhukumiwa kifungo kwa makosa ya kujamiana, utekaji au wizi wa watoto, kupoka na kuwapa mimba wanafunzi au makosa yoyote yale yanayohusiana na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na kujihusisha kwa namna yoyote ile na biashara haramu.

Wengine ni wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu, unyang'anyi wa kutumia silaha au kujaribu kutenda makosa hayo, wafungwa wanaotumia vifungo kwa makosa ya kujihusisha kwa namna yoyote ile na nyara za serikali na ujangili, wizi na ubadhirifu wa fedha za serikali.

Pia wafungwa wanaotumikia vifungo vya makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo.

# Mbowe: Nilikamatwa na kufungwa kitambaa usoni

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameyashukuru makundi yaliyompigania alipokamatwa kwa tuhuma za ugaidi.

Vilevile amedai kuwa siku chache baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, alikamatwa na kufungwa kitambaa cheusi usoni akiwa Dar es Salaam na baada ya siku tatu, alijikuta yuko Bagamoyo mkoani Pwani.

Mbowe aliyasema hayo juzi alipozungumza na Watanzania wanaoishi Marekani katika ziara yake ya siku sita, akihudhuria pia mkutano wa Umoja wa Vyama vya Demokrasia Afrika (IDU) ambao CHADEMA ni wa mwanachama.

Mbowe alisema kuwa wiki mbili baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. Magufuli, walimwandikia barua Rais aliyepokea kijiti, Dk. Samia Suluhu Hassan kumwomba maridhiano ya kitaifa, wakiamini ni njia sahihi ya kufanya kazi kwa pamoja kujenga nchi.

"Akajibu, katika siku tatu za kwanza Rais akajibu barua ile, akasema anatambua na yupo tayari tuzungumze mambo haya. Tukaupokea uamuzi wake na barua ile kwa mapenzi makubwa," alisema Mbowe.

Aliwashukuru wanadiaspora, wanaharakati, wanasiasa na viongozi wa dini waliopaza sauti dhidi ya kukamatwa kwake.

Aliusifia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa usikivu, akibainisha kuwa hata walipomwandikia, aliwajibu ndani ya siku tatu walipohitaji maridhiano ya kitaifa.

Mwenyekiti wa CHADEMA huyo alisema kuwa katika mkutano wao wa kwanza na Rais Samia, walimwomba wawekeane misingi, ikiwamo kujadili kuwapa haki Watanzania kwenye uchaguzi na mahakama, akisisitiza kuwa Mkuu wa Nchi alikubali hoja hiyo.

KITAMBAA CHEUSI

Mbowe alidai kuwa alikamatwa Oktoba 30, 2020 majira ya saa nne usiku baada ya kumaliza kikao na viongozi wenzake waliojumuisha vyama vingine vya upinzani, akiwamo Zitto Kabwe, Kiongozi wa ACT-Wazalendo).

Alibainisha kuwa katika mkutano wao huo, mbali na Zitto, viongozi wengine walioshiriki ni pamoja na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, Godbless Lema, Boniface Jacob na mwakilishi wa Maalim Seif Sharif Hamad (hayati) aliyegombea urais wa Zanzibar alituma mwakilishi) ambaye hakumtaja kwa jina.

Alisema mkutano wao huo ulilenga kujadili mchakato wa uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 28, 2020.

"Kama vyama vikuu vya upinzani tulijadiliana na tukakubaliana kuhusu uchaguzi huu na yote tuliopitia.

"Makubaliano ya kikao kile ni kwamba tusikubaliane na uchaguzi huo na tuwaombe Watanzania wenzetu tufanye maandamano ya amani kupinga uchafuzi ule kwa taifa," alisema.

Hata hivyo, Mbowe alidai kuwa muda mfupi baada ya mkutano huo, alikamatwa na kufungwa kitambaa cheusi usoni na kupelekwa sehemu asiyoifahamu.

Alidai kuwa baada ya siku tatu, aligundua alikuwa Bagamoyo pasi na kufahamu wenzake, akiwamo Lema walikokuwa.

"Mheshimiwa Lissu hakukamatwa, alijua atakamatwa, akakimbilia kwenda Ubalozi wa Ujerumani kutafuta hifadhi ya ukimbizi na akaipata, wakamhifadhi na hatimaye akaondoka kwenda Ubelgiji na Lema baada ya kuachiwa kwa dhamana, akaondoka akaenda Kenya na baadaye akaenda Canada," alisema Mbowe.

Hata hivyo, kiongozi huyo hakuwataja watu aliodai walimkamata na kumpeleka Bagamoyo.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akipokea tuzo ya kimataifa iliyotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya Iconic Awards ya nchini India (IIA) kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na umahiri wake alioonesha kwenye filamu ya 'Tanzania The Royal Tour' walimwa mwongoza watalii namba moja nchini. Kushoto anayekabidhi tuzo hiyo ni Martin Rajab ambaye ni mmoja wa viongozi kutoka Miss Jungle International na Bega kwa Bega na Mama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tutaendelea kushirikiana na wanachama OACPS - Majaliwa

**Na Mwandishi Maalum,** LUANDA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS) katika kudumisha usalama na amani miongoni mwa nchi washirika.

Pia amesema Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na jumuiya hiyo katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wao.

Aliyasema hayo juzi alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za OACPS uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Interconental jijini Luanda, Angola.

Alisema licha ya changamoto ambazo nchi hizo zimeendelea kupitia, likiwamo janga la Uviko-19 na athari za migogoro inayotokea duniani, jumuiya hiyo imeendelea kushirikiana kikamilifu katika kutimiza malengo husika na kuratibu shughuli zake kwa maslahi ya nchi wanachama.

"Tanzania itaendelea kuwa mshirika thabiti katika jumuiya hii na ili kuhakikisha malengo ya nchi washirika yanatimia, ni vyema kila mmoja wetu akajenga nia hiyo ili kupata mafanikio ya pamoja," alisema.

Majaliwa alisema tangu kuanzishwa kwa jumuiya hiyo, malengo mengi ya pamoja yamefikiwa na manufaa yamepatikana kupitia programu mbalimbali na utekelezaji wa miradi ya ubia miongoni mwa nchi washirika.

"Hatujafanya vya kutosha kutimiza kikamilifu malengo ya kuanzishwa kwa OACPS, hivyo ni vyema tuendelee kutekeleza sera, shabaha, programu na miradi tuliyoweka ili kufikia malengo tarajiwa," alihimiza.

Waziri Mkuu alisema mshikamano miongoni mwa nchi wanachama ndiyo nguzo pekee inayoweza kuziweka nchi zote salama na kuleta maendeleo ya kweli yanayowagusa wananchi moja kwa moja.

Jumuiya ya OACPS ina jumla ya nchi wanachama 79 kutoka Afrika, Karibiani na Pasifiki yenye madhumuni ya kuimarisha mshikamano, umoja na maendeleo kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo ikiwamo Umoja wa Ulaya (EU) na wadau wengineo ili kufikia maendeleo endelevu.

# TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED (TANESCO)

"We light up your life"

# JOB OPENINGS

**1.0. Introduction**

Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO) is undergoing massive reformation of its operations focusing on increasing the outreach and service quality in Tanzania and region as well. The reformation includes increasing power generation, enhancing business excellence, power reliability and improving customer service. To reach its goals, the Company has reviewed its Organization Structure and therefore invites self-motivated, honest, hardworking and committed Tanzanians to fill the under-mentioned posts at Head Office.

**2.0. Vacant Positions**

**2.1. Director Communication and Corporate Affairs**

**Position Details:**
**Reports to: Managing Director**
**Supervises: All Employees in the Communication and Corporate Affairs Directorate**
**Workstation : Head Office**

**Duties and Responsibilities:**

(i) Advise the Managing Director on all matters pertaining to communications and corporate affairs in the Company;
(ii) Oversee development of comprehensive Corporate Communication plans, strategies and approaches to promote TANESCO image to stakeholders, businesses, industry and media locally, regionally and nationally;
(iii) Formulate and implement Public Relations and Marketing policies that support the organization's activities, objectives and policies, and geared towards realization of Company's vision and mission;
(iv) Plan and prepare a comprehensive Marketing and Communication Strategies/Initiatives for the Company aimed at promoting company products and services as well as enhancing the corporate image and reputation;
(v) Drive a strong public affairs agenda representing current and anticipated future needs of the business;
(vi) Serve as company's spokesperson in highly sensitive, complex or emergency situations – in liaison with Managing Director;
(vii) Develop and maintain healthy relationships with key stakeholders: government, investors, policy influencers and advocate with them, and work with them on relevant and emerging matters that affects the business;
(viii) Provide professional advice to the Company Management in all matters related to Communication, Marketing and Public Relations in the Company; and

**Qualifications**

- Bachelor's Degree in Mass Communication/Marketing/Public Relations/ or Journalism.
- Must have Master's degree in Mass Communication/Marketing/Public Relations/ or Journalism.
- Minimum of 12 years' working experience and proven good performance in energy sector, out of which at least three (3) years should be in managerial level.

**2.2. Director Resource Mobilization and Business Development**

**Position Details:**
**Reports to : Deputy Managing Director Planning, Research and Investment**
**Supervises : Managers under the Resource Mobilization and Business Development Directorate**
**Workstation : Head Office**

**Duties and Responsibilities**

(i) Develop and implement a Resource Mobilization Strategy;
(ii) Spearhead proposal development efforts ensuring efficient coordination with teams and the submission of funding proposals in strategic priority theme;
(iii) Continually seek innovative means of attracting private funds and donor interest to meet our investment objectives;
(iv) Contribute to private sector development by executing innovative, developmental and profitable resource mobilizations activities;
(v) Build including development of collateral materials to support fundraising efforts, such as brochures and donors' conferences;
(vi) Create and monitor relationships with new and existing external partners, and creating resource mobilization plans, strategies/guidelines for these partners;
(vii) Manage the resource mobilization functions by monitoring and reporting on the implementation of strategic projects;
(viii) Engage in donor relationship management through networking, meetings and research to ensure donor retention and upgrades while capturing new development partners;
(ix) Establish resource development objectives to support strategic priorities;
(x) Prepare and develop donor information and related supporting documentation to present to donors such as basic brochures, success stories, description of organization activities, monitoring and evaluation reports etc.

**Qualifications:**

- Bachelor and Master Degree in Business Administration/Economics/Statistics or Finance.
- A minimum of 12 years of relevant working experience and proven good performance, out of which at least three (3) years should be in managerial level.

**2.3. Manager Risk and Compliance Management**

**Position Details:**
**Reports to : Managing Director**
**Supervises : All Employees in the Risk Management and Compliance Section**
**Workstation : Head Office**

**Duties and Responsibilities**

(i) Advise Managing Director on all matters pertaining to risk and compliance management in the Company;
(ii) Develop and coordinate implementation of the organization risk management policy and process;
(iii) Perform a risk assessment by analysing current risks and identifying potential risks that are affecting the company;
(iv) Coordinate the development of a Business Continuity strategy and plans to ensure Business Continuity in the events of Business Interruption;
(v) Design and implement an early warning or trigger system for breaches of the company's risk appetite or limits;
(vi) Coordinate the set up and maintenance of a Risk Register and other risk information with clearly defined risk categories and risks;
(vii) Investigate irregularities and non-compliance issues;
(viii) Monitor compliance with laws, regulations and internal policies;
(ix) Collaborate with other departments to create a culture of compliance;
(x) Implement and manage an effective legal compliance program; and
(xi) Perform any related duties as may be assigned by the Managing Director.

**Qualifications**

- Bachelor Degree in Risk Management, Insurance from a recognized and reputable institution.
- Must have a Master Degree in Risk Management, Insurance or related qualification from a recognized institution.
- Minimum of ten (10) years' working experience and proven good performance.
- Must be registered with relevant profession Board.

**2.4. Manager Resource Mobilization**

**Position Details:**
**Reports to: Director Resource Mobilization and Business Development**
**Supervises: All Employees in the Partnership and Resource Mobilization Section**
**Workstation: Head Office**

**Duties and Responsibilities**

(i) Advise Director Resource Mobilization and Business Development on all matters pertaining to resource mobilization in the Company;
(ii) Identify funding opportunities, listing them and appraise the management;
(iii) Collaborate with public and private teams to on-board resources/ investments;
(iv) Contribute to private sector development by executing innovative, developmental and profitable resources/investments;
(v) Assist in developing a fund generation and resource mobilization Work plan and constantly follow-up the implementation of the plan through communication with different prospective donors and agencies;
(vi) Coordinate processing of agreements in connection with funding opportunities and ensure effective and timely follow-up in terms of submission of reports to the donors and grant renewal proposals;
(vii) Develop both short and long-term resource plans, recommend investments and assign assets e.g. Public Equities, Fixed Income, Private Equity;
(viii) Ensure that fundraising and resource mobilization information are up to date;
(ix) Solicit and link prospective sponsors for programmatic sessions; and
(x) Monitor and participate in the negotiations and resource structuring process with analysis to optimize outcomes that adhere to the Government policies.
(xi) Perform any other related duties as may be assigned by Director Research, Environment and Projects.

**Qualifications**

- Bachelor and Master Degree in Business Administration/Economics/Statistics or Finance.
- Minimum of 10 years of relevant working experience and proven good performance.

**2.5. Manager Utility Fibre Network & Telecommunication Services**

**Position Details:**
**Reports to: Director Transmission Lines and Substations**
**Supervises: All employees in Utility Fibre Network & Telecommunication Services Section**
**Workstation: Head Office**

**Duties and Responsibilities**

(i) Advice the Director of Transmission Lines and Substations on all matters pertaining to Utility Fibre Network & Telecommunication Services;
(ii) Operation, maintenance, installation and upgrades of all grid communication network systems including tele-protection;
(iii) Operation, maintenance and installation of DC system for all substations (primary and secondary substations);
(iv) Operation, maintenance and installation of VHF radio network systems in generation, distribution and transmission;
(v) Operation, maintenance and installation of grid voice communication systems (grid PABX alias carrier telephones);
(vi) Operation, maintenance and installation of office telephony systems (office PABX both IP and analogue);
(vii) Coordinate connection of new offices district and regional offices to optical fibre network systems;
(viii) Liaising with National ICT backbone technical staff on maintenance schedules of the optic fibre cable systems; and
(ix) Perform any other related duties as may be assigned by Director Transmission Lines and Substations.

**Qualifications**

- Bachelor and Master Degree in Telecommunication/Electronics/ICT Engineering.
- A minimum of ten (10) years of relevant working experience and proven good performance.
- Must be registered with Engineers' Registration Board (ERB) at least as Professional Engineer.

**3.0. How to Apply:**

All interested candidates should send a detailed written application attached with detailed curriculum vitae (CV) attached with all relevant certificates including two (2) referees. Application closing date is **Monday, 26th December, 2022 before 5:00PM.** All applications should be addressed to:

**MANAGING DIRECTOR,**
**TANESCO HEAD OFFICE,**
**Dar Es Salaam Road,**
**PO BOX 453,**
**DODOMA.**

**Note:**

- All applications shall be sent through email **recruitment@tanesco.co.tz.**
- No physical application shall be accepted.
- TANESCO provides equal opportunity and fair and equitable treatment in employment to all people without regard to race, color, religion, sex, age, disability, political affiliation, marital status, or sexual orientation.
- Women are highly encouraged to apply.
- All Applicants who will not be invited for an interview should consider themselves unsuccessful.

You can also visit our website **www.tanesco.co.tz** to view these job openings.

17189501

Coca-Cola Real Magic TUZO ZA RAIS ZA MZALISHAJI BORA WA MWAKA KILIMANJARO DRINKING WATER

# Bonite Bottlers Ltd: Uwekezaji katika teknolojia za kisasa umetufanya tung'are katika PMAYA 2022

*Na mwandishi wetu*

Novemba 18, 2022 Bonite Bottlers Ltd, wazalishaji wa bidhaa za Coca Cola na Maji ya kunywa ya Kilimanjaro, iliyopo Shirimatunda, Kilimanjaro walitunukiwa Tuzo ya Rais ya Mzalishaji bora wa mwaka katika kipengele cha vinywaji visivyo na kilevi.

Hii ni mara ya pili kwa kampuni hii bora kupokea tuzo hiyo, 2021 ikiwa ya kwanza. Tuzo hiyo ilitolewa na Makamu wa Rais, Philip Mpango kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

**PMAYA ni nini na jukumu lake ni lipi?**

Tuzo za Rais za Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA) ni hafla ya kila mwaka ambayo huandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) ili kutoa tuzo kwa kampuni zilizofanya vizuri katika mwaka uliotangulia.

Tuzo hizi zilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2005 na zimefanyika kila mwaka tangu wakati huo. Tuzo hizo zinalenga; kutambua na kuthamini mchango muhimu wa sekta ya viwanda katika mchakato wa maendeleo ya uchumi wa Tanzania, kuinua kiwango cha ufanyaji wa biashara na utawala bora wa mashirika nchini na kutambua na kutathmini maendeleo ya kiteknolojia katika sekta ya viwanda.

Kwa kipindi cha miaka 17 mfululizo (tangu 2005), CTI imekuwa ikiandaa tukio hili la kifahari zaidi la wanachama linalojumuisha sekta zote za uchumi.

Washindi wa shindano hilo hukabidhiwa tuzo wakati wa hafla ya chakula cha jioni ya kibiashara inayoandaliwa na CTI ambayo kwa kawaida huhuduriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni mlezi wa CTI.

**Mwakilishi wa Bonite azungumzia siri ya ushindi**

Katika mahojiano na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bonite Bottlers Raman Anantha Narayanan, alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali na Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na Uongozi wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) kwa tuzo hiyo chini ya kipengele cha vinywaji visivyo na kilevi, ambavyo ni maji ya kunywa ya kilimanjaro na soda za Coca Cola.

Akibainisha baadhi ya mambo yaliyosababisha kutwaa tuzo hiyo, Narayanan aliishukuru Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa msaada wa mara kwa mara katika masuala ya sera na miundombinu ambayo inawawezesha wenye viwanda kote nchini kuzalisha bidhaa zinazokidhi mahitaji ya watu.


Sababu nyingine aliyoitaja ni uwekezaji katika teknolojia za kisasa zaidi za uzalishaji na uboreshaji wa chupa za bidhaa zao zote mbili Coca Cola na maji ya kunywa ya Kilimanjaro ambazo inazipa ubora wa hali ya juu kwa watumiaji wao.

Narayanan pia alitoa shukrani kwa bodi ya wakurugenzi, uongozi na wafanyakazi chini ya uenyekiti wa Abdiel Mengi kwa miongozo na msaada wanaoutoa katika kufikia malengo ya kampuni. Abdiel alichukua nafasi hiyo iliyoachwa na Hayati, Dk Reginald Mengi na ana ndoto kubwa za kuendeleza misingi na maadili mema iliyowekwa na Hayati Dk Mengi.

Kampuni ya Bonite Bottlers itaendelea kuheshimu dhamira yake kwa umma wa Watanzania kwa kuhakikisha wanaendelea kuzalisha bidhaa zao katika ubora wa hali ya juu kwa watumiaji wao.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Fillip Mpango (kulia) akikabidhi cheti kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bonite Bottlers, Raman Anantha Narayanan wakati wa hafla ya ugawaji wa tuzo za Rais za Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA).



Coca-Cola Real Magic

TUZO ZA RAIS ZA MZALISHAJI BORA WA MWAKA

KILIMANJARO DRINKING WATER

# WINNER 2021 & 2022

President's Manufacturer of the Year Award

**BONITE BOTTLERS LTD**




Coca-Cola Real Magic

KILIMANJARO DRINKING WATER

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB iongeze makali zaidi kwa waamuzi raundi ya pili Ligi Kuu

**WAKATI** mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukitarajiwa kuanza Alhamisi wiki hii baada ya timu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo kukamilisha kucheza mechi 15 kila moja, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), imekiri kwamba bado kuna changamoto kubwa katika suala zima la waamuzi kwenye ligi hiyo.

Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mguto, katika tathmini yake ya mzunguko wa kwanza amesema kuwa kila kitu kimekwenda vizuri na hakuna malalamiko yoyote kutoka kwa wachezaji na hata klabu kuhusu kucheleweshewa malipo yao, lakini changamoto kubwa imekuwa suala zima la waamuzi.

Katika ligi hiyo ambayo inaingia mzunguko wa pili, Yanga ikiwa kileleni mwa msimamo baada ya kujikusanyia alama 38 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 35 moja mbele ya Simba inayoshika nafasi ya tatu, baadhi ya waamuzi walionekana kuwa tatizo katika kuzitafsiri sheria 17 za soka ama kwa kutojua au kwa dhamira yao mbaya wenyewe, jambo ambalo lilikuwa kero raundi ya kwanza.

Hadi mzunguko huo unakamilika, timu ya Polisi Tanzania ndiyo inayoburuza mkia ikiwa na alama tisa ikifuatiwa na Ruvu Shooting na Ihefu FC zenye pointi 11 katika nafasi ya 14 na 13, hivyo kwa ligi hiyo inaelekea katika raundi ngumu zaidi, jambo ambalo suala la waamuzi kuvurunda linapaswa kumulikwa zaidi.

Ni ukweli usiopingika waamuzi wa soka nchini wamekuwa chanzo kikubwa kwa baadhi ya timu kumaliza mzunguko wa kwanza katika nafasi zisizostahili. Katika hilo, zipo zilizonufaika kwa kuzawadiwa pointi ambazo zimezifanya kumaliza nafasi za juu, lakini kuna baadhi ambazo zimeporwa alama zao na kujikuta zikimaliza mzunguko wa kwanza kwa kushika nafasi za chini ama za kati.

Hiyo inamaana kama huu ndio ungekuwa mzunguko wa pili, baadhi ya timu zingeshuka daraja ama kwenda kucheza mechi za mchujo 'play off ' kutokana na maamuzi mabovu ya baadhi ya waamuzi, lakini hata bingwa angepatikana pasipo haki kutendeka.

Kwa kuthibitisha hilo, tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa TPLB, pamoja na kamati zake ikiwamo cha Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), imeonyesha meno yake kwa kuwafungia baadhi ya waamuzi waliobainika kufinyanga sheria 17 za soka.

Hivyo, kuelekea mzunguko huu wa pili wiki hii pamoja na TPLB kukiri kuwapo tatizo, waamuzi hawana budi kujitathmini zaidi na kugeukia katika kutenda haki na ionekane kweli ikitendeka ili ligi yetu izidi kuwa bora na kuvutia wawekezaji wengi zaidi.


Si hilo tu, bali pia waamuzi wakichezesha kwa haki tutapata wawakilishi bora wa nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu Afrika, ambazo zitabeba jukumu la kwenda kuipeperusha bendera ya Tanzania.

Hivyo, TFF, TPLB na FRAT hawana budi kuongeza makali zaidi kwa waamuzi wanaozifinyanga sheria 17 za soka kwani lengo letu ni kutaka kuona anapatikana bingwa aliyestahili na hata timu zinazoshuka daraja na zile za kucheza mechi za mchujo kuwania kubaki na kupanda Ligi Kuu, ziwe zile zilizostahili kutokana na maamuzi bora na si vinginevyo.

Tunaamini maamuzi mengi ya ovyo yanayofanywa na waamuzi wetu si makosa ya kibinadamu kama mara kadhaa inavyodaiwa, bali wanadhamiria kwa sababu zao binafsi, hivyo mzunguko huu wa pili TFF na TPLB zisilale maana ndicho kipindi ambacho uvurundwaji mkubwa hufanyika.

Lakini umefika wakati kwa waamuzi wetu kujitathmini wenyewe kwamba wanatosha kuifanya kazi hiyo na kuanza kubadilika ili kuwa miongoni mwa wale wanaopewa nafasi mara kwa mara ya kuchezesha michuano ya kimataifa kama zilivyo nchini jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Sudan.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Morocco na somo la bure soka la Tanzania

**NCHI** ya Morocco imeingia kwenye rekodi ya kuwa ya kwanza kuipeleka Afrika kwenye michuano ya Kombe la Dunia ambayo inaendelea kutimua vumbi nchini Qatar.

Inawezekana ikachukua muda mrefu kwa Afrika kuweza kufikia tena rekodi iliyowekwa au inayoendelea kuwekwa na timu ya taifa ya nchi hiyo.

Mara ya mwisho timu ya Afrika kufika hatua ya robo fainali iliyokuwa ni miaka 12 iliyopita nchini Afrika Kusini wakati Ghana ilipofikia hatua hiyo na ingeweza kwenda nusu fainali kama ilivyokuwa kwa Morocco kama si Luis Suarez kuukamata mpira uliokuwa unaelekea wavuni kwa makusudi na kuzaa penalti ambayo ilikoswa na Asamoah Gyan. Hiyo ilikuwa 2010.

Timu zingine za Afrika ambazo zimeshawahi kutinga hatua ya robo fainali ni Cameroon ambayo iliweka rekodi ya kuwa ya kwanza kufanya hivyo barani humo mwaka 1990, michuano iliyofanyika nchini Italia.

Miaka 12 baadaye, 2002, timu nyingine ya Afrika, Senegal ilifanya hivyo kwenye michuano iliyofanyika nchi za Korea Kusini na Japan.

**Miaka 12 baadaye, 2002, timu nyingine ya Afrika, Senegal ilifanya hivyo kwenye michuano iliyofanyika nchi za Korea Kusini na Japan.**

Hapa tunaona ni miaka 32 sasa imepita ndiyo Afrika imepata timu nne zilizoweka rekodi ya kukumbukwa kwenye michuano hiyo, timu tatu zikitinga robo fainali na moja ikivuka hapo zilipokuwa zinakomea, Morocco ikienda nusu fainali.

Inawezekana ikaonekana kama imebahatisha, lakini ukifuatilia kwa undani unaona kabisa kuwa Morocco kwa sasa ndiyo inatawala soka la Afrika.

Tukianza kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, timu ya Wydad Casablanca, kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, bingwa wake ni RS Berkane na Ligi ya Mabingwa kwa soka la wanawake pia ni AS FAR ya Morocco.

Hapo unaona kabisa kuwa hawakubahatisha, ni mpango wa muda mrefu na mfupi ambayo ilipangwa kitaalamu mpaka kufikia hapo.

Tukirudi kwenye Timu ya Taifa ya Morocco, tunaona kuwa wachezaji wake wengi si wazaliwa wa nchi hiyo, badala yake wana uraia wa nchi mbili. Wengi wana uraia pia wa Ufasansa hadi kocha wao na mmoja amekulia Hispania.

Hii tumeiona hata kwenye Timu za Taifa za Comoro na Madagascar kwenye michuano ya AFCON, ambapo waliwaita wachezaji wanaocheza madaraja ya chini tu nchi za nje, lakini walikuja kutetemesha na kuzifanya nchi zao kufanya vema.

Inaonyesha kuwa siku hizi nchi za Afrika kama hawana mpango wa muda mrefu, basi watafanya mipango ya muda mfupi kwenye timu zao za taifa.

Mpango wa muda mrefu ni kutengeneza shule za soka, miundombinu kama viwanja, vifaa vya mazoezi na hata kuwapeleka vijana kulelewa kwenye 'akademi' mbalimbali nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya taifa baadaye.

Kama nchi ikiona inachelewa inawatafuta wachezaji wenye asili ya nchi walio nje ya nchi, kwa sababu wenzetu wana uraia wa nchini mbili na wachezaji wengi hawaitwi kwenye timu za huko wanakoishi, wanaamua kuchezea nchi zao za asili.

Ukiangalia Morocco wanaonekana hawa wana mipango ya aina zote mbili. Ndiyo maana hata klabu zao zinapata mafanikio. Wanatengeneza wachezaji wazuri nchini kwao, lakini wanachukuwa wachezaji nje ya nchi kwa ajili ya kulitumikia taifa.

Hili liwe somo hata hapa kwetu. Tumekuwa hatuna mipango ya muda mrefu, lakini hatuna ya muda mfupi. Timu ya Taifa, Taifa Stars, inaendeshwa zaidi na Kamati za Ushindi na hamasa kuliko uhalisia wa timu yenyewe. Hatuwaandai vema vijana kitaalamu na kuwa washindani zaidi ya kuwa waburudishaji tu.

Nadhani sasa umefika wakati kwa serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na uraia pacha hata kwa wanamichezo tu, kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa.

Wale wachezaji wa Morocco kuna baadhi hata nchi yao hawaijua vizuri, lakini sifa zote zinakwenda kwa nchi husika, kwa nini nasisi tusifikirie kufanya hivyo kuwapata wanamichezo tu?

Tanzania ina wachezaji wengi tu nje ya nchi, lakini wanatatizwa na suala ya uraia pacha. Tukumbuke, tukiwapa hao na kuifanyia kazi nzuri Tanzania, sifa itakuwa kwa nchi nzima kama ilivyo kwa Morocco.

## ‘Wanaume mnaofanyiwa ukatili na wenza jitokezeni’

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

OFISA Maendeleo ya Jamii mkoani Morogoro amewataka wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, ikiwamo kunyimwa unyumba na chakula na wenzi wao, wajitokeze kutoa taarifa ili kupatiwa msaada.

Delfina Pacho ameonya kuwa kuendelea kuficha vitendo hivyo kunaweza kusababishia magonjwa mbalimbali, yakiwamo ya sonona na yasiyoambukiza hususani shinikizo la damu.

Alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki mjini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto na Wanawake.

Alisema wanaume wanaofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili na wenza wao, wanao wajibu wa kufunguka kwenye madawati ya jinsia na watoto juu ya vitendo wanavyofanyiwa ili kusaidiwa pamoja na kuchukuliwa hatua dhidi ya wanaohusika.

Ofisa huyo alisema wanaofanyiwa vitendo vya ukatili si watoto na wanawake pekee, bali lipo kundi la wanaume ambao wamekuwa wakifanyiwa ukatili huo na wenzi wao kutokana na hali zao kuwa duni na kushindwa kuendesha maisha yao na familia na kujikuta wakitegemea wenzi wao.

“Wanaume wanaofanyiwa vitendo hivyo zaidi ni wale wenye vipato duni pale wanapoishi na wenza wao ambao wana uwezo mkubwa kiuchumi, wanatumia uwezo huo kuwanyima chakula na unyumba. Sasa tunawashauri watoe taarifa ili wapewe ushauri nasaha na wahusika wachukuliwe hatua,” alisema.

Pacho aliongeza kuwa vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa mara kwa mara na wenza wao, vinasababisha baadhi yao kupatwa na magonjwa mbalimbali ukiwamo wa sonona, na yasiyoambukiza hususani shinikizo la damu kutokana na msongo wa mawazo uliopitiliza.

Akitoa tamko la serikali kuhusu Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto na Wanawake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Mussa Ali, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia yamepungua kutoka 347 kwa mwaka 2021 hadi 303 mwaka huu mkoani hapa.


Katibu Tawala huyo alisema mkoa unaendelea na jitihada zaidi kupunguza vitendo hivyo kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na kupinga ukatili.

Alifafanua kuwa kati ya matukio 303 yaliyoripotiwa mwaka huu, 56 ni ya ubakaji, 50 ulawiti na 38 ni ya mimba kwa wanafunzi.

Mengine na idadi yake katika mabano ni utoro kwa wanafunzi (38), shambulio la aibu (24), kutorosha wanafunzi (11), kujaribu kubaka (14), kujeruhi (18), wizi wa mtoto (1), shambulio la kawaida (26), shambulio la kudhuru mwili (10) na kufanya mapenzi na wanafunzi (7).

Alibainisha kuwa kati ya matukio hayo, 161 yamefikishwa mahakamani huku 35 yakitolewa hukumu na mengine 119 yako katika uchunguzi na matukio 26 yamefutwa.

“Matukio yote haya, hasa ya kingono yamefanyika kwa kiasi kikubwa kwa watoto na wanawake,” alisema.




Mwanafunzi bora wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Goodluck Abel Kombe (wa pili kulia), akipokea hundi ya Sh. milioni moja kutoka kwa Meneja Mkuu, Uhasibu na Fedha wa Kampuni ya Simba Supply Chain Solution (SSCS), Hasnain Abbas (wa pili kushoto), iliyokabidhiwa na Mkurugenzi Uthibiti wa Barabara kutoka Mamlaka ya Uthibiti Usafiri Aridhini (Latra), Johansen Kahatano (wa tatu-kulia) katika kongamano la tisa la wana-alumni wa chuo hicho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampasi mpya kuanzishwa mafunzo ya usafiri wa reli

**Na Prosper Makene**

UONGOZI wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) umesema upo kwenye mipango ya kuanzisha kampasi mpya mkoani Tabora itakayotoa mafunzo ya reli ili kuendana na kasi ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali katika eneo hilo.

Naibu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Prosper Mgaya, alibainisha mpango huo mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa kongamano la tisa la wahitimu wake, mwaka huu likihudhuriwa na zaidi ya wahitimu 2,700.

Alisema kampasi hiyo inaanzishwa kwa msaada wa serikali ili kuzalisha wahitimu wa kutosha ambao watakidhi mahitaji katika eneo la usafiri wa reli.

“Tupo karibu kabisa kuanzisha kampasi hiyo mpya ambayo itakuwa mahususi katika kutoa mafunzo usafiri wa reli, yakifadhiliwa na serikali,” alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa chuo kipo kwenye mazungumzo na Shirika la Reli (TRC) lililoko chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili kuanzisha kampasi hiyo, akisisitiza itakuwa na tija kwa taifa.

Dk. Mgaya alisema NIT wanajitahidi kutoa wanafunzi wenye weledi kwenye njia tano za usafirishaji, ambapo mwaka huu mada yao kuu ipo kwenye usafiri wa reli na wamefanya hivyo kwa kuzingatia serikali inavyoweka fedha nyingi katika usafiri wa reli.

Alisema ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambao umefikia kwa asilimia 95 na mabehewa yameshaingia, ni uthibitisho tosha wa uwekezaji huo wa serikali kwenye eneo hilo.

Dk. Mgaya aliongeza: “Na kama mlivyosikia, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amesema nchi yetu imekaa kwenye eneo la kimkakati ambayo nchi za Congo na Burundi zinategemea nchi yetu, ndiyo maana reli zitajengwa hadi kwenye hizo nchi ili tusafirishe mizigo kuja Tanzania.”

Alisema anaamini ndani ya mwaka mmoja mafunzo hayo yatakuwa yameanza kutolewa, huku wakitarajiwa kupokea ndege mbili za mafunzo mengine ya urubani.

Kabla ya kutolewa kwa tuzo kwa wanafunzi bora, Dk. Mgaya alisema: “Ninawapongeza wahadhiri wote, wakufunzi na wafanyakazi wengine wote kwa kufanya juhudi kubwa kwa kutoa elimu bora na mafunzo yaliyotukuka na kuwafanya wahitimu hawa kumaliza masomo yao vyema,” alisema.

Aliwapongeza wanafunzi bora kwa mafanikio makubwa waliyoyapata ambayo yasingewezekana bila msaada wa wazazi, walezi, wadhamini na marafiki.

Mkurugenzi Uthibiti wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Johansen Kahatano, alisema chuo hicho kinaendelea kutanua wigo wa mitaala kwa kufikia maeneo mengi ya usafirishaji.

Mwenyekiti wa NIT Alumni, Dk. Amon Mwasandube, alisema dhamira kuu ya kongamano hilo ni kuhamasisha wanachuo waliosoma na wanajumuiya wa NIT wenye mapenzi mema, kuendelea kutoa msaada wa hali na mali kwa chuo.

Baadhi ya wanajumuiya ya NIT Alumni walisema wanajivunia kusoma kwenye chuo hicho.

“Tunawaomba wazazi na vijana wa kitanzania kuchangamkia fursa ya kupata mafunzo haya. Kozi hizi zitawatengenezea mazingira mazuri ya kupata ajira na kujiajiri,” alisema Shubira Mwakyoma, mhitimu wa NIT ambaye sasa ni mhandisi wa matengenezo ya ndege wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**12.12.2022**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi ) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **13-12-2022** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA** gari hizo zina namba za usajili:

**T 681 DUB /T 881 EAU** | **T 454 DYG /T 877 EAU** | **T 460 DYG /T 879 EAU**
**T 905 DSD /T 146 CHN** | **T 684 DUB /T 385 DHQ** | **T 990 DTN /T 137 CHN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20** **Upana - mita 5.55** **Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM** hadi **TUNDUMA** kupitia **MOROGORO ROAD.**

Gari zitasafiri muda wa usiku (**Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri**) Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Mlandizi
Kutoka Mlandizi kwenda Uyole gari zitasafiri muda wa mchana ( **kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)
Kutoka Uyole Mpaka Mbalizi Gari zitasafiri muda wa usiku (**Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri**)
Kutoka Mbalizi kwenda Tunduma gari zitasafiri muda wa mchana (**kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

17189702

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya SENGEREMA kituo cha KASENYI mkoa MWANZA**
**Usimamizi wa mirathi Na 07/ 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: CHARLES JUMA NOMOLOMO wa NYAMAZUGO(W) SENGEREMA.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARTHA MALANDO NG’HINDA.**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni ya usimamizi wa mirathi mahakama ya mwanzo**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu ,wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo TAREHE 15 Mwezi 12 Mwaka 2022 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kulete mahakamani kukaguliwa.
Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo 02 Mwezi 12 Mwaka 2022.

.........................................
**HAKIMU**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

SALUM J ABDALA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya TVS yenye usajili namba **MC 120 DBS**, CHASSIS NAMBA: **MD625AF4XMIE17079** na ENGINE NAMBA: **DF4EM1611555.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **LIN/LIN/RB/428626/2022**

**KUPOTEA KWA KADI YA GUTA**

**TANZANIA CHINA COMPANY LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi ya Guta yenye namba za usajili **MC 356 DMQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/475764/2022.**

# 'TAKUKURU isifumbie macho wanasiasa wanaonunua uongozi'

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutowafumbia macho wanasiasa wanaonunua uongozi.

Elia Digha ameonya kuwa kadhia hiyo isipochukuliwa, itakuwa na madhara makubwa kwa taifa.

Akizungumza juzi wakati wa Mdahalo wa Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Digha alisema rushwa imekuwa janga kubwa kwa nchi.

"Niwaombe ninyi TAKUKURU mnaosimamia suala la rushwa, simamieni vizuri, msiruhusu kabisa wanasiasa kununua uongozi, wanatupotosha. Hili ninalizungumza mimi ambaye ni mwanasiasa, ninayaona yanayofanyika," alisema.

Digha alisema kama kila mtu atatimiza wajibu wake, suala la rushwa halitakuwapo nchini, akisisitiza TAKUKURU wanao wajibu mkubwa wa kuhakikisha vitendo vya rushwa vinadhibitiwa ili nchi iendelee kupiga hatua kimaendeleo.

Ofisa wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Lumemi Kisonga, alisema wananchi wanatakiwa kuonyesha uzalendo kwa kufichua vitendo vya rushwa kwa kutoa taarifa kwa taasisi hiyo ili hatua zichukuliwe kwa wahusika.

"Ukiibiwa TV unakwenda polisi kutoa taarifa lakini ukiona vitendo vya rushwa huendi TAKUKURU, huu sio uzalendo kabisa! Wananchi tubadilike, tutoe ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa," alihimiza.

Kisonga alisema maendeleo yaliyoko na yanayoonekana kwenye mikoa mingine, yanawezekana kupatikana hata kwenye Mkoa wa Singida iwapo suala la uzalendo litapewa kipaumbele kwa kuacha kuhujumu miradi ya maendeleo.

"Unayesomea mfano uhasibu, jiandae uwe na uwezo wa kuaminika serikalini ili watu wakuamini watakapokupa majukumu. Kama huwezi kuwa mwaminifu, hata mapambano dhidi ya rushwa huyawezi," alionya.

Kisonga alisema tamaa ya mali, ubinafsi, uchu wa madaraka na kupenda njia za mkato vimekuwa chanzo kikubwa kwa baadhi ya watu kujiingiza katika vitendo vya rushwa.



Mwenyekiti wa Lions Club ya Dar es Salaam Infinity, Lion Nafisa Khanbhai (kushoto), akikabidhi zawadi ya taulo za kike kwa mmoja wa wasichana wa Halmashauri ya Chalinze, pia walitoa zawadi mbalimbali kwa kinamama waliojifungua na wajawazito katika Hospitali ya Msoga Chalinze. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC ataka ushirika usaidie utoaji wa huduma za jamii

**Na Jumanne Juma**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, amevitaka vyama vya ushirika kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kuisaidia jamii kuboresha huduma za afya kwa kutoa vifaa tiba na dawa.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa akikabidhi mashuka 300 yenye thamani ya Sh. milioni 11 yaliyotolewa na Chama cha Kuweka Akiba na Mikopo (SACCOS) cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

"SACCOS zingine zinatakiwa kuiga namna nzuri ya uendeshaji wake kwa sababu hiki ni chama kilichoamua kuisaidia jamii kwa vitendo," alisema.

Ludigija alisema serikali imefanikiwa kufanya maboresho mbalimbali kwenye hospitali hiyo ikiwamo upatikanaji wa vifaa tiba, hivyo ni muhimu chama hicho na vingine kusaidia huduma za mama, baba, vijana, wazee na watoto.

Alisema msaada waliioutoa TANESCO SACCOS katika taasisi hiyo utaongeza ari kwa wafanyakazi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwa mazingira yataboreka zaidi. "Kwa namna wagonjwa tunaowapata hapa Ocean Road, mashuka haya yatawasaidia sana watumishi wetu katika kuwahudumia kwa ukaribu wagonjwa, kuwabadilishia mashuka mara kwa mara kwenye mazingira kama yale yanayofanana na nyumbani kwani ni tiba kubwa," alisema.

Mwenyekiti wa TANESCO SACCOS, Somoe Ismail, alisema usambazaji wa vifaa hivyo ulianza mkoani Mtwara kisha Kilimanjaro na Geita na sasa wapo Dar es Salaam, huku mpango ukiwa ni kufikisha huduma nchi nzima kusaidia kuboresha huduma.

# Serikali yayaonya mashirika dhidi ya biashara ya watoto

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imesema itayachukulia hatua kali za kisheria mashirika binafsi yatakayobainika kujihusisha na biashara ya watoto badala ya dhamana yaliyopewa katika uendeshaji wa makao ya watoto na nyumba salama.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju, alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao kazi kati ya serikali na wadau wa Jukwaa la Kitaifa la Malezi Mbadala ya Watoto mjini Morogoro.

Alisema yapo makao ya watoto 325 yamesajiliwa yakiwamo mawili ya serikali yenye jumla ya watoto 9,011 (wavulana ni 4,897 na wasichana 4,114).

Wakili Mpanju alisema serikali imelazimika kutoa onyo hilo kutokana na kuwapo taarifa za vitendo vya baadhi ya makao na nyumba hizo kujihusisha na biashara ya watoto kwa maslahi yao binafsi.

"Makao nyumba ni vituo mbadala na kimbilio la watoto, kuna watu wanaofanya kwa nia ya makao ya biashara kwa maslahi yao binafsi, sasa tukimbaini anayefanya hivyo, huyo tutamchukulia hatua kali sana na atakuwa mfano kwa wengine," alisema Mpanju.

Naibu Katibu Mkuu huyo alimwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii pamoja na wadau kuhakikisha makao ya watoto na nyumba salama zinazosajiliwa, zinaendeshwa kwa kuzingatia miongozo, kanuni na sheria za nchi.

"Msitumie nafasi hiyo kwa maslahi binafsi kwa sababu lengo la serikali ni kuhakikisha makao na njia zote mbadala zinalenga kumlinda mtoto na kumwendeleza kwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2019," aliagiza Wakili Mpanju.

Alimwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii na watendaji wengine wa wizara hiyo ngazi za wilaya na mikoa kuhakikisha makao ya malezi mbadala yaliyoko kwenye maeneo yao yanafuatiliwa ili yasiwe sehemu ya manyanyaso kwa watoto, kufanyiwa ukatili na wengine kugeuzwa bidhaa za biashara.

Alimwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha makao takriban 98 yaliyotambuliwa kuendesha shughuli zake bila leseni na yale ambayo hayajatambuliwa, wamiliki wapewe utaratibu wa kiserikali wa namna ya kuyaendesha ili wauzingatie.

"Wapeni utaratibu wa kiserikali tulioweka na kama hawataweza kuutekeleza, makao hayo yafungwe mara moja na watoto waliopo watafutiwe makao yaliyo karibu nao wapelekwe yakiwamo ya serikali ambayo pia yana nafasi," aliagiza.

Wakili Mpanju alisema serikali imeendelea kuratibu huduma ya malezi ya kambo na kuasili ambapo kwa kipindi cha 2020/21 wizara ilipokea maombi 110.

Alisema jumla ya watoto 40 waliwekwa kwenye malezi ya kambo na watoto 50 waliasiliwa wakiwamo wa kiume 28 na wa kike 22 kulinganishwa na maombi 131 ambapo jumla ya watoto 48 kati yao wakiume 21 na wa kike 27 waliwekwa kwenye malezi ya kambo na watoto 56 waliasiliwa kati ya hao wakiume 17 na wa kike 39 kwa mwaka 2021/22. Aliomba Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kutumia mifumo madhubuti ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) itakayosaidia kuweka takwimu sahihi kwa kuwabaini watoto wanaohitaji malezi mbadala.

Wakili Mpanju alisema suala la malezi mbadala linapaswa kuwa la mpito kwa kuwa anaamini kuwa kila mtoto aliye ndani ya jamii ana mlezi wake, hivyo Jamii isichululie suala la malezi mbadala kama suluhisho la kudumu.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mariam Nkumbwa, alisema ofisi hiyo itaimarisha mifumo ya ufuatiliaji na shughuli zote za malezi ili ziingie kwenye mipango ya bajeti na kuimarisha ushiriki wa wadau kwa lengo la kuwa na takwimu sahihi.

Mratibu wa Malezi Mbadala Kitaifa kutoka Shirika la SOS Children's Villages, Onesmo Itozya, alisema usalama wa watoto wa leo ndiyo usalama wa taifa la kesho.

Alisema SOS wamekuwa nchini kwa zaidi ya miaka 30, wakisaidia shughuli mbalimbali na bado wanaona ipo haja suala la malezi mbadala kupewa kipaumbele.

"Ninafurahi tukiwa tunatimiza miaka 61 ya Uhuru kwa mara ya kwanza tunakuwa na jukwaa la pamoja la kujadili masuala ya malezi mbadala, hii haijawahi kutokea, hivyo tutatumia fursa hii kutoka na afua zitakazolinusuru taifa na watu waliokosa malezi bora," alisema Itozya.

Awali akitoa salamu za Mkoa wa Morogoro, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Wahida Ntiro, aliiomba wizara kuongeza wataalamu wa ustawi wa jamii kwenye ngazi za mikoa na halmashauri ili kuepusha shughuli hizo kutokukwama.

## MECIRA yajitosa utunzaji vyanzo vya maji, mazingira

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Wanahabari, Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA) kimeandaa kongamano litakalokutanisha wadau wa maendeleo, mazingira, uhifadhi na utalii kwa ajili ya kujadili umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji na uhifadhi wa mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar er Salaam jana, Mwenyekiti wa MECIRA, Habib Mchange, alisema kongamano hilo linatarajiwa kufanyika Desemba 19, mwaka huu, mkoani Iringa na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema chama chao kimeamua kukutanisha wadau hao ili kujadiliana na kuja na mawazo mbadala namna ya kuelimisha wananchi kudhibiti uharibifu huo wa mazingira na vyanzo vya maji kwa kuwa athari zake zinapokuja hazichagui itikadi ya mtu.

"Sisi kama Watanzania, tuna wajibu wa kulinda mali zetu, tumeona kwamba tukiendelea kusubiri serikali pekee ifanye huku tumekaa tukiangalia, hali hii ya uharibifu wa mazingira inaendelea kama ilivyo sasa, tutajikuta tunaendelea kulaumu tu huku athari ikiongezeka.

"Kwa hiyo, sisi kama MECIRA, tumeamua kuchukua hatua badala ya kuwa sehemu ya wanaolalamika, tutumie taaluma zetu kubadili mitizamo ya wananchi kuhakikisha jamii inaamka na inashiriki katika kuhifadhi, kutunza na kutetea rasilimali zake.

"Tunataka mwananchi anayelima kwa mfano kando ya Mto Ruvu au Ruaha ambaye huenda hajui kwamba anaharibu mazingira, ajue sasa. Kwa hiyo, sisi kama wanahabari tutafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wataalamu wa mazingira, kilimo, mifugo, kuwaonyesha kwamba ni namna gani wanatakiwa wawaambie wananchi kwamba katika eneo fulani hawatakiwi kulima na sehemu gani hawatakiwi kuingiza mifugo.

"Tunataka tuwe wanahabari ambao kupitia kazi zetu tunaleta tija katika jamii na taifa letu kwa kutoa elimu iliyo sahihi juu ya suala hili, nchi yetu ni miongoni mwa mataifa yanayoumia sana na suala la uharibifu wa mazingira, tushirikiane tutengeneze uelewa kwa wananchi," alisema.

Mdau wa Uhifadhi, Manyerere Jackton alisema ni wajibu wa waandishi wa habari kujipambanua badala ya kuwa sehemu ya watu wanaolalamika, kutumia kalamu zao kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kutunza mazingira hayo.

"Mazingira yanapoathirika, hayachagui mtu, sisi sote tunaathirika. Leo hii kuna mgawo wa umeme, watu wote wanaathirika bila kujali itikadi ya mtu, kwa hiyo tumeona sisi kama wanahabari tulete mabadiliko chanya katika suala hili la kutunza na kuhifadhi mazingira yetu kwa sababu tunao wajibu huo wa kushirikiana na serikali kuelimisha jamii," alisema Manyerere.

Ofisa Mawasiliano wa MECIRA, Hamisi Mkotya, alisema waandishi wa habari wana wajibu wa kupaza sauti kusemea jambo hilo kama ambavyo wamekuwa wakifanya katika mambo mengine ili kupambana na uharibifu huo wa mazingira na vyanzo vya maji.

# Matapeli wawaliza wastaafu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KUMEIBUKA wimbi la matapeli wanaojitambulisha kuwa watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango, wakipiga simu kwa watu waliokwishalipwa mafao na mifuko ya hifadhi ya jamii kuwaambia serikali inatarajiwa kuwalipa kiwango walichopunjwa baada ya kufanya uhakiki upya.

Matapeli hao wanadaiwa kuwa wanapowapigia simu wastaafu, wanawaeleza kuwa malipo ya mafao waliyopunjwa, serikali itawalipa kwa awamu tatu tofauti na fedha hizo zitaingizwa moja kwa moja kwenye akaunti zao.

Kwa mujibu wa wastaafu waliopigiwa simu na matapeli hao, walipewa taarifa serikali ilianza kulipa fedha hizo mapema mwaka huu na imeshalipa awali ya kwanza na ya pili na awamu ya tatu ilitarajiwa kuanzia Novemba 5 hadi Novemba 30 mwaka huu.

Matapeli hao wamekuwa wakiwataka wastaafu waliostaafu kwa ugonjwa ili fedha hizo ziweze kutoka haraka serikalini, waende kwa mawakili kwa ajili kula kiapo na kutoa Sh. 30,000 lakini baada ya kutekeleza maelekezo hayo cha kushangaza fedha hazijaingizwa kwenye akaunti zao kama walivyoahidiwa. George Bwemolo, ni mmoja wa wastaafu aliyepigiwa na simu na matapeli hao mwanzoni mwa mwezi uliopita, alidai kuwa alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha ni Boniface ... (jina la pili tunalihifadhi) kwamba ni mtumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango. Bwemolo ambaye alistaafishwa kutokana na tatizo la macho, alisema mtu huyo (tapeli) ambaye alitumia namba 0674860... (namba za mwisho tunazo) alimweleza kuwa katika mafao aliyolipwa na Shirika la Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) alipunjwa.

Alisema mtu huyo alimweleza kwamba serikali imefanya uchunguzi na kubaini alivyopunjwa mafao na wenzake waliostaafu na hivyo imeamua kuwalipa wastaafu wote waliopunjwa na fedha zitatolewa na Wizara ya Fedha na Mipango yenyewe na siyo kuzipitishia katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema katika hali ya kushangaza ilipofika Novemba 30, alipoulizia benki kama kuna fedha zake zozote zimeingizwa katika akaunti yake aliambiwa hakuna na alipojaribu kumpigia simu mtu aliyempa taarifa hiyo, simu yake imekuwa ikiita bila kupokewa. Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja amewatahadharisha wastaafu kuwa makini na wimbi la matapeli wanaotoa taarifa za uongo kwa lengo la kujipatia kipato kwa njia zisizo halali.

Mwaipaja alisema wastaafu wawe makini na matapeli kwani serikali ina utaratibu wake mzuri wa kutoa taarifa kwa wastaafu, hivyo suala la watu wanaowapigia simu kwamba walipunjwa mafao na sasa serikali itawalipa ni uongo kwa kuwa wizara hiyo hailitambui.

Alisema matapeli wamekuwa wakitumia kila njia kuwaibia wastaafu na kwamba wanapowatilia shaka watu wanaowapigia simu, wasisite kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili hatua zichukuliwe dhidi yao.



Mkurugenzi Msaidizi wa Biashara, Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji, Athuman Nkungu, akiangalia bidhaa ya mmoja wa wajasiriamali alipotembelea meza yake kwenye maonesho ya 22 ya Juakali yanayoendelea katika Viwanja vya Uhuru vya Kololo jijini Kampala, Uganda. **PICHA: MAMBO YA NJE**

# Mwinyi apokewa kwa shangwe visiwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana amepokewa kwa shangwe na nderemo visiwani hapo baada ya kuwasili kutoka Dodoma ulikofanyika Mkutano Mkuu wa chama hicho na uchaguzi.

Mwinyi alipokewa katika Viwanja vya Ndege vya Abeid Amani Karume kwa burudani ya vikundi mbalimbali vya ngoma.

Akiwa katika gari la wazi, aliwalaki wananchi na wanachama mbalimbali waliokuwa wamesimama katika Barabara ya Uwanja wa Ndege hadi Ofisi Kuu za CCM, Kiswanduni.

Mapokezi hayo yalitawaliwa na wanachama waliovalia mavazi ya rangi za njano na kijani yakiambatana na burudani huku baadhi ya shughuli za kijamii zikisimama kwa zaidi ya saa sita.

Mwinyi ambaye ni Rais wa Zanzibar alipowasili katika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui, alikabidhiwa rasmi Ofisi yake na kusaini kitabu maalum na kisha kuzuru kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume.

Akizungumza na wanachama wa chama hicho, Dk. Mwinyi aliwataka wananchi kuendeleza hali ya amani na usalama katika nchi.

Alisema hakuna mbadala wa amani na usalama katika nchi na kuwataka viongozi wa siasa, dini na wananchi kuendelea kuhubiri amani kwa kuwa itakapokosekana hakutakuwa na uchumi wala maendeleo yoyote.

"Nayasema haya kila mara kwa sababu kuna viashiria vya uvunjifu wa amani na kauli zinazotelewa na baadhi ya viongozi wa kisiasa zinazoashiria uvunjifu wa amani hivyo wana CCM endeleeni kuhubiri amani tusijibu wala tusichokozeke," alisema.

Dk. Mwinyi alisema umoja ni silaha muhimu katika chama na kwamba ni vyema kuwa wamoja kwa wale waliompigia kura na ambao hawajampigia na kuondoa tofauti ili kukijenga chama.

"Katika uchaguzi kule Dodoma kura tatu ndizo zilizonikataa sasa nasema wale walionipigia kura na ambao hawajanipigia kura tuwe wamoja kukijenga chama na kuondosha tofauti zetu," alisema.

"Waliochaguliwa wote kule Dodoma ndio timu ya ushindi ya mwaka 2025 kwa ngazi zote kuendelea kujipanga kushika dola katika chaguzi zinazofuata hivyo kuwa kitu kimoja na kutoendeleza makundi," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kazi iliyopo ni kukijenga Chama Cha Mapinduzi, kwa sababu kuna maeneo kadhaa ya ujenzi wa chama ikiwamo miundombinu kuwa bora zaidi katika ngazi zote lazima kuwa na ofisi za kisasa zinazoendana na ukumbwa wa chama, kuwa na vifaa vya kutosha na vyombo vya usafiri vinavyoendana na hadhi ya chama.

Alisema mafunzo kwa watendaji wa chama hicho yanahitajika kwa sababu viongozi wengi ni wapya wanahitaji kujua mahitaji yao hivyo kufanya mafunzo kwa watendaji, ikiwamo ya matumizi ya teknolojia ya kidijitali na chama kuendana na kasi kwa kuwa na kadi za kielektroniki.

Naye mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Hemed Suleiman Abdullah, alisema lazima viongozi wakijenge chama cha kusimamia serikali ili kufikia malengo.

"Majungu, fitina, wanaotaka vyeo havina nafasi kama umekuja kwa fitina na majungu hufai...ulichopewa kwanza kifanyie kazi, hicho ulichopewa hujakiweza sijui kama mkeka ukija utakuwamo," alisema Hemed ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais.

Alisema wapo baadhi ya wana CCM miongoni mwao ni viongozi wanapanga safu ya uongozi na wameanza kujipendekeza ili wapate vyeo hivyo njama zao zimeshajulikana kujiandaa vizuri na mabadiliko.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Abdallah Juma Sadallah, alisema chama kina utaratibu wa kupokezana kijiti cha uongozi kwa salama na amani na kimekamilisha hilo.

# TEF yaanza kuona mwanga mabadiliko Sheria ya Habari

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, amesema serikali imechukua sehemu kubwa ya mapendekezo ya wadau kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016.

Kutokana na hali hiyo, Balile amesema wadau wa habari nchini wanatakiwa kuwa watulivu wakati wakisubiri hitimisho la mchakato huo utakaoonyesha maoni yao yamefanyiwa kazi kwa kiasi gani.

Balile aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na mwandishi wa habari.

"Kwa hakika, sisi kama wadau wa habari tuna kila sababu ya kusema tumefikia hatua nzuri inayotufanya tuwe na matumaini chanya hasa baada ya kikao cha mwisho tulichokifanya na serikali jijini Dar es Salaam.

"Hatua inayofuata sasa ni ya serikali katika kuelekea mabadiliko ya sheria hiyo na kwa hatua tuliyofikia, tunaamini kuna jambo jema linakwenda kutokea," alisema Balile.

Kwa mujibu wa Balile, jambo linalotia moyo ni jinsi serikali ilivyoshirikisha wadau wote wa habari katika mchakato wa mabadiliko ya sheria hiyo ya habari.

"Kwa kuwa wadau wa habari tunapigania kitu kimoja, tuliamua kwa pamoja kujiweka chini ya mwamvuli tunaouita CORi ambao ni Umoja wa Wadau wa Kupata Habari.


"Kwa ujumla, umoja huo ulirahisisha mchakato wetu kwani tulikuwa na sauti moja na hivyo kuifanya serikali ijue inazungumza na watu gani na ninaamini kama tusingekuwa na umoja huo, inawezekana pengine mambo yasingekwenda kwa namna tulivyoona," alisisitiza Balile.

Wakati Balile akisema hayo, hivi karibuni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alizungumza na wadau wa habari jijini Dar es Salaam na kuwahakikishia serikali ina nia ya dhati ya kukamilisha mchakato wa mabadiliko ya vipengele vya sheria hiyo.

"Ninapenda niwahakikishie kwamba serikali inayo nia ya dhati katika jambo hilo na ndiyo maana katika mkutano huu nimekuja mwenyewe kuwasikiliza na imani yangu ni kuona sekta ya habari inaendelea kukua," alisema Nape.

Baadhi ya vifungu vyenye utata ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa na wadau wa habari katika sheria hiyo ni kifungu cha tano ambacho kinampa mamlaka makubwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) katika utekelezaji wa majukumu yake wakati wa kuvisimamia vyombo vya habari.

Vifungu vingine vinavyolalamikiwa ni vya 7(2) (b) (iv), 11, 12, 13, 14, 15, 16, 17, 18, 19, 20, 21 na kifungu cha 23.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa pili kulia), akikabidhi zawadi ya televisheni janja kwa Sophia George baada ya kuibuka mshindi katika wiki ya pili ya Kampeni ya Amsha Ndoto, Amsha Shangwe ya Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Masta Shangwe na (kulia) kwa mshindi ni Kaimu Mkuu wa Vodacom Kanda ya Kati, Andrew Temu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yasifu kuimarika kwa uhuru wa kujieleza nchini

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

DUNIA juzi iliadhimisha Siku ya Haki za Binadamu huku Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikiipongeza serikali kwa kuanza kuboresha mazingira ya haki za binadamu, ikiwamo uhuru wa kujieleza na kutoa maoni.

Kila mwaka tarehe 10 Desemba ni siku ambayo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha mwaka 1948 kuwa ya haki za binadamu kupitia Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu (UDHR).

Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa wa CHADEMA, Mch. Peter Msigwa, alibainisha kuanza kuimarika kwa uhuru wa kujieleza na kutoa maoni alipozungumza wakati wa kongamano lililofanyika mjini Iringa.

Alisema serikali duniani kote ina wajibu wa kuhakikisha inalinda haki za raia wake, ikiwamo haki ya kuishi, kukusanyika, kutoa maoni na nyinginezo.

Mch. Msigwa alisema hali ya kujieleza hapo nyuma ilikuwa siyo ya kuridhishwa lakini kwa sasa mambo yameanza kubadilika katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita.

Mch. Msigwa pia alifafanua kuwa Siku ya Haki za Binadamu huadhimishwa kila tarehe 10 Desemba ili kujenga uelewa na kuhamasisha utashi wa kisiasa ili kukuza heshima kwa haki na uhuru zilizoainishwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1948.

"Kaulimbiu ya 2022 ya Siku ya Haki za Kibinadamu ni Utu, Uhuru na Haki kwa Wote," alisema.

Kiongozi huyo aliitaka serikali kuendelea kuboresha haki mbalimbali zikiwamo ya afya na siasa ili kuendelea kufanya mikutano ya hadhara, hivyo kudumisha uhuru na umoja wa kitaifa.

"Haki ya afya inahusu kuhakikisha kwamba kila mtu, kila mahali anaweza kupata huduma za afya za bei nafuu.

"Pia inategemea usawa wa kijinsia na utambuzi wa haki nyingine za binadamu ikiwa ni pamoja na chakula, elimu, nyumba na upatikanaji wa maji salama na usafi wa mazingira," alisema. Mch. Msigwa aliiomba serikali kuendelea kuboresha sera na sheria za haki za binadamu nchini ikiwamo haki ya kisiasa na demokrasia kwa maslahi mapana ya taifa kwa ujumla.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, John Heche aliyekuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo, aliitaka serikali kuongeza bajeti ya kilimo ili kupunguza kero zinazowakabili wakulima nchini.

Alisema serikali inatakiwa kuboresha mifumo ya kilimo nchini ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuondokana na utegemezi wa kuagiza chakula nje. Heche alisema serikali inatakiwa kuongeza bajeti ya kilimo ili kuchimba mabwawa, kuboresha miundombinu, kutengeneza maghala, kufanya utafiti wa mbegu bora na kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo pamoja na kuwatafutia wakulima masoko ya mazao.

# Mamilioni yatolewa kukarabati hospitali

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. milioni 900 kwa Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara kwa ajili ya kuanza ukarabati wa miundombinu ya majengo ya Hospitali ya Mkomaindo.

Kutolewa kwa fedha hizo kumelenga kuboresha utoaji wa huduma za afya wilayani Masasi.

Kutolewa kwa fungu hilo kulithibitishwa na wilayani hapa juzi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Elias Ntiruhungwa, wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya Miaka 61 ya Uhuru lililofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi mjini Masasi.

"Kama Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hii, ninapenda kuwaeleza wananchi kuwa wiki iliyopita ya mwezi huu wa Desemba, nimepokea Sh. milioni 900 kutoka serikali kuu ambazo maelekezo yake ni kwamba zitumike kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Mkomaindo Masasi," alisema.

Ntiruhungwa alisema hayo ni mafanikio makubwa yanayofanywa na serikali kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wananchi wake.

"Hospitali yetu imepata fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya majengo, fedha hizo zinakwenda kuifanya hospitali yetu kuwa ya kisasa," alisema. Ntiruhungwa alisema Wilaya ya Masasi ni miongoni mwa wilaya ambazo zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika uboreshaji wa miundombinu kuanzia sekta ya elimu, afya, barabara, umeme hadi maji ndani ya miaka 61 ya uhuru.

Alisema serikali zote zilizoongoza na hata iliyopo madarakani kwa sasa, zimefanya kazi kubwa ya kimaendeleo ndani ya wilaya yao na wananchi wanafurahia matunda ya serikali yao.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa zenye mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali za kijamii.

Kitta aliwataka wakazi wa Wilaya ya Masasi kuendelea kudumisha amani na upendo kwa kuwa ndiyo nguzo muhimu ya maendeleo, huku akiwataka kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo.

Ibara ya 8 ya Katiba ya Tanzania, Toleo la Mwaka 1977, pamoja na mambo mengine, inawataka wananchi kushiriki katika shughuli za serikali yao huku ikielekeza serikali kuwajibika kwa wananchi.





## Wananchi 5,000 wapima afya maadhimisho miaka 61 ya Uhuru

**Novatus Makunga,** ARUSHA

ZAIDI ya wananchi 5,000 wamejitokeza kupata huduma ya uchunguzi wa afya na matibabu bure, iliyotolewa na madaktari bingwa wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika.

Walionufaika na huduma hiyo ni wakazi wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, kati yao 465 walifaidika na dawa za bure na 465 kupata miwani ya bure.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Alex Ernest, huduma hiyo ilitolewa kwa wahitaji kwa siku nne, kuanzia Desema 5 hadi 9, mwaka huu.

"Idadi kubwa ya wananchi walijitokeza ni wenye magonjwa ya macho na uoni hafifu na ya ndani kama kisukari, shinikizo la damu na vidonda vya tumbo. Katika siku hizo walijitokeza wananchi 964, na kati yao wenye tatizo la macho na uoni hafifu walikuwa 465," alisema.

Jopo la madaktari bingwa 24 waliofanya kazi hiyo liliongozwa na Dk. Alex, walifanya vipimo 96 vya uchunguzi wa kitabibu, huku mafanikio makubwa yakiwa kwa wanawake 196 waliochunguzwa saratani ya shingo ya uzazi na matiti.

Dk. Alex alisema uchunguzi wa tatizo la mifupa, misuli na majeraha, walijitokeza watu 408, pua, koo na masikio (394), wanawake wenye matatizo ya uzazi (326) na magonjwa ya watoto (196).

Baadhi ya wananchi waliojitokeza wakiwamo Monica Nangasi, Mkazi wa Unga Limited na Noah Mwanga, Mkazi wa Olasiti Jiji Arusha, kwa nyakati tofauti waliipongeza serikali, kwa kutumia maadhimisho ya uhuru kutoa huduma ya uchunguzi na matibabu ya maradhi bure.

"Wasiishie hapa kwenye maadhimisho tu tunaomba utaratibu huu, uwe unafanyika angalau kila baada ya miezi mitatu, ili kuokoa maisha ya wananchi wasiokuwa na uwezo wa kiuchumi kufikia huduma za uchunguzi wa afya, na hasa maradhi yanayohitaji fedha nyingi kupata tiba," alisema.

# H'shauri Babati yamaliza mgogoro Hifadhi Burunge

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, imeingilia kati mgogoro unaofukuta wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (JUHIBU), baada ya kuamua kuirejesha madarakani Bodi ya Wadhamini iliyokuwa imevunjwa kinyume na utaratibu.

Pia imewarejesha kazini Katibu wa Jumuiya hiyo, Benson Mwaise na Mwenyekiti wa bodi, Hamis Juma, waliondolewa Novemba 18, mwaka huu na Baraza la Uongozi la Jumuiya hiyo (AA),

Uamuzi wa kuirejesha bodi hiyo, ulitangazwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Anna Mbogo, kwa kufafanua kuwa waliotekeleza kusudio ya kuwaondoa madarakani walivunja sheria inayosimamia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA).

"Kutokana na malalamiko ya wenyeviti wa vijiji na bodi ya wadhamini, kupinga uamuzi wa Baraza la Uongozi la Jumuiya hiyo (AA), waliiomba serikali na kuingilia kati mgogoro huo, nimeamua kuirejesha kazini kuendelea na majukumu yake, kwa mujibu wa sheria na kanuni za WMA," alibainisha.

Viongozi hao walisimamishwa kutokana na mgogoro wa uwekezaji katika kitalu cha uwindaji cha hifadhi hiyo ambacho kampuni ya EBN iliwekeza tangu 2013, kwa wao kupinga mkakati wa Mwenyekiti Hamis kuvunja mkataba.

Kwa mujibu wa barua ya Mkurugenzi huyo kwenda kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, yenye kumbukumbu, namba DED/BBT/L.3/1/38, (Nipashe imeona nakala yake), ameagiza bodi hiyo kurejea kazini kuendelea na majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kanuni za WMA.

Alifafanua kuwa kikao cha kuvunja bodi hiyo kilifanyika bila kushirikisha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Baraza la Ushauri wa Maliasili la Wilaya Babati na mamlaka zinazowajibika kisheria kuishauri JUHIBU.

Barua hiyo ilifafanua kuwa uamuzi uliofanywa na Baraza la AA, ulikuwa na maslahi binafsi ya Mwenyekiti wa JUHIBU, Hamis, na kuwa amejiridhisha pasipo shaka kwamba Baraza la AA, halina mamlaka kisheria, kuvunja bodi ya wadhamini iliyosajiliwa kisheria mwaka 2004, kwa usajili namba 2905 kwa Sheria ya Bodi ya Wadhamini ya mwaka 1956.

Mmoja wa Wajumbe wa Bodi ya JUHIBU, Lembice Makoa, akizungumza na Nipashe, alithibitisha kupokea barua na kurejea kazini na kupongeza uamuzi wa serikali kutatua mgogoro huo.

"Tunashukuru ofisi ya mkurugenzi na serikali kwa ujumla kwa kuingilia kati na kutatua mgogoro huu kwa kulinda maslahi mapana ya uhifadhi na utalii nchini, lakini pia maendeleo ya jumuiya yetu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wenyeviti wa vijiji 10 vinavyounda JUHIBU, Mwenyekiti wa Kijiji cha Vilima Vitatu, Abubakari Msuya, alisema wanapongeza serikali kurejesha bodi na kumsimamisha Mwenyekiti wa JUHIBU, Hamis.



Ofisa Mradi wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO, Haika Manase, akizungumza na wananchi wa Kata ya Kibosho Magharibi, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, mwishoni mwa wiki, kuhusu tishio la ukatili wa kijinsia linavyoathiri maisha ya wenye ulemavu. Mradi huo wa hukumu uwezo wangu na sio ulemavu wangu, unatekelezwa kwa ubia na Shirika la NAFGEM. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Katibu Tawala aonya utupaji taka ovyo

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Upendo Wella, amewaonya wananchi wa Mji Mdogo wa Mailisita, kuacha kupuuza agizo lake la kuacha kutupa taka ovyo huku akitangaza kutengwa eneo jipya la kujenga dampo la kisasa.

Aidha, amesema watakaokamatwa wakichafua mazingira wasimlaumu kwa hatua zitakazochukuliwa dhidi yao huku akitoa siku saba kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Shiri Njoro, Alifonsina Titus na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mnadani, Sembuli Mkilaha, kuwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Juma Irando, mpango kazi wa namna watakavyokusanya taka na kuzihifadhi sehemu salihi.

Wella alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, ambayo yalifanyika kwa kufanya usafi na kupanda miti maeneo mbalimbali.

"Sio kwamba sisi tunapenda kuja kufanya usafi hapa, tumekuja ili tuwape fundisho, kwa sababu kuwapo mrundikano wa uchafu hapa na wakati ninyi mpo inapendeza kweli?

Sio sawa kwa sababu kama mngekuwa mmefanya na kutimiza wajibu wenu, hili dampo hapa lisingekuwapo. Tumekuja hapa ili mshtuke kwamba mpaka viongozi wamekuja kutoka wilayani ikiwa na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama.

"Tumekuja kuleta ujumbe kwenu kwamba kuanzia sasa, hapa hatutaki kuona tena uchafu kwenye eneo hili.

Muweke utaratibu mzuri wa kutupa taka, siku hizi taka nayo ni fursa, ni ajira. Watu wanaajiriwa wanapata pesa kupitia taka.

"Ofisa Tarafa, Mtendaji wa Kata na Kijiji cha Shiri Njoro, wekeni utaratibu mzuri wa kuhifadhi hizi taka na sio kutupa hapa.

Tukipita tukikuta tena taka tutachukua hatua kali, na tukichukua hatua msitulaumu. Mimi naongea sauti ni hii hii (ya upole), lakini mkitupa taka hapa msije kunilaumu."


Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Dionis Myinga, aliwasisitiza viongozi hao kukutana na wananchi na kuweka mkakati wa kudhibiti taka zinazozalishwa nyumbani na soko la samaki la Mailisita ili kuepuka mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu na kuhara.

"Nimeambiwa mnataka kujenga dampo, leteni huo mpango tuuone kama unatekelezeka. Waelimisheni wafanyabiashara wa soko la samaki kwamba hii sio sehemu ya kutupa taka, lakini tuwaelekeze mahali pa kuzitupa,"alisisitiza Myinga.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Shiri Njoro, Alfonsina Titus, alithibitisha walikuwa na utaratibu wa kukusanya fedha kwa ajili ya uzoaji na utunzaji wa taka, lakini baada ya uwapo wa soko la samaki, makusanyo yalilegalega na ubishi kuongezeka.

"Jambo zuri ni kwamba tayari tumekubaliana wiki ijayo, tutakutana wote hapa kujadili hali iliyoko na kuja na mikakati ya kukabiliana na uchafu katika mji wa Mailisita.

Tutawaita wataalamu wa mazingira na ofisa afya wa wilaya, waje kutoa elimu kwa wananchi na kuliona eneo tulilopendekeza liwe dampo kama panafaa pawe ndio dampo la kudumu," alibainisha.





## Wakulima watakiwa kuacha matumizi makubwa viuatilifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MTAFITI kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Dk. Jones Kapeleka, amesema endapo wakulima wataacha utumiaji wa viuatilifu kwa viwango vikubwa kwenye mazao ya mboga na matunda, watapunguza madhara ya kiafya kwa walaji na uchafuzi wa vyakula.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati akifungua semina ya wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari, iliyoandaliwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Mkoani Arusha (MVIWAARUSHA), Taasisi za CARI, Iles de Paix na GAIN kuhusu mifumo endelevu ya chakula.

"Endapo wakulima watatumia kwa usahihi viutilifu hivyo watapunguza madhara kwa watumiaji wanayopata mwilini mwao yanayotokana na baadhi ya vyakula kuwa na viuatilifu, kama ilivyobainika katika utafiti uliofanywa mwaka jana, ambao ulibaini uwapo wa masalia ya viuatilifu katika mboga na matunda," alisema.

Dk. Kapeleka alisema kutokana na tatizo hilo juhudi kubwa zimeanza kufanyika za utoaji elimu kwa wakulima, juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu, ili kupunguza athari kwa binadamu na uharibifu wa mazingira.

Alisema ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anatumia viuatilifu kwa njia sahihi ili visilete madhara ikiwamo uboreshaji wa masoko ya chakula, ili kupata chakula salama.

Aidha, alisema ni lazima vyakula viandaliwe vyema na matumizi sahihi ya mboga na matunda kwa kuhakikisha wafanyabiashara sokoni wanaweka bidhaa zao sehemu salama na kutumia vitambaa vya kufutia matunda kuwa visafi, ili kutopakaza uchafu kwenye bidhaa hizo.

Pia aliwataka wanaosimamia masoko kuhakikisha usafi unaboreshwa ikiwamo wa majisafi na salama hasa katika matumizi ya kusafisha mboga au kuzinyunyizia maji, ili zisikauke na taka kuzolewa kwa wakati kuepuka kuzagaa na kusababisha madhara kwa walaji.

"Taka zinapozagaa ni hatari kwa afya za watu, kwani kwenye haya masoko yetu bidhaa nyingi zinapangwa chini hazipangwi kwenye meza, hivyo kujikuta watu wakila uchafu," alisema.

Alisema utafiti huo umefanywa katika mikoa inayolima na kutumia mboga ya Dar es Salaam, Iringa, Morogoro, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

## Mwalimu aanzisha kampeni kusaidia wanafunzi kaya maskini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWALIMU Easter Simba maarufu 'Hekima' ameahidi kuanzisha kampeni endelevu ya kuwasaidia wanafunzi wa shule za msingi za pembezoni wanaotoka kaya maskini wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro, kukabiliana na tatizo la utoro linalosababishwa na kukosa fedha za kununua taulo za kujisitiri.

Hekima ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la UWEZA Foundation, aliahidi kuja na kampeni hiyo itakayochochea hamasa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo wakati wa kugawa taulo hizo (sodo) mwishoni mwa wiki kwa wanafunzi 20 wa Shule ya Msingi Mnini, Uru.

Alisema taulo hizo zina uwezo wa kutumiwa kwa miaka mitatu bila kuharibika.

"Ni kweli kabisa kwamba wasichana wengi, hasa walioko vijijini na maeneo ya pembezoni, wazazi wao wana uwezo mdogo kiuchumi na wasichana wadogo kama hawa hupata mtihani mkubwa wanapokuwa hedhi. Mara nyingi wanakosa taulo za kike za kuwasaidia wakiwa katika mazingira hayo na kujikuta wakitumia vitambaa wakati mwingine.

"Kwa kuwa jambo hili linahitaji uwekezaji wa fedha, kama shirika tumewasaidia kwa kuanza na wanafunzi 20. Tumeuliza, tumeambiwa wamebaki wanafunzi 10. Tunachokifanya hivi sasa tunakwenda kutafuta tena taulo hizo kwa ajili ya wanafunzi 10.

"Kwa vile hili ni tatizo hatuwezi kuwapa seti moja kwamba itakuwa imewatosheleza mahitaji yao, wakati mwingine mvua ni nyingi na taulo zinaweza zisikauke kwa wepesi, kwa hiyo tutakwenda pia kutafuta seti nyingine, ili wawe na angalau seti mbili ziweze kuwafaa kwa majira yote."

"Naamini kuanzia sasa uwezo wa wanafunzi hao utaongezeka darasani, kwa sababu watakuwa hawakosi vipindi. Kwa mwaka mmoja, takwimu mbalimbali zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kike walio katika mazingira hayo, hukosa masomo kwa muda wa siku tano hadi saba kila mwezi, sawa na siku 60 hadi 70 kwa mwaka kutokana na kukosa taulo za kike za kujisitiri."

"Wanafunzi hawa hukosa vipindi darasani, kwa siku hizo kutokana na kukosa taulo za kike au sodo kwa ajili ya hedhi. Tumeamua kuzigawa baada ya kuona kuna tatizo kwa watoto wa kike. Baadhi yao wamekuwa wakikosa masomo yao na kukaa majumbani wanapoingia kwenye hedhi," alisisitiza Hekima.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Roseria Assey, alilishukuru Shirika la UWEZA Foundation, kwa taulo za kike walizogawa kwa wanafunzi wao ambazo ni za kufua.

"Taulo hizi za kufua zitawasaidia wasichana wanaotoka familia maskini, ambazo hazimudu kununua taulo za kike, kuhudhuria masomo wakati wanapokuwa hedhi. Kumekuwa na tatizo la utoro, wanapokuwa katika siku zao. Anapokuja shule asubuhi halafu ikamtokea, huwa wanaogopa kusema na wanatoroka na kwenda nyumbani.

"Wengi wao ni wale wa darasa la sita na darasa la saba. Sasa kwa kuwa baadhi yao wanapokuwa kwenye hedhi, wazazi wengi wanakuwa hawana uwezo wa kuwahudumia hayo mahitaji na pengine wazazi wanakuwa wanaogopa kuzungumza nao kuhusu hali waliyonayo. Huwa tunawaita ofisi tunawapa maelekezo ya namna ya kujisitiri na kujiweka safi," alisema Mwalimu Assey.

Mmoja wa wanafunzi walionufaika na msaada huo, Elizabeth Peter, alimshukuru Mkurugenzi kwa kuwa hali duni ya maisha kwenye familia inawafanya washindwe kumudu huduma hiyo.



Wakazi wa Kata ya Potwe wilayani Muheza mkoani Tanga, wakiwa wameshika miche ya miti kwa ajili ya kupanda ili kutunza mazingira, katika wiki hii wamepanda miti 600 kufikia lengo la mwaka huu kupanda miche milioni 1.5. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wenye ulemavu kutetewa kufikia ndoto zao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MASHIRIKA ya kiraia yanayopambana kufuta mitizamo hasi kwenye jamii dhidi ya watu wenye ulemavu kufikia ndoto zao, wameanza kampeni maalum ya kuwainua kiuchumi na kujinasua dhidi ya unyanyapaa maeneo ya Kibosho, Moshi Vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Kibosho Magharibi, katika kilele cha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Alisema kutokana na mfumo wa makuzi na malezi ndani ya jamii au mfumo dume ndani ya jamii, kujikita kuwanyima wanawake fursa, wameamua kuweka nguvu kutoa elimu katika eneo hilo, ili kupunguza tatizo lisiendelee kuwaumiza wenye ulemavu.

"Wanawake wenye ulemavu wana matatizo mara tatu ya wale ambao hawana ulemavu. Fursa za kiuchumi wanazikosa na hata wakiingia katika taasisi za fedha kwenda kukopa wanakosa mikopo, na saa nyingine hata kufanya biashara sokoni ili wakubalike na biashara zao ziendelee, wanakutana na mitizamo hasi ya watu," alisema na kuongeza:

"Wenye taasisi za fedha wanaona mama huyu mwenye ulemavu, ana uwezo gani wa kufanya kitu niridhike kwamba atarudisha mkopo. Kwa hiyo kuna kuwa na maswali mengi ya sintofahamu na masuala ya kimitizamo kwa asilimia kubwa."

Shirika hilo la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO, linatekeleza mradi wa ubia na Shirika la NAFGEM wa 'Hukumu uwezo wangu, na sio ulemavu wangu' unaofadhiliwa na Shirika la Cross Road International.

Kwa mujibu wa Rutazaa, mradi huo unalenga zaidi kugusa masuala ya kutengeneza uwezo wa kiuchumi, kwa kundi la watu wenye ulemavu kuwasaidia kutambua haki zao na kuisaidia jamii inayowazunguka kutambua na kuheshimu haki za watu wenye ulemavu.

Alisema ni muhimu kutambua wenye ulemavu ni binadamu wana utashi na wana stahiki zao za msingi zilizoainishwa kwenye mikataba na matamko mbalimbali ya kimataifa zinaheshimiwa.

"Mradi huu unawalenga watu wapatao 150 ambao ni walengwa wa moja kwa moja, wakiwamo wanawake 130, wanaume 20. Kwa nini idadi ya wanawake ni kubwa zaidi. Ni kwa sababu tunaelewa kwamba mfumo wa makuzi na malezi ndani ya jamii au mfumo dume ndani ya jamii umejikita katika kuwanyima wanawake fursa na inakuwa ni hatari zaidi kwa wanawake wenye ulemavu kukosa fursa hizo kwa sababu ya ulemavu walionao.

"Kwa ujumla mradi huu, utakuwa umebeba walengwa wa moja kwa moja na wasio wa moja kwa moja wapatao 480. Eneo la kwanza tulilolilwekea nguvu ni kuhamasisha ufikiaji wa huduma ya elimu ya afya ya uzazi na elimu ya kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake wenye ulemavu," alisema na kuongeza:

"Tunajua ukimpa elimu ya usawa wa kijinsia mwanamke mwenye ulemavu, elimu ya kutokomeza ukatili na elimu kuhusu masuala ya uzazi, inampa fursa kubwa sana ya kuweza kuwa na afya njema, lakini kusimamia ndoto zake za kuweza kukua kiuchumi kama mwanamke.

"Eneo jingine tunalolifanyia kazi ni kusaidia kuongeza uelewa, ujuzi na stadi za masuala ya ustawi na kujikwamua kiuchumi kwa walengwa wa moja kwa moja, ambapo ndani yake tunawaundia vikundi vya Vicoba," alisema na kuongeza:

Nipashe

# Spotika



NUKUU 10 BORA KUHUSU RONALDO UK.16 - 17



## ISIKUPITE

Harry Kane alifikia rekodi ya Wayne Rooney ya kufunga mabao 53 England baada ya bao lake la kwanza la kusawazisha dhidi ya Ufaransa kwenye mechi ya Robo Fainali ya Kombe la Dunia, lakini usiku wake juzi uliisha kwa huzuni baada ya kuchapwa 2-1 huku akikosa penalti ambayo ingeiwezesha timu yake kusawazisha. Hata hivyo, Kane amefikisha mabao hayo baada ya mechi 80 wakati Rooney alihitaji mechi 120 kufikisha idadi hiyo.

## LA NUSU FAINALI...

Mshambuliaji wa Morocco, Youssef En-Nesyri (kulia), akiifungia timu yake kwa kichwa bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Ureno kwenye mechi ya Robo Fainali ya Kombe la Dunia la Fifa nchini Qatar juzi. Bao hilo limeiwezesha Morocco kufuzu nusu fainali ambapo sasa itakutana na Ufaransa Jumatano saa nne usiku. **PICHA: MTANDAO**

# NYOTA WA5 WATAKAOSTAAFU BAADA YA KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

KOMBE la Dunia la FIFA ni moja ya mashindano ya kimataifa yenye hadhi ya juu zaidi na wachezaji hutoa kila walichonacho kupata nafasi ya kushiriki katika mashindano hayo.

**Kama ilivyo kwa kila mchezo, wachezaji wa soka pia wanaona ubora wao ukishuka kadri muda wanavyosonga mbele. Kutokana na hili, wachezaji mara nyingi huchagua kuacha kuwakilisha nchi zao pale wanapoona umri na uwezo unawatupa mkono. Wachezaji wengi hupenda kufanya hivyo baada ya mashindano makubwa kama vile Kombe la Dunia la FIFA, ambalo huja mara moja tu kila baada ya miaka minne.**

Katika makala haya, tunaangalia baadhi ya wachezaji wakongwe ambao wanaweza kuaga timu zao za taifa baada ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022, haya sasa...

### #5. Pepe | Ureno

Akiwa na umri wa miaka 39, mkongwe Pepe ndiye mlinzi mwenye umri mkubwa zaidi katika Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Mchezaji huyo wa FC Porto anajulikana sana kama mmoja wa mabeki wa kati wakubwa wa karne ya 21.

Pepe amecheza katika kila mchezo hadi sasa kwenye Kombe la Dunia huko Qatar kabla ya Ureno kutolewa na Morocco hatua ya robo fainali Jumamosi iliyopita. Mshindi huyo mara tatu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, ametoa uzoefu na ubora unaohitajika kwa Ureno.

Kwa ujumla, Pepe ameichezea nchi yake mechi 131 tangu aanze kucheza kimataifa miaka 15 iliyopita. Katika michezo hiyo, amefunga mabao saba na kutoa pasi nne za mabao.

Pepe amecheza katika mashindano yake makubwa ya nane ya kimataifa kwa Ureno. Michuano yake ya kwanza ilikuwa Euro 2008, na aliisaidia nchi yake kushinda Euro mwaka 2016. Beki huyo mwenye uzoefu anatarajiwa kustaafu soka ya kimataifa hivi karibuni, na huenda ikawa mapema mwaka huu.

### #4. Sergio Busquets | Hispania

Nahodha wa Hispania Sergio Busquets, ndiye mshiriki pekee aliyesalia katika enzi yao ya dhahabu ambaye bado anachezea 'La Roja'. Kiungo huyo alikuwa na jukumu la kuunda upya nafasi ya kiungo wa ulinzi kwa uwezo wake wa kiufundi na ustadi.

Busquets ameshiriki katika mechi zote nne za kikosi cha Luis Enrique kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022 nchini Qatar. Sasa mchezaji huyo ana umri wa miaka 34.

Amecheza jumla ya mechi 142 za kimataifa tangu alipocheza kwa mara ya kwanza mwaka 2009, akifunga mabao mawili na asisti tisa. Busquets aliichezea Hispania michuano yake ya saba. Aliisaidia nchi yake kushinda Kombe la Dunia mwaka 2010 na Euro mwaka 2012.

Iwapo ataweza kufanya hivyo, nyota huyo wa Barcelona hivi karibuni anaweza kuungana na wenzake wengi mashuhuri kuamua kuachana na timu ya taifa.

### #3. Manuel Neuer | Ujerumani

Kipa wa Ujerumani Manuel Neuer amekuwa mmoja wa makipa bora na thabiti wa karne ya 21. Nyota huyo wa Bayern Munich anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi na kipa kwenye Kombe la Dunia la FIFA.

Neuer alicheza katika mechi zao zote tatu za hatua ya makundi huku wakitolewa. Yeye ni namba moja ambaye amekuwa akiaminika kwa kikosi hicho.

Kipa huyo mkongwe ameshacheza mechi 19 katika michuano ya Kombe la Dunia tangu alipoanza kucheza michuano hiyo mwaka 2010. Kwa ujumla ameichezea timu yake ya taifa mechi 117 na ameisaidia kufikisha mabao 48 huku akiruhusu mabao 113.

Neuer ameichezea Ujerumani katika michuano saba mikubwa na anatarajiwa kustaafu hivi karibuni. Akiwa na umri wa miaka 36, mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2014 anaweza kuondoka hivi karibuni na Marc-Andre ter Stegen wa Barcelona atachukua nafasi yake.

### #2. Thomas Muller | Ujerumani

Baada ya Ujerumani kutolewa mapema kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022, Thomas Muller, alionekana akiwapungia mkono mashabiki kana kwamba alikuwa amecheza mechi yake ya mwisho.

Muller alishinda Kiatu cha Dhahabu katika Kombe la Dunia la 2010 nchini Afrika Kusini akiwa na umri wa miaka 20 tu Ujerumani ilipomaliza nafasi ya tatu. Amechangia mabao kumi na asisti sita katika mechi 19 za Kombe la Dunia, akishinda michuano hiyo mara moja mwaka wa 2014.

Kwa ujumla, Muller ameichezea Ujerumani jumla ya mechi 121 tangu alipocheza mechi yake ya kimataifa, akifunga mabao 44 na kutoa asisti 40.

Muller ameiwakilisha Ujerumani katika mashindano saba makubwa katika maisha yake ya soka. Hili ni jambo la kustaajabisha ikizingatiwa kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, aliachwa nje ya timu ya taifa kati ya 2019 na 2021 na kocha wa zamani, Joachim Low. Na sasa anaonekana kuwa tayari kutundika viatu vyake.

### #1. Angel Di Maria | Argentina

Mapema mwaka huu, Angel Di Maria alidokeza uwezekano wa kustaafu kucheza timu ya taifa baada ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022 (kupitia AS). Fowadi huyo mwenye uzoefu amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani katika miaka 15 iliyopita.

Di Maria amekuwa katikati ya kila wakati muhimu unaofurahiwa na Timu ya Taifa ya Argentina tangu alipoanza kucheza. Alifunga bao la ushindi kwa timu yake ya chini ya umri wa miaka 23 waliposhinda medali ya dhahabu kwenye Michezo ya Olimpiki ya Beijing ya 2008. Pia alifunga bao la ushindi kwa La Albiceleste hao walipoifunga Brazil na kutwaa ubingwa wa Copa America msimu uliopita wa majira ya joto.

Kwa ujumla, Di Maria ameichezea Argentina mechi 127, akifunga mara 27 na kutoa asisti 26. Ameiwakilisha nchi yake katika mashindano makubwa tisa. Mchezaji huyo wa Juventus atataka kumalizia soka lake akiwa na timu ya taifa kwa kiwango cha juu kwa kuisaidia kushinda Kombe la Dunia.



PEPE

MICHEZO




# TIMU 5 ZENYE MECHI NYINGI ZAIDI ZA LIGI BILA KUPOTEZA

**LONDON,** England

MABINGWA wa kihistoria Tanzania, Klabu ya Yanga imezuiwa kufikia rekodi ya kucheza michezo 50 mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara bila kupoteza.

**Ni klabu ya Ihefu, ambayo usingetarajia kuiona ikiizuia Yanga, lakini iliweza kufanya hivyo Jumanne ya Novemba 29, mwaka huu katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya baada ya kuichapa Yanga kwa mabao 2-1.**

Mara ya mwisho kwa Yanga kufungwa kabla ya mchezo wa Ihefu ilikuwa ni Aprili 25, 2021 dhidi ya Azam ilipolala kwa bao 1-0.

Hata hivyo, michezo yake 49 kabla mchezo wa Ihefu iliyocheza bila kupoteza ni rekodi kwa Tanzania. Hakuna timu iliyowahi kufanya hivyo katika historia ya soka la nchi hii.

Kabla ya Yanga, Azam ndio iliyokuwa ikiishikilia rekodi ya kucheza michezo mingi bila kupoteza, wakicheza mechi 38, rekodi iliyodumu kwa muda wa miezi 18 kati ya Februari 23, 2013 hadi Oktoba 25, 2014

Rekodi ya Yanga kucheza michezo 49 bila kupoteza inafananishwa na rekodi ya 'Washika Mitutu' wa London, Arsenal waliocheza michezo 49 bila kufungwa katika msimu wa 2003-2004.

Sasa sahau kuhusu rekodi ya timu ya Wananchi, Yanga na ile ya Arsenal, klabu hizi tano ziliwahi kucheza michezo mingi zaidi ya ligi zao bila kupoteza na kuweka rekodi katika historia ya soka.

**#5. Al Ahly SC - Misri - 71**

Al Ahly mabingwa wa kihistoria wa Misri ni moja ya klabu kubwa na tishio barani Afrika, ikiwa na rekodi ya kutwaa mataji 42 ya Ligi Kuu nchini Misri na mataji 10 ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ikiwa na makao yake katika Jiji la Cairo, klabu hii iliweka rekodi ya kucheza michezo 71 bila kupoteza katika msimu wa mwaka 2004-2007. Ikiwa ni sawa sawa na misimu mitatu rekodi hii haijavunjwa mpaka leo.

**#4. Esperance Sportive de Tunis-Tunisia – 85**

Esperance ni moja ya klabu maarufu barani Afrika, ikiwa imeanzishwa mwaka 1919, ni miongoni mwa klabu kongwe zaidi nchini Tunisia ikishabihishwa na jezi yake yenye mistari ya njano na nyekundu, imefanikiwa kutwaa mataji 32 Ligi Kuu Tunisia na kimataifa ikiwa na jumla ya mataji 13 yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Esperance imewahi kucheza Ligi Kuu Tunisia bila kupoteza ikicheza michezo 85 kati ya mwaka 1997 na 2001.

**#3. Lincoln Red Imps Fc – Gibraltar – 88**

Hawa ni mabingwa mara 24 wa Ligi Kuu ya nchini Gibraltar ikitumia Uwanja wa Victoria, uwanja ambao unatumiwa na karibu timu zote kubwa zinazoshiriki ligi ya nchini humo.

Ukiacha kucheza michezo 88 ya Ligi Kuu bila ya kufungwa kati ya mwaka 2009 mpaka 2014 pia klabu hii inarekodi ya kutwaa mataji 14 ya ligi katika misimu 14 mfululizo kuanzia mwaka 2003 hadi 2016.

Mwaka 2014 ilikuwa klabu ya kwanza kutoka Gibraltar kucheza Ligi ya Mabingwa barani Ulaya.

**#2. FC Steaua Bucureşti - Romania - 106**

FC Steaua Bucureşti ya Romania ni moja ya klabu maarufu nchini humo, na ilifahamika zaidi katika soka la Ulaya baada ya kutwaa Kombe la Ulaya mwaka 1986 ilipoifunga Barcelona.

Ilikuwa haishikiki katika miaka ya 1980. Iliwahi kucheza mechi 104 bila kufungwa kwa miaka zaidi ya minne kuanzia Juni 1986 hadi Septemba 1989.

Katika kipindi hicho imefanikiwa kutwaa mataji manne ya Ligi Kuu. Inatajwa ndio klabu bora kuwahi kutokea Romania.

**#1. ASEC Mimosa – Ivory Coast – 108**

Les Mimos, kama wanavyofahamika kwa jina la utani, ni moja ya klabu kongwe barani Afrika ikitwaa mataji 24 ya Ligi Kuu nchini Ivory Coast. Ikiwa na maskani yake Abidjan, ina historia isiyozingatiwa sana ya kucheza michezo 108 ya ligi bila kupoteza. Ilifanya hivyo kati ya mwaka 1989 na 1994. Mpaka sasa rekodi yake haijawahi kuvunjwa.

ASEC ilizuiwa kuweka rekodi zaidi ya kutopoteza kwenye ligi kwa kuchapwa na wapinzani wao, Klabu ya SO de l'Armée, ilikuwa mwaka 1994.

Kwa miaka 28 sasa, rekodi yake haijavunjwa na inabaki katika historia ya soka duniani ya kuwa timu iliyocheza michezo mingi zaidi ya ligi ya nyumbani bila kupoteza.

NJE YA UWANJA

CAMEROON mwaka 1990, Senegal (2002) na Ghana (2010), zote ziliishia robo Fainali ya Kombe la Dunia, lakini Morocco imevunja rekodi hiyo na kuwa taifa la kwanza kutoka Afrika na nchini za Kiarabu zenye waislamu wengi kutinga hatua hiyo kwenye mashindano hayo makubwa ya soka duniani.





# NUKUU 10 BORA KUHUSU RONALDO

**LONDON,** England

HAIJALISHI klabu gani unayoshabikia au mchezaji yeyote unayempenda, lakini huwezi kukataa kwamba Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora zaidi kuwahi kutokea. Katika muongo mmoja uliopita, amevunja kila rekodi inayowezekana ya kufunga. Amejaza kabati lake kila sifa ya mtu binafsi na ya pamoja.

**Mwaka 2016, aliiongoza Ureno kutwaa ubingwa wa Ulaya na ndio mfungaji bora wa wanaume kwa timu ya taifa wa wakati wote.**

Hapa, tunaangalia nukuu kumi maarufu za wachezaji wenzake, wapinzani na wachezaji wa zamani juu ya ustadi wake.

### #10. Jose Mourinho

Jose Mourinho alikuwa akizungumza kabla ya mechi ya Real Madrid dhidi ya Manchester United mwaka 2013 kule Old Trafford. Aliamini kwamba Mreno mwenzake huyo tayari alikuwa amewazidi Maradona na Pele kama mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea.

***"Yeye ndiye bora zaidi. Bora zaidi duniani, ndiyo. Pengine bora zaidi. Nilimwona Maradona mara kadhaa. Sijawahi kumwona Pele."***

***"Lakini Cristiano ni wa kushangaza. Mtu huyu ndiye bora zaidi. Cristiano ni mashine ya mabao. Ni mchezaji wa ajabu. Ni kama Zidane; hakutakuwa na Ronaldo mwingine."***

Kocha huyo aliiongoza Real Madrid kwa misimu mitatu yenye mafanikio ya wastani.

### #9. Zinedine Zidane

Zidane, bila shaka, aliiongoza timu yenye mafanikio makubwa ya Real Madrid. 'Los Blancos' walitwaa mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya chini yake, huku Ronaldo akiongoza safu hiyo kabla ya kutimkia Juventus msimu wa majira ya joto wa 2018.

Wawili hao walipata mafanikio makubwa katika muda wao wa kukaa pamoja katika mji mkuu wa Hispania na kama kuna mtu alishangaa jinsi ilivyokuwa raha kuwa na mtu wa aina ya Ronaldo kwenye timu, Zidane ameweka wazi kuhusu hilo.

***"Unapocheza na Ronaldo kwenye timu yako, tayari uko mbele kwa bao 1-0."***

### #8. Ryan Giggs

Ryan Giggs, ambaye anachukuliwa kama gwiji wa Manchester United, alikuwa na maisha yenye mafanikio makubwa kwenye Ligi Kuu England. Ronaldo alipofika Old Trafford, mchezaji huyo wa Wales tayari alikuwa nyota mkubwa.

Mchezaji huyo wa Wales alikuwa na mchango wa kudumu kwa Ronaldo. Baada ya yote, ilikuwa chini ya macho yake ambapo Ronaldo alikuwa kutoka kijana mdogo hadi mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.

***"Ronaldo anapopata mpira, unaweza kumwacha tu kwani atamshinda mchezaji mmoja baada ya mwingine."***

### #7. Luis Figo

Luis Figo alikuwa mtangulizi wa Ronaldo, kwa kila maana ya neno hilo. Wawili hao walikuwa na taswira zinazofanana, huku Figo akianzia soka yake nchini Ureno na kisha kujiunga na moja ya klabu kubwa za Ulaya, Barcelona. Kisha akahamia Real Madrid na kupata mafanikio huko.

Ronaldo alicheza chini ya uongozi wa Figo katika upande wa taifa hadi Figo alipostaafu baada ya Kombe la Dunia la 2006.

***"Kuna baadhi ya mambo ambayo Ronaldo anaweza kufanya akiwa na soka ambayo yananifanya niguse kichwa changu na kujiuliza ni jinsi gani anavyofanya."***

### #6. Sir Bobby Charlton

Sir Bobby Charlton, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa viungo bora zaidi wa wakati wote, ni gwiji wa Manchester United.

Akiwa mmoja wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Man United, alipata fursa ya kuona maendeleo ya Ronaldo. Sir Bobby hakuacha kujizuia kumsifia.

***"Yeye (Ronaldo) anafanya mambo ambayo sijawahi kuona kutoka kwa mchezaji mwingine yeyote na ni ajabu kutazama."***

### #5. Johan Cruyff

Johan Cruyff hapo awali aliwahi kusema kwamba Ronaldo alikuwa kitu maalum. Wakati mashabiki na wachambuzi wa mambo walipoanza kumlinganisha Ronaldo na George Best na Denis Law, magwiji wawili wa historia ya United, aliweka rekodi ya kusema kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alikuwa bora zaidi kuliko wawili hao.

***"Cristiano Ronaldo ni bora kuliko George Best na Denis Law, ambao walikuwa wachezaji wawili mahiri na wazuri katika historia ya United."***

### #4. Eusebio

Cristiano Ronaldo alifananishwa na Eusebio. Kasi yake, mbinu, mbio, mashuti makali ya mguu wa kulia, na uwezo wake wa kupachika mabao ulichangia kufanana kwa ajabu na nguli huyo wa Ureno.

Eusebio, mwenyewe, alivutiwa na sifa za mrithi wake na akamsifu Ronaldo.

***"Ana uchawi kwenye viatu vyake. Jambo la kwanza unalogundua juu yake ni kwamba ana haraka sana na ana nguvu sana."***

***"Ana udhibiti mzuri, wa karibu na mbinu yake ni bora. Anaamini kuwa anaweza kufanya lolote akiwa na mpira, na kujiamini huko kunamfanya awe wa pekee sana."***

### #3 George Best

George Best anachukuliwa na wengi kama mwanasoka bora zaidi wa wakati wote, bora zaidi ya Pele na Diego Maradona. Winga huyo ambaye alikuwa na sifa nyingi zinazofanana na za Ronaldo, ni gwiji wa Manchester United.

Bila shaka, alikuwa mwanasoka aliyeifanya jezi namba saba kuwa maarufu zaidi pale United, na ni sehemu ya urithi wake unaoifanya namba hiyo kuwa maalum sana. Ronaldo, baadaye, alivaa jezi hiyo pale Old Trafford na baadaye alifananishwa naye.

***"Kumekuwa na wachezaji wachache walioelezewa kama George Best mpya kwa miaka mingi, lakini hii ni mara ya kwanza imekuwa pongezi kwangu."***

### #2. Sir Alex Ferguson

Mmoja wa makocha waliofanikiwa zaidi katika historia ya soka ni Sir Alex Ferguson ambaye alisimamia zama za mafanikio zaidi katika historia ya Manchester United. Ni yeye ambaye kwanza alitambua uwezo halisi wa Ronaldo, akamleta England na kumtengeneza kuwa gwiji wa dunia.

Miaka 26 katika klabu moja si mafanikio rahisi. Katika miaka hiyo yote, Sir Alex alikuwa ameona baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani, kuanzia David Beckham hadi Paul Scholes. Hata hivyo, alichagua kumweka Ronaldo kileleni.

***"Tumekuwa na wachezaji wazuri katika klabu hii katika miaka yangu 20, lakini Ronaldo ni mchezaji bora zaidi."***

### #1 Lionel Messi

Lionel Messi, bila shaka, ndiye mpinzani mkubwa wa Ronaldo. Wachezaji hao wawili wametawala soka la dunia katika muongo mmoja uliopita. Tangu mwaka 2008, wawili hao wameshiriki tuzo ya Ballon d'Or mara 12, huku Ronaldo akishinda mara tano na Messi saba.

Muargentina huyo, ambaye mara chache amekuwa akiongea wazi kuhusu mpinzani wake, alimwagiwa sifa kemkem kwenye mahojiano mwaka 2013. Ingawa alikuwa ametoka tu kutwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa kufunga mabao mengi zaidi msimu uliopita, alikuwa mwepesi kutambua ubora wa Ronaldo wa kufunga.

***"(Ronaldo) huwa anafunga mabao katika michezo yote. Amekuwa akifanya hivyo kwa miaka mingi na yuko kwenye kilele chake."***

## Nukuu

"Sifikirii hivyo, hakuna majuto. Nadhani hii ilikuwa timu ambayo ilicheza vizuri sana dhidi ya Uswisi. Cristiano Ronaldo ni mchezaji mzuri, aliingia wakati tulifikiri ilikuwa muhimu, kwa hiyo hakuna majuto. Ikiwa tutachukua watu wawili ambao walikasirishwa zaidi ni Cristiano Ronaldo na mimi mwenyewe. Bila shaka tumekasirika, lakini hiyo ni sehemu ya kazi ya kocha na mchezaji," **Kocha Mkuu wa Ureno, Fernando Santos, akielezea kutojuta kwa kutomwanzisha Ronaldo dhidi ya Morocco kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia wakati wakichapwa bao 1-0.**



"Mimi si mtu wa kufikiria sana kuhusu hilo. Ninajiandaa ikiwa nitapata penalti moja au mbili kwenye mchezo. Siwezi kukosea maandalizi yangu au undani kabla ya mchezo. Lakini tunachoweza kufanya ni kujivunia kila mmoja wetu na kujua timu iko mahali pazuri sana na lazima tujaribu kutazama siku zijazo," **Mshambuliaji wa England, Harry Kane baada ya kukosa penalti ya pili wakati wakichapwa 2-1 na Ufaransa kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia.**



"Ni kwa uwezo wa wachezaji kuwa katika nafasi nne za mwisho tena. Tulipata bahati kidogo ingawa tulitoa penalti mbili, lakini tuliendelea kuongoza kwa mioyo yetu na moyo wetu," **Kocha Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps baada ya timu yake kuitoa England kwa mabao 2-1 juzi na kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia.**



## Michezo




CHAMA

# REKODI LIGI KUU ZILIVYO MZUNGUKO WA KWANZA

Na Adam Fungamwango

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika, kila timu ikicheza mechi 15 na kuvuna kile ilichokipanda.

**Jumla ya timu 16 zinashiriki ligi hiyo kwa zikisaka ubingwa wa Tanzania Bara, mshindi wa pili atakayeungana na bingwa kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, na timu itakayoshika nafasi ya tatu ambayo itaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika endapo Tanzania itaendelea kutetea nafasi ya kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa.**

Katika makala haya, tunaangaza rekodi na takwimu zilizowekwa na baadhi ya timu na wachezaji kwenye Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza...

**#1. Yanga inashinda, pointi kibao**

Mabingwa Watetezi Yanga wamemaliza mzunguko wa kwanza wakiwa wanaongoza kwa kuwa na pointi nyingi, lakini kushinda mechi nyingi.

Imemaliza mzunguko wa kwanza ikiongoza kwa pointi 38, ikifuatiwa na Azam ambayo ina pointi 35. Yanga pia ndiyo timu iliyoshinda mechi nyingi, ikiwa imepata ushindi kwenye mechi 12 mpaka sasa, ikifuatiwa pia na Azam ambayo imeshinda mechi 11 hadi kumalizika kwa mzunguko huo.

**#2. Simba fowadi wembe, ukuta chuma**

Simba ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake 34, ndiyo timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi, huku ikifungwa machache zaidi kuliko timu yoyote.

Timu hiyo imefunga mabao 31, ikifuatiwa na Yanga ambayo imepachika mabao 27. Mbali na hilo, mpaka mzunguko wa kwanza unamalizika, Simba imeruhusu wavu wake kuguswa mara saba tu, ikifuatiwa na Yanga ambao imeruhusu mabao manane mpaka sasa kwenye wavu wake.

**#3. Mbeya City wazee wa sare**

Hadi mzunguko wa kwanza unamalizika, timu ya Mbeya City ndiyo ina sare nyingi zaidi. Ina sare nane mpaka sasa ambazo ni nyingi zaidi kuliko timu yoyote. Timu hiyo imecheza mechi 15, ikishinda nne, sare nane na kupoteza tatu. Timu zinazoifuatia ni Geita Gold na KMC ambazo kila moja imetoka sare mara saba.

**#4. Polisi pointi kiduchu, ushindi tatizo**

Maafande wa Polisi Tanzania wamemaliza mzunguko wa kwanza wakiwa na pointi chache zaidi, lakini pia ndiyo timu iliyoshinda mechi chache zaidi kuliko timu zingine. Kibaya zaidi inashika mkia kwenye msimamo wa ligi.

Timu hiyo imeshinda mechi mbili tu kati ya 15 ilizocheza, ikiwa na pointi tisa tu ambazo ni chache zaidi kwenye ligi na mpaka sasa inaburuza mkia.

**#5. Mtibwa beki chekeche**

Mtibwa Sugar, japo inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini ndiyo timu iliyofungwa mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza. Imeruhusu mabao 25 ambayo ni mengi zaidi kuliko hata iliyoruhusu Polisi Tanzania inayoburuza mkia. Polisi Tanzania imeruhusu mabao 23, hivyo ina wastani mzuri wa mabao ya kufungwa kuliko Mtibwa. Kwa maana hiyo timu hiyo inaonekana kuwa na matatizo kwenye safu yake ya ulinzi.

**#6. Phiri na Mayele hawashikiki**

Mastraika wa kigeni, Mosses Phiri wa Simba na Fiston Mayele wa Yanga wamemaliza mzunguko wa kwanza kila mmoja akipachika mabao 10 kwenye nyavu.

Phiri raia wa Zambia ni msimu wake wa kwanza kucheza soka nchini, huku Mayele ambaye ni raia wa Jamhuri wa Kidemokrasi ya Congo akiwa kwenye msimu wake wa pili na timu ya Yanga.

Wachezaji hao wanafuatiwa na Mtanzania, Sixtus Sabilo anayeichezea Mbeya City ambaye ana mabao saba mpaka sasa. Mkongomani, Idris Mbombo wa Azam FC na Mtanzania Reliants Lusajo, wote hawa wana mabao sita kila mmoja.

**#7. Chama mkali wa 'Assist'**

Hadi mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu unamalizika, kiungo mshambuliaji raia wa Zambia Clatous Chama anayeichezea Simba, akiwa anaongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao akiwa na 'asisst' saba.

Kiungo mshambuliaji wa Geita Gold Saido Ntibazonkiza, Ayoub Lyanga wa Mbeya City na Sixtus Sabilo wanafuata kila mmoja akiwa na pasi za mwisho sita.

NDANI YA 18



IVAN Perisic kwa sasa amefunga mabao 10 kwenye Kombe la Dunia na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa pamoja, ikiwa ni mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa Croatia katika historia ya soka.

# SOKA



**KOMBE LA DUNIA QATAR**
Kylian Mbappe anaongoza katika orodha ya wafungaji wanaowania Kiatu cha Dhahabu akiwa na mabao matano hadi sasa. Anafuatiwa na Lionel Messi wa Argentina pamoja na Mfaransa Olivier Giroud ambao kila mmoja ana mabao manne wakati huu timu zao zikiwa zimetinga hatua ya nusu fainali.

**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Kylian Mbappe
**KUZALIWA:** Desemba 20, 1998 (miaka 23)
**ALIPOZALIWA:** Paris, Ufaransa
**KIMO:** 1.78 m (5 ft 10 in)
**NAFASI:** Mshambuliaji
**KLABU:** Paris Saint-Germain
**JEZI:** Namba 7/ Taifa Na. 10

HAIJALISHI klabu gani unayoshabikia au mchezaji yeyote unayempenda, lakini huwezi kukataa kwamba Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora zaidi kuwahi kutokea. Katika muongo mmoja uliopita, amevunja kila rekodi inayowezekana ya kufunga. Amejaza kabati lake kila sifa ya mtu binafsi na ya pamoja.

Uk. 16-17




# MAKINDA WANAOWEZA KUMRITHI HAZARD UBELGIJI

**BRUSSELS,** Ubelgiji

KUNA jambo la kusikitisha sana kuhusu jinsi maisha ya soka ya Eden Hazard yalivyoshuka tangu kuondoka kwake Chelsea. Mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alichukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kuelekea mwisho wa wakati wake kwenye Ligi Kuu England.

**Ndio maana Real Madrid walitumia pauni milioni 143 kumleta katika mji mkuu wa Hispania mwaka 2019. Ilikuwa ndoto kwa Hazard kuhamia Real Madrid. Lakini kwa upande wake mambo hayakwenda vizuri kama ilivyokuwa kwa Gareth Bale Cristiano Ronaldo na Luka Modric.**

Amefunga mabao saba na kupata asisti 11 katika mechi 72 alizoichezea 'Los Blancos', chini ya kiwango kilichotarajiwa. Hilo limeathiri kiwango chake katika Timu ya Taifa ya Ubelgiji ambayo aliwahi kuwa kinara.

Baada ya Ubelgiji kushindwa kufuzu kutoka hatua ya makundi kwenye Kombe la Dunia la Qatar 2022, Hazard ameamua kustaafu kucheza soka la kimataifa.

Maneno 'kizazi cha dhahabu' hutumiwa kila mara kuhusu timu hii ya Ubelgiji, na sasa inaonekana kwamba mapinduzi yanahitajika. Kocha Roberto Martinez amekwenda, Hazard amekwenda, na wengine watafuata, hivyo sasa kinahitajika kizazi kingine.

Ni wachezaji gani vijana wa Ubelgiji waliopo uwanjani hivi sasa ambao wanaweza kuleta ubunifu unaohitajika kushinda mashindano makubwa?

Makala haya inawaangalia vijana wanaoweza kuvaa viatu vya Hazard, hawa hapa...

**Jeremy Doku**

Jeremy Doku ni jina ambalo limekuwa kwenye Timu ya Taifa ya Ubelgiji kwa miaka kadhaa sasa na alivutia sana wakati wa Euro 2020. Hata hivyo, hakuwa na mchango mkubwa nchini Qatar.

Doku alikuwa nyota katika klabu ya Anderlecht kabla ya kuhamia Rennes bila kutarajiwa huku akihusishwa na klabu kubwa zaidi za Ulaya. Alijiunga na timu hiyo ya Ufaransa kwa euro milioni 26 na tayari amefunga mabao manne na pasi sita za mabao katika mechi 65.

Bado ana umri wa miaka 20 tu na ikiwa atapata kiwango bora zaidi nchini Ufaransa au kuhamia kwingineko, Doku bado ana uwezo wa kuwa mchezaji muhimu wa kushambulia kutoka maeneo mengi ya Ubelgiji katika siku zijazo.

**Charles De Ketelaere**

Mchezaji wa AC Milan, Charles De Ketelaere yuko katika hatua muhimu ya maendeleo yake hivi sasa. Alifanikiwa mapema sana akiwa Club Brugge na kufunga mabao 25 na kupata pasi za mabao 20 katika mechi 120, akishinda mataji ya ligi katika mchakato huo.

Milan imekuwa mahali pazuri kwa wachezaji wachanga kupata wakati na nafasi ya kujiendeleza, lakini bado hajaweza kuleta matokeo yoyote nchini Italia. Klabu na mashabiki wengi wana imani naye na ataonyeshwa uvumilivu, lakini inaweza kuchukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa. Bado ana umri wa miaka 21 tu na anaweza kuwa mbadala mzuri wa Hazard.

Yari Verschaeren

Kama Doku, Yari Verschaeren ni jina lingine ambalo lilionekana kudhamiriwa kujulikana miaka michache iliyopita na kisha kujitahidi kuendelea. Kama ilivyo kwa wachezaji wengi wachanga ambao mara moja wanatarajiwa kubadilisha ulimwengu, bado ni mchanga na ana nafasi ya kuwa nyota. Sasa ana umri wa miaka 21.

Yeye ni mshambuliaji na amekuwa katika kiwango kizuri akiwa na Anderlecht msimu huu, akiwa na mabao matatu na asisti tatu katika mashindano yote. Namba hizo zinaweza kuboreshwa. Kama De Ketelaere, alipitia umri mdogo sana na tayari amecheza mechi 136 akiwa na Anderlecht. Verschaeren anaweza kuwa nguzo muhimu kwa Ubelgiji.

**Anouar Ait El Hadj**

Akiwa na umri wa miaka 20, Anouar Ait El Hadj ni jina lisilojulikana kwenye orodha hii, lakini ni kipaji kingine cha kusisimua kinachopatikana Anderlecht, mojawapo ya akademi bora zaidi duniani.

Anapendelea kucheza chini katikati na amekuwa akipambana na Verschaeren kuwania nafasi msimu huu, lakini pia anaweza kucheza zaidi kama winga wa kushoto. Amecheza mechi chache tu msimu huu akiwa na Anderlecht, lakini kuna msisimko katika klabu kuhusu mustakabali wake na ni mmoja wa kuangaliwa.

**Cisse Sandra**

Cisse Sandra anacheza kwa kina kidogo kuliko unavyoweza kumfikiria Hazard akicheza, lakini anaweza kuwa mbele zaidi inapohitajika.

Sandra ana umri wa miaka 18 pekee na anacheza mechi nyingi akiwa na Club Brugge kwenye ligi. Ni jina la kuangaliwa na kocha mpya wa Ubelgiji anaweza kuangalia kumwinda haraka kwenye kikosi cha kwanza hivi karibuni.

**JE, WAJUA?**

VINICIUS Junior (miaka 22 na siku 146), ni mchezaji kinda zaidi kuweza kuifungia Brazil kwenye michuano ya Kombe la Dunia la Fifa tangu Neymar alipofanya hivyo mwaka 2014 dhidi ya Croatia akiwa na miaka 22 na siku 127.



## Serikali yawaonya wanaopotosha wananchi Hifadhi Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali, imewatahadharisha watu wanaowapotosha wananchi wa vijiji vinavyotakiwa kuondolewa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wakiwataka kuendelea kukaa kwenye maeneo hayo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alitoa tahadhari hiyo juzi baada ya baadhi ya watu wanaojifanya wanasheria kuwashawishi wananchi waendelee kuishi kwenye maeneo wanayotakiwa kuondoka.

Alisema hivi karibuni jopo la mawaziri wanane wa kisekta walitembelea maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kutoa utaratibu na kwamba wananchi wanatakiwa kuwasikiliza viongozi wa serikali na sio watu wengine.

Alisema baada ya maelekezo yaliyotolewa na mawaziri kinachofuata ni uwekaji wa mipaka mipya ambayo itasaidia kuondoa mwingiliano wa shughuli za uhifadhi na shughuli za kibinadamu.

"Hatutasita kuchukua hatua za kisheria kwa wale watakaobainika kuwapotosha wananchi, nawataka wananchi watusikilize sisi viongozi wao na sio hao wapotoshaji," alisema Mfune.

Alisema kumekuwapo na mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na hifadhi tangu mwaka 2008 baada ya kutolewa kwa tangazo la serikali namba 28 ambalo lilikuwa linaainisha mipaka mipya ya hifadhi hiyo.

Serikali imetenga zaidi ya hekta 74,000 kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo na ufugaji kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Mbarali wakiwamo watakaoondolewa kwenye vijiji vya kwenye hifadhi.

# Mbunge awakatia bima ya afya watoto 150

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MBUNGE wa Jimbo la Lupa wilayani Chunya, Masache Kasaka, amewakatia bima za afya watoto 150 wenye ulemavu wilayani humo kwa lengo la kuzipunguzia familia zao gharama za kuwatibu wanapougua.

Aidha, ameshiriki chakula cha mchana na baadhi ya watoto hao, wazazi wao pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo wilayani humo ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa.

Masache alikabidhi kadi za bima kwa watoto hao mwishoni mwa wiki wakati wa hafla maalumu iliyofanyika nyumbani kwake na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wilayani humo.

Alisema aliamua kuwakatia bima watoto hao kwa sababu kundi la watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi yanayohitaji uangalizi wa karibu hasa kwenye masuala ya afya.

Alisema Wilaya ya Chunya ina zaidi ya kaya 300 zenye watoto wenye ulemavu, lakini alianza na watoto 150 kutokana na uwezo wa kiuchumi aliokuwa nao na ataendelea kutafuta fedha ili kuwakatia waliobaki.

"Mwaka huu nimeona nisherehekee siku yangu ya kuzaliwa kwa kuwakumbuka watoto hawa wenye ulemavu, nimewakatia bima hizi hawa 150, lakini lengo langu ni kuwapatia wote 300 ambao wanafahamika," alisema Kasaka.

Alisema wakati serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wote, yeye ataendelea kuyasaidia makundi maalumu huku akisisitiza kuwa Mswada wa Bima ya Afya kwa wote utakapopelekwa bungeni watahakikisha unapita.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alimshukuru Masache kwa kulikumbuka kundi hilo huku akiwaomba wadau na viongozi wengine wa maendeleo wilayani humo kuiga mfano huo wa kusaidia makundi maalumu.

Alisema serikali inaendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini, kununua vifaa tiba na kuajiri watumishi, wadau wanatakiwa kuungana na serikali kwenye mikakati hiyo.

Alisema bima za afya walizokatiwa watoto hao zitazisaidia familia zao kupunguza ukali wa gharama za matibabu kwa makundi hayo kwa kuwa baadhi ya watoto wenye ulemavu wanakuwa katika hatari ya kupata magonjwa kutokana na maumbile yao.

"Watu wenye ulemavu ni binadamu kama tulivyo sisi wengine, tofauti ni kwamba wenzetu wanakuwa na upungufu wa baadhi ya viungo kwa hiyo ni lazima tuwasaidie binadamu wenzetu hawa, nampongeza sana mbunge wetu maana hata mimi sijawahi kufikiria kitu kama hiki," alisema Mayeka.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Chunya, Mwalimu Gerald Shitindi, aliwataka wazazi na walezi wilayani humo kuwafichua watoto wenye ulemavu na kuwapeleka shuleni ili wasome kama ilivyo kwa watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Alisema katika wilaya hiyo zipo shule maalumu zinazotoa elimu jumuishi kutokana na serikali kuajiri walimu wenye ujuzi wa kuwafundisha watoto wa makundi hayo.

Alisema kuna tatizo la baadhi ya wazazi kuwaficha watoto wenye ulemavu na kuwazuia kwenda shule jambo alilosema ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Mtoto.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Simon (katikati), akimkabidhi kadi ya Bima ya Afya mmoja kati ya watoto 150 wenye ulemavu wilayani humo mwishoni mwa wiki, walizokatiwa na Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka (kulia kwa mkuu huyo wa wilaya). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kanisa latoa neno kulinda amani, utulivu nchini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KANISA la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi, limewataka Watanzania kuendelea kushirikiana na serikali kulinda amani na utulivu uliopo ili shughuli za maendeleo ziendeleaa kufanyika.

Kanisa hilo pia limeipongeza serikali kwa kuweka mifumo imara ya uwekezaji ambayo inazifanya taasisi mbalimbali zikiwamo za dini kuwekeza kwenye miradi ikiwamo inayohusu sekta ya elimu na ufundi.

Mwenyekiti wa jimbo hilo, Mchungaji Robert Pangani, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa mahafari ya Chuo cha Ufundi Stadi cha kanisa hilo kuwa katika baadhi ya mataifa watu wanashindwa kufanya kazi kwa sababu hakuna utulivu.

Alisema Watanzania wanapata nafasi ya kuabudu bila kuwa na ulinzi kutokana na kuwa ni taifa lenye amani na utulivu.

Alisema serikali imeweka sheria na taratibu ambazo zinamruhusu kila Mtanzania kuabudu dini anayoiamini bila kushinikizwa tofauti na mataifa mengine ambayo yanaongozwa na mifumo ya udini.

"Tumekusanyika hapa kwa amani bila hata kuwa na ulinzi kwa sababu taifa letu ni lenye amani na utulivu wa kutosha, lakini pia tumeanzisha chuo hiki na kukiendesha kwa kufuata miongozo iliyowekwa na serikali yetu, hivyo ni lazima tushirikiane kulinda amani yetu," alisema Mchungaji Pangani.

Alisema kanisa hilo limeanzisha taasisi za elimu ili kuungana na serikali kwenye vita dhidi ya umaskini na ujinga kwa kuhakikisha vijana wanapata fani zinazowawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Aliwataka vijana waliohitimu kwenye chuo hicho kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo wao wenyewe na taifa huku akiwataka kuwa na nidhamu ya fedha ili kujiinua kiuchumi.

Mkuu wa Chuo hicho, Gadi Lwinga, alisema kwa mwaka huu vijana waliohitimu mafunzo ya ufundi kwenye fani mbalimbali wako 213 huku akisisitiza wamepata utaalamu utakaowasaidia kwenye maisha yao.

Alisema chuo hicho awali kilikuwa kina usajili wa VETA, lakini baada ya serikali kufanya marekebisho kinasimamiwa na NACTE na kinafuata mitaala iliyoandaliwa na serikali.

Alisema chuo hicho kinashirikiana na mashirika mbalimbali kuwasomesha vijana wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuwapatia vifaa ili wajiajiri baada ya kupata mafunzo.

"Hapa tunatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwenye fani za ufundi magari, ufundi umeme, ufundi bomba, mapishi, ushonaji na useremala, tunao wataalamu wanaofundisha hapa ili kuhakikisha vijana wanapata ujuzi sahihi," alisema Lwinga.

Mwenyekiti wa Bodi ya chuo hicho, Mhandisi Arthu Mwabulambo, alisema wataendelea kushirikiana na kanisa kuboresha miundombinu yake kuhakikisha wanafunzi wanapata mafunzo kwenye mazingira mazuri.

Aliwataka wahitimu kuutumia ujuzi walioupata kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa na serikali ama taasisi binafsi.





# Rais Samia atunukiwa tuzo ya mwongoza watalii bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa tuzo ya kimataifa ya kuwa muongoza watalii bora kupitia filamu ya 'Tanzania The Royal Tour'.

Akipokea tuzo hiyo iliyotolewa na International Iconic Award ya India na kukabidhiwa na Taasisi ya Miss Jungle International na Taasisi ya Bega kwa Bega na Mama Foundation jana jijini hapo kwa niaba ya Rais, Balozi Dk.Pindi Chana, alisema wizara hiyo inamshukuru Rais Samia kwa kuwaongoza katika kwenye filamu hiyo ambayo sekta mbalimbali zimenufaika na kufungua utalii nchini.

Alisema idadi ya watalii wanaokuja Tanzania imeongezeka kutoka 992,692 mwaka 2021 na kufikia zaidi ya milioni moja mwaka huu.

"Nampongeza Rais kwa kutunukiwa tuzo hii na kuwa muongoza watalii namba moja na huu ni wakati wetu sisi kujipima kwenye kutangaza utalii, tuje na ubunifu wa aina mbalimbali kutangaza madini ya tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee duniani,"alisema.

Alisema wageni wengi wanaendelea kuja nchini kutokana na kuangalia vigezo vilivyoko ikiwamo utulivu, amani na siasa imara.

Alisema kuwa fursa zilizoko ni kuvutia uwekezaji ikiwamo kujenga hoteli na vyuo vya utalii.

Alisema sekta ya utalii imeongeza mauzo ya nje kwa asilimia 25, wastani asilimia 17.2 ya pato ghafi la taifa huku kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja ni milioni 1.5.

"Mchango wa sekta ya utalii unapaswa kuongezeka zaidi kulinganisha na vivutio vya utalii vilivyoko, tunashukuru Miss Jungle inakuja na mazao mapya ya kutangaza tanzanite, lakini hivi sasa tumesema ni ruksa kuwa na makumbusho binafsi,"alisema.

Alisema lengo ni kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano na mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Juma Mkomi, aliwahimiza watendaji wa wizara hiyo kuendelea kuongeza ubunifu katika kuhifadhi na kutangaza maeneo ya utalii yaliyoko.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Miss Jungle International, Haroun Kinega, alisema filamu hiyo ni hatua ya kuichukua Tanzania kuipeleka duniani na kilichofuata ni kuileta dunia Tanzania.



Wajane kutoka madhehebu mbalimbali ya dini wakipokea zawadi za nguo zilizotolewa na mdau wa maendeleo Anna Ngowi ambaye ni muumini wa Kanisa la TAG Dodoma kwenye hafla iliyoambatana na chakula cha pamoja jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jaji Mkuu: Kuna ukiukwaji wa haki za uadilifu kwa viongozi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JAJI Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, amesema kumekuwapo na vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa haki za uadilifu kwa viongozi na watumishi wa umma na sekta binafsi.

Alibainisha hayo juzi jijini hapo wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya kilele cha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu.

Alisema mhimili wa mahakama upo macho kuwachukulia hatua viongozi au watumishi wa umma watakaobainika kuvunja sheria na kupatikana na hatia atapata adhabu kwa mujibu wa sheria.

"Hapa niipongeze serikali kwa kuwa imekuwa ikichukua hatua stahiki dhidi ya wahusika kila wakati hali hiyo inapojitokeza. Hapa niseme kuwa, mhimili wa mahakama uko macho kuhakikisha kuwa kila anayejihusisha na uvunjifu wa sheria na kupatikana na hatia, atapata adhabu kwa mujibu wa sheria,"alisema.

Alieleza kuwa tabia zinazosababisha kiongozi kuonekana hana uaminifu ni kupendelea kukuza au kuchochea rushwa katika shughuli za umma hali inayohatarisha maslahi au ustawi wa jamii.

Alisema ni vyema viongozi wakasimamia utoaji huduma katika sekta ya umma na binafsi bila kudai au kupokea rushwa.

"Watumishi wa umma na sekta binafsi nchini wanapaswa kukumbuka kuwa misingi ya maadili ya viongozi wa umma, ipo kwa mujibu wa Ibara ya 132 (5)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,"alisema.

Aliongeza:"Tukumbuke watumishi wa umma wanaojihusisha na vitendo vya rushwa huwakosesha wananchi haki zao za msingi ustawi wao na wa taifa. Kwa kufanya hivyo watambue kuwa wanafanya vitendo vya kijinai na pia wanakiuka haki za binadamu na kwamba wanavunja Ibara ya 12 - 21 ya Katiba ya mwaka 1977."

Alisema kuwa rushwa isipodhibitiwa hujijengea mfumo wake usio rasmi ambao huweza na kutokomeza mfumo rasmi.

"Kila kiongozi, mtumishi, mwananchi na wadau wote tuna wajibu wa kupinga na kukataa kila aina ya uovu katika jamii ikiwamo rushwa, uonevu, wizi, ubadhirifu wa mali na uvunjifu wa haki za binadamu,"alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawara Bora, Jenista Mhagama, alisema mapambano dhidi ya rushwa nchini ni jukumu la kila mtu na siyo la serikali peke yake.

Kamishna wa Maadili nchini, Jaji Sivangilwa Mwangesi, alisema Tanzania huungana na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Mataifa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa(UNCAC).

Alisema serikali iliamua kuita siku hiyo kuwa ya maadili na iadhimishwe Desemba 10 kila mwaka, kwa mwaka huu walitembelea Gereza la Isanga na Msalato kwa lengo la kuongea na kuwasilikiza wafungwa.

# Matukio ya vipigo yashamiri wilayani Chamwino

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

MATUKIO ya vipigo yametajwa kuongoza kwenye vitendo vya ukatili wa kijinsia katika Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Deodatus Damian, alitoa takwimu hizo wakati wa mkutano ulioandaliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ActionAid Tanzania na AFNET ikiwa ni maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema licha ya serikali na mashirika kuendelea na kampeni ya kupinga vitendo vya ukatili lakini kwa wilaya hiyo bado vitendo hivyo vinashika kasi.

"Takwimu zilizotolewa Desemba 9, 2022 na zinaonyesha watu 600 walifanyiwa ukatili, huku kesi nne zikiwa za ulawiti, kesi nyingi zinakosa ushahidi kutokana na kumaliza kimila," alisema.

Alieleza kuna umuhimu wa wananchi kupata elimu ili kujiepusha na vitendo hivyo na mkakati mkubwa uliopo ni kuimarisha Kamati za Ulinzi na Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), ngazi ya kijiji, kata na wilaya.

Ofisa kutoka Dawati la Jinsia na Watoto katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, Kija Banka, alisema kwa sasa wanapata takwimu nyingi za watoto wa kiume kulawitiwa na kuwataka wazazi kutobweteka na kupaza sauti kuhusiana na watoto wao.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, alisema ili kupambana na ukatili wa kijinsia njia mbalimbali zinapaswa zitumike mojawapo ni kutoa elimu kwa wananchi kuachana na vitendo vya unyanyasaji ambavyo ni kinyume cha sheria za nchi.



HABARI ZANZIBAR

# ‘Muhimu kuwapo na mfumo maalum fidia kesi udhalilishaji’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Salum Hassan Bakari, amesema washtakiwa wengi hasa wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia hushindwa kulipa fidia wanazotozwa mahakamani kutokana na kutokuwa na uwezo.

Aliyasema hayo jana mjini hapo, katika kongamano la siku ya haki za binadamu lililoandaliwa na Kituo cha Huduma na Sheria Zanzibar.

Alisema ni vyema kukaanzishwa mfumo maalum wa fidia ili mfuko huo usaidie waathirika wa matukio hayo kupata fidia.

“Tunashuhudia hukumu zinatolewa mahakamani mshtakiwa anapewa adhabu ya kutumikia kifungo, lakini hutakiwa alipe fidia ya fedha kwa ajili ya kupatiwa waathirika wa udhalilishaji, lakini fidia hiyo haipatikani,” alisema.

Alisema washtakiwa hao hushindwa kulipa fidia na hutumikia kifungo pekee kwa sababu hawana uwezo wa kifedha.

Aidha, alisema washtakiwa hao wanapokua gerezani wanahitaji kupatiwa elimu ya ushauri nasaha kwa sababu wengi wao huathirika kisaikolojia.

Alisema kituo cha huduma na sheria ni mdau muhimu wa mahakama hasa katika suala la uwakilishi wa mahakama za watoto na watu wanaohitaji msaada wa kisheria na kituo hicho kinaisaidia mahakama.

Akifungua kongamano hilo, Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Mgeni Jailan Jecha, alisema historia inaonesha kuwa kwa kipindi tofauti dunia ilipitia changamoto kubwa zilizovuruga haki za binadamu.

Alisema mwaka 1948 limepitishwa azimio muhimu kuweka misingi ya haki za binadamu duniani na tamko hilo lilifuatiwa na mikataba mingi ikiwamo wa haki za kitaifa kwa kijamii na kiuchumi ili binadamu popote alipo apatiwe haki zake bila ya pingamizi.

Alisema katiba zote za nchi zinatambua haki za binadamu na ili aishi vizuri kuna haki anahitaji kuzipata kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar.

Alisema amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa ni nguzo za kupatikana kwa haki za msingi za binadamu nchini kwa sababu nchi isiyo na amani na utulivu haiwezi kupiga hatua kwa maendeleo kwa kasi na ni kawaida haki za binadamu kuvurugwa.

“Mfano tukiwa na jamii inayoishi katika vurugu miundombinu ya maendeleo ikiwamo barabara, maji nayo huvurugwa, huduma za kijamii hukosekana, rushwa na ubadhirifu hushamiri, misingi ya utulivu na amani inasababisha haki kutekelezwa kwa ufanisi,” alisema.

Seif Maabadi kutoka Tume ya Haki za Binadamu, alisema tume hiyo inathamini mchango unaofanywa na asasi za kiraia kwa sababu mchango wao ni chachu kubwa katika utetezi na uhifadhi wa haki za binadamu.

Alisema upatikanaji wa haki upo rasmi zaidi na wananchi wengi ni wanyonge, majukumu yanayofanywa na asasi za kiraia ikiwamo kituo cha huduma na sheria ni majukumu ya msingi na yanastahiki kutekelezwa kwa nguvu zote ili kuisaidia serikali kufikia malengo iliyojiwekea. Aliyaja miongoni mwa malengo hayo kuwa ni ustawi wa haki za binadamu na ndio maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi wa Kituo cha Huduma na Sheria Zanzibar, Harusi Miraji Mpatani, alisema wananchi 1,1876 wakiwamo wanawake 60,203, wanaume 39,641 na watoto 18, 232 wamenufaika na elimu, msaada na ushauri wa kisheria kwa muda wa miaka 30 na kati yao, 18,860 wameshinda na kupata haki mbalimbali.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akisalimiana na Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Bishagazi, ambaye ni mmoja wa waliokuwa kwenye msafara uliozunguka maeneo mbalimbali nchini kupinga vitendo vya ukatili, katika Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara kurahisishiwa huduma bandarini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao (E- Government), Said Seif Said, amesema lengo la kuwa na kituo cha huduma jumuishi kwa wafanyabiashara bandarini ni kuwa na uchumi wa kidijitali na kurahisisha utoaji wa huduma.

Akizungumza mjini hapo na wadau wa Shirika la Bandari, alisema serikali mtandao imewafikia wafanyabiashara na kuhakikisha hawapati usumbufu na kuwa na urahisi wa kupata huduma hizo popote waliko.

Alisema lengo la serikali kuja na mifumo hiyo ni kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa umma zinapatikana kwa urahisi na mapato ya serikali kuwa imara zaidi. Mkurugenzi Said, alisema lengo ni kuona mzigo unafanyiwa kazi baada ya kuwasili bandarini na kupewa namba ya malipo kwa taasisi zote husika moja kwa moja bila ya mtu kupata usumbufu.

Alisema dhima ya serikali mtandao ni kuhakikisha huduma za TEHAMA ambazo ni habari teknolojia na mawasiliano utendaji wa serikali unafanyika kwa kutumia njia hizo na huduma nyingine kwa umma kwa njia ya kimtandao.

Alisema wamejipanga kuhakikisha mfumo huo unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na kwa haraka na usalama wakati wote ili kuhakikisha mapato ya serikali yanapatikana sambamba na udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato kwa asilimia 100.

Akizungumzia mfumo wa ununuzi mtandao, alisema lengo la mfumo huo ni kuondoa changamoto zote na watoaji huduma wengi walikuwa wakilalamika kwamba kuna upendeleo na kuweka mfumo ambao unapatikana katika masuala ya ununuzi kwa uwazi na urahisi.

Naye Mkurugenzi Utawala na Rasilimali Watu, Shirika la Bandari Zanzibar, Othman Simba Makame, alisema wapo tayari kuendeleza ushirikiano walioanza na tayari wameshatenga eneo kwa ajili ya kituo cha One Stop Center ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa urahisi na haraka.

Aidha, alisema eneo hilo litatumika kwa taasisi zote zinazotoa huduma katika utaratibu mzima wa utoaji na upakiaji wa mizigo kwa lengo la kuwaondolea changamoto wafanyabiashara wakubwa.

Alisema Shirika la Bandari limeanza kutengeneza eneo la upakuaji wa mizigo Bwawani wakiwa na lengo la kuondoa msongamano bandarini na kutumia kituo hicho kupunguza mrundikano wa mizigo ndani ya bandari.

Alisema anaamini wanapokwenda kuanza kwa mfumo huo watakutana na changamoto, lakini kama wadau kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (E- Government) pamoja na wafanyabiashara wapo tayari kupokea changamoto hizo ili kufikia ufanisi na uharaka wa utoaji wa huduma za mizigo.

## Serikali imeleta mapinduzi ya kijamii sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said, amesema serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, imekuja kuleta mapinduzi makubwa ya kijamii katika sekta ya elimu ikiwamo elimu mjumuisho.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa Kamati ya kusimamia mradi wa elimu mjumuisho huko kisiwani Pemba.

Alisema elimu hiyo inajumuisha watoto wote, jamii wasitafsiri ni ya watu wenye mahitaji maalumu pekee wakiwamo wenye ulemavu.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wafadhili ili vijana wote wapate elimu bora.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mradi huo kwa mwaka mmoja, Katibu wa Kamati ya kusimamia mradi wa Elimu Mjumuisho, Said Amour Abdalla, alisema kwa kipindi hicho mradi huo umefanya mambo mbalimbali ikiwamo usambazaji wa moduli za elimu mjumuisho (njia za ushirikishwaji wa elimu mjumuishi) katika shule 51 zilizoko kwenye shehia 15.


Pia kuzijengea uwezo jumuiya za watu wenye ulemavu kwenye masuala ya elimu mjumuisho ambayo ilikuwa na lengo la kuifahamu na kuifanyia utetezi.

Aidha, alisema kwa mwaka mzima wamepata mafanikio ili kuboresha uwelewa kwa kutoa maarifa na ujuzi kwa watu wenye ulemavu kupigania haki zao ikiwamo ya kupata elimu.

Mafanikio mingine alisema ni kuingizwa elimu mjumuisho katika mtaala wa vyuo vikuu, Mafunzo ya Elimu Mjumuisho kuwafikia walimu mbalimbali.

Alizitaja baadhi ya changamoto zikiwamo wakufunzi kulalamika kupewa posho sawa na washiriki, kupokea washiriki wasiostahiki wa mafunzo, umri wa washiriki wengi wao wakiwa wazee hali iliyosababishwa ushiriki duni. Pia alisema utekelezaji wa elimu mjumuisho ni tatizo hasa katika suala la miundombinu kutokuwa rafiki kwa majengo ya madarasa na vyoo pamoja na uchache wa walimu wenye taaluma na baadhi ya shule ukosefu wa vifaa vya nukta nundu na watumiaji wa lugha ya alama.

Wajumbe wa kamati hiyo waliishukuru serikali kwa kuwa na umakini wa kuharakisha mambo mbalimbali ambayo kamati walikuwa wakiyawasilisha.





# Misungwi wapanda miti 500,000 kukabili ukame

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

WILAYA ya Misungwi imepanda miti zaidi ya 500,000 katika maeneo ya ndani na nje ya wilaya hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, lengo kuu likiwa ni kudhibiti hali ya ukame katika baadhi ya maeneo.

Pia wilaya hiyo imejiwekea malengo ya kupanda miti zaidi ya milioni 1.5 ifikapo mwaka 2023.

Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS) wilayani Misungwi, Latipha Ally, alisema hayo juzi wakati wa upandaji wa miti 2,000 katika eneo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Akiwa katika upandaji wa miti hiyo alisema hatua hiyo imesaidia baadhi ya maeneo kuendelea kuwa ya kijani.

Latipha alisema katika juhudi hizo wamekuwa wakishirikiana na serikali pamoja na wananchi kuhakikisha wanafanikisha kuiwezesha Misungwi kuwa ya kijani wakati wote na kudhibiti hali ya ukame ambayo bado ipo katika baadhi ya maeneo.

Aliongeza kuwa kufuatia agizo la serikali la kupanda miche milioni 1.5 kila wilaya, tayari Wilaya ya Misungwi imeotesha miche zaidi ya 100,000 huku wakiendelea na hatua za kuotesha miche mingine ili kufikia idadi ya miche hiyo ndani ya mwaka 2023.

Aidha, aliwataka wananchi kushiriki kikamilifu katika kutekeleza jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu mbalimbali za wakala hao ili kujipatia miche ya miti kwa ajili ya kupandikiza katika makazi yao pamoja na maeneo muhimu yenye uhitaji.

Meneja TFS Wilaya ya Misungwi aliuomba uongozi wa serikali ya halmashauri hiyo kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya baadhi ya wafugaji wanaolisha mifugo yao katika maeneo yaliyopandwa miti na kusababisha miche hiyo kuharibika.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Misungwi, Petro Sabatto, aliwataka wafugaji kuwa waangalifu na kuepuka kulisha mifugo yao katika maeneo yaliyooteshwa miti.

Hivyo alitoa angalizo kwa mfugaji yoyote atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufunguliwa mashtaka.

Sabatto alisema Wilaya ya Misungwi itaendelea kutoa ushirikiano kwa TFS ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa misitu ili kuhakikisha wanakabiliana na hali ya ukame iliyotikisa ulimwengu kwa kipindi hiki.



Mkurugenzi wa Shirika la Fikra Mpya mkoani Shinyanga, Leah Josiah, akitoa elimu ya makuzi ili kujitambua, kujikinga na virusi vya Ukimwi na afya ya uzazi, kwa vijana rika balehe mkoani Shinyanga ili wajitambue na kuzifikia ndoto zao, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watoto yatima waomba msaada wa vifaa vya shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAHITIMU wa elimu ya msingi wanaolelewa katika Kituo cha Watoto Yatima cha Mvuma, wameomba msaada wa vifaa vya shule ili kuendelea na masomo ya sekondari mwakani.

Kituo hicho kilichoko katika Kata ya Nyasubi Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kina watoto yatima 32 kati yao wanaume ni 15 na wanawake 18.

Walitoa ombi hilo juzi baada ya kupokea msaada wa mchele, sabuni na sukari vikiwa na thamani ya Sh. 200,000 kutoka kwa Katibu Tawala wa Halmashauri ya Kahama, Timoth Ndanya na Mchungaji wa Kanisa la Sauti ya Mungu, Cahrles Lusakamila.

Mmoja wa wanafunzi hao Victoria Justine, alisema wanahitaji msaada wa vifaa vya shule ikiwamo nguo za shule, vitabu na madaftari ili kuendelea na masomo.

Alisema pindi wanapokosa vifaa hivyo wanashindwa kuendela na masomo ikiwa moja ya hatua inayofifisha ndoto zao walizojiwekea kielimu.

Naye Kibosha Gerald, aliiomba jamii isiwachoke kuwasaidia katika mahitaji mbalimbali wanayoyahitaji na pale wanapofaulu kuendelea na masomo yao basi wawapelekee shuleni kusoma au wawachukue na kuwasomesha kwani nao hawakupenda kuishi katika mazingira hayo.

Ofisa Ustawi wa kituo hicho, Lauren Noel, alishukuru kwa msaada huo na kuahidi kuwafikia walengwa wote na kuwasihi watu wengine kujitokeza na kusaidia mahitaji ya watoto kwani kituo kinamahitaji makubwa huku kikiwa na uwezo mdogo wa kujiendesha.

Alisema serikali imekuwa ikitoa msaada wa huduma ya afya na elimu, hivyo waliohitimu elimu ya msingi na kidato cha nne mwakani wataweza kuendelea na masomo yao.

Mchungaji wa Kanisa la Sauti ya Mungu, Cahrles Lusakamila, alisema katika vitabu vya dini vimeainisha kusaidia kundi la wajane, wazee na watoto yatima ili kupata ufalme wa Mungu, hivyo aliwasihi watu wengine kujitokeza na kulisaidia kundi hilo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndaya, aliiomba orodha kwa uongozi wa kituo hicho ya watoto waolifanya vema katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi ili kuangalia namna ya kuwasaidia na kutimiza ndoto zao kwa kupata vifaa vya shule kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

# Wanaowazuia watoto kwenda shule kutozwa faini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI wa Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, wametungiwa sheria ndogo ya kutozwa faini kwa wale ambao wanawazuia watoto wao kwenda shule.

Mtendaji wa kata hiyo, Hussen Majaliwa, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ilipotembelea kwenye kata hiyo.

Alisema wakati wa msimu wa kilimo wazazi wengi huwafanyia ukatili watoto wao kwa kuwanyima haki ya kielimu.

Alisema baadhi yao huwazuia kuhudhulia shuleni kwa ajili ya kwenda kulima na kukosa vipindi vya masomo, hali ambayo imewalazimu kutunga na kupitisha sheria ndogo ya kuzuia utoro kwa wanafunzi.

"Mwanafunzi wa shule ya msingi asipoonekana shuleni mzazi anatozwa faini ya Sh. 500 kwa siku moja, mwanafunzi wa sekondari Sh. 1,000," alisema Majaliwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga, Zacharia Ntemi, alisema wakati wa utungaji wa sheria hiyo wananchi walishirikishwa na kukubaliana, japokuwa kuna baadhi ya wazazi ambao bado wanakaidi.

Alisema siku ambayo mtoto anakwenda shuleni anakwenda na fedha ya siku zote ambazo amekaa nyumbani na kumlipa Mkuu wa Shule kwamba fedha hizo zinaingia kwenye mfuko wa shule.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Masengwa, Twalah Sawalehe, alisema utozwaji wa faini hiyo umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza utoro kwa wanafunzi hasa katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo.

Alisema kabla ya utozwaji wa fedha hizo, wanafunzi wengi walikuwa hawaendi shule kwamba wengi wao walikuwa wakipelekwa shambani kulima.

Mmoja wa wazazi katika eneo hilo, Amosi Magembe, alisema utozwaji wa fedha hizo umewakumbusha wazazi wajibu wao wa kuwapatia elimu watoto wao.

# Shambulio la Urusi mil 1.5 wakosa umeme Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema zaidi ya watu milioni 1.5 kwenye mji wa kusini wa Odessa wamekosa umeme jana baada ya Urusi kufanya mashambulizi ya usiku kucha kwa kutumia ndege zisizo na rubani.

Kiongozi huyo alisema jana kuwa hujuma zilizofanywa na Urusi kwa kutumia ndege zisizo na rubani ambazo zinashukiwa kuwa zimeundwa nchini Iran, zimeutumbukiza mji wa Odesa na vijiji vingine jirani kwenye giza.

"Hadi sasa, zaidi ya watu milioni 1.5 wa mkoa wa Odessa hawana umeme," alisema Zelenskyy.

Naibu Mkuu wa Ofisi ya Rais wa Ukraine Kyrylo Tymoshenko, alisema huduma ya umeme bado inapatikana kwenye maeneo muhimu ikiwamo hospitali na wodi za wanawake wajawazito, akieleza kuwa hali bado ni mbaya lakini inadhibitiwa.

Aidha, mamlaka za mji wa Odessa zilielezwa kwamba matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa yanaweza kuchukua muda wa kati ya wiki kadhaa au miezi mitatu.

Vile vile ilielezwa kuwa mji huo ulio kwenye mwambao wa Bahari Nyeusi ulikuwa kitovu cha shughuli za watalii wengi kutoka Urusi na Ukraine kabla ya vita kuanza.

Naye Gavana wa Mkoa wa Odessa, Maksym Marchenko, alisema droni za Urusi za kamikaze, zilifanya hujuma usiku kucha mwisho mwa juma lililopita na kwamba vikosi vya Ukraine vilifanikiwa kudondosha ndege mbili zisizo na rubani.

Mamlaka nchini Ukraine, ilisema majimbo ya kusini mwa nchi hiyo ndiyo yanapitia kipindi kigumu cha kukosekana kwa umeme baada ya mfululizo wa mashambulizi ya Urusi yanayoilenga gridi ya taifa.

Inatajwa kwamba Urusi ilianza kuilenga miundombinu ya umeme nchini Ukraine, baada ya kupoteza maeneo kadhaa kwenye uwanja wa vita na vikosi vya Kyiv kusonga mbele.

Alhamisi iliyopita, Rais wa Urusi Putin, alisema ataendelea kuihujumu gridi ya taifa ya Ukraine licha ya miito ya kutaka vikosi vyake vikomeshe mashambulizi yanayoilenga miundombinu ya kiraia.

Pia ilibainishwa kwamba hujuma hizo zimesababisha mgao mkubwa wa umeme nchini Ukraine katika kipindi cha sasa cha baridi kali.

**DW**

## Matumaini yaonekana kuwasili chanjo Ebola Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema chanjo ya virusi vya ebola aina ya Sudan ni moja kati ya chanjo tatu zilizopendekezwa kufanyiwa majaribio na jopo huru la wataalamu wa WHO.

Kwa mujibu wa ripoti ya WHO iliyotolewa mwishoni mwa juma lililopita, chanjo nyingine mbili zitaongezwa kwenye majaribio wakati dozi zitakapowasili nchi Uganda.


WHO ilisema kuwasili kwa moja ya chanjo tatu za majaribio ya ebola nchini Uganda kunaashiria hatua muhimu ya kihistoria katika uwezo wa kimataifa wa kukabiliana na milipuko.

"Dozi 1,200 za chanjo ya virusi vya ebola aina ya Sudan ziliwasili siku 79 baada ya mlipuko kutangazwa Septemba 20, mwaka huu," ilisema WHO.

Waziri wa Afya wa Uganda, Dk. Jane Acero, alisema nchi hiyo inaonyesha kuwa utafiti wa kuokoa maisha unaweza kupangwa mara moja katikati ya mlipuko.

**VOA**

**"Dozi 1,200 za chanjo ya virusi vya ebola aina ya Sudan ziliwasili siku 79 baada ya mlipuko kutangazwa Septemba 20, mwaka huu," ilisema WHO.**




Mfano wa chanjo ya majaribio ya virusi vya ebola aina ya Sudan. **PICHA: MTANDAO**

# Iran yatajwa kuwa mshirika wa Urusi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MSEMAJI wa Baraza la Usalama la Taifa la Marekani, John Kirby, amesema uhusiano wa Urusi na Iran umeongezeka hadi kufikia ushirikiano kamili wa ulinzi na kwamba Urusi inatoa msaada wa kijeshi ambao haujawahi kushuhudiwa.

Aliyabainisha hayo mwishoni mwa juma lililopita, na kuongeza kwamba nchi hizo mbili zinazingatia uzalishaji wa pamoja wa ndege zisizo na rubani.

Aidha, Australia ilitangaza kuwawekea vikwazo Wairani watatu na biashara moja ya Iran kwa kuipatia Urusi ndege zisizo na rubani za kutumia dhidi ya Ukraine.

Ushirikiano kati ya Urusi na Iran umebainishwa siku kadhaa, huku Ukraine ikiishutumu Urusi kwa kutumia ndege zisizo na rubani za Iran katika mashambulizi yake.

Kirby alisema kuwa ushirikiano kati ya Iran na Urusi katika kuzalisha ndege zisizo na rubani utakuwa na madhara kwa Ukraine, majirani wa Iran na jumuiya ya kimataifa.

"Urusi inataka kushirikiana na Iran katika maeneo ya utengenezaji wa silaha na mafunzo," alisema.

Aliongeza kuwa Marekani inahofia kwamba Urusi ilikusudia kuipa Iran silaha za hali ya juu za kijeshi, ikiwa ni pamoja na helikopta na mifumo ya ulinzi wa anga na kwamba Irani imekuwa mfadhili mkuu wa kijeshi wa Urusi.

"Urusi imekuwa ikitumia ndege zisizo na rubani za Irani kugonga miundombinu ya nishati na kuwanyima mamilioni ya Waukraine nguvu, joto na huduma muhimu. Watu wa Ukraine leo wanakufa kutokana na hatua za Iran," alisema.

Akijibu maoni ya Kirby, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, James Cleverly, alisema kuwa Iran imekuwa mojawapo ya waungaji mkono wakuu wa kijeshi wa Urusi na kwamba uhusiano kati yao unatishia usalama wa dunia.

Pia alisema mkataba huo mbaya kati ya nchi hizo mbili umeshuhudia Iran ikituma mamia ya ndege zisizo na rubani nchini Urusi.

"Kama hatua ya kuonyesha ushirikiano, Urusi inatoa msaada wa kijeshi na kiufundi kwa serikali ya Iran, ambayo itaongeza hatari inayoleta kwa washirika wetu katika Mashariki ya Kati na kwa usalama wa kimataifa," alisema.

Alisema Uingereza ilikubaliana na Marekani kwamba uungaji mkono wa Iran kwa jeshi la Urusi utaongezeka katika miezi ijayo huku Urusi ikijaribu kumiliki silaha zaidi, ikiwa ni pamoja na mamia ya makombora ya masafa marefu.

Ukraine iliishutumu Iran kwa kuipatia Urusi ndege zisizo na rubani zilizotumika katika mfululizo wa mashambulizi ambayo yaliua takriban watu wanane.

Inaelezwa kuwa Iran baadaye ilikiri kutuma idadi ndogo ya ndege zisizo na rubani nchini Urusi, miezi kadhaa kabla ya vita vya Ukraine.

Rais wa Ukraine Zelensky, alisema huo ni uwongo na kwamba Ukraine ilikuwa ikidungua takriban ndege 10 za Iran zisizo na rubani kwa siku.

Katika taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Australia, alisema usambazaji wa ndege zisizo na rubani kwa Urusi ni ushahidi wa jukumu la Iran katika kuyumbisha usalama wa kimataifa na kwamba orodha hiyo inaangazia wale wanaotoa msaada wa mali kwa Urusi watakabiliwa na athari zake.

**BBC**

HABARI KITAIFA

# Abiria Kituo cha Magufuli walia nauli mabasi kupaa

**Na Jenifer Gilla**

ABIRIA katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia kupandishiwa nauli na baadhi ya mawakala, tofauti na bei elekezi zilizotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Kituo hicho cha mabasi kinahudumia mabasi yanayofanya safari ndani na nje ya nchi.

Wakizungumza na Nipashe abiria waliofika katika kituo hicho pia walilalamikia ugumu wanaoupata wakati wa kukata tiketi kwa njia ya mtandao, wakieleza kuwa hiyo ni mojawapo ya sababu inayowalazimu kwenda kulipia kwa njia ya kawaida na kuishia kupata kadhia ya kutozwa nauli zaidi.

Abiria, Hawa Mohamed, alisema alipiga simu kwenye moja ya gari linalofanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Moshi, akaomba nafasi akaambiwa atapata ila hataweza kulipia hadi siku ya kusafiri kwa kuwa nauli inabadilika mara kwa mara.

"Niliambiwa na utingo wa basi hilo kuwa nauli zinabadilika tunakuruhusu kushika nafasi ila hatutapokea fedha yako maana ikifika usiku bosi (mmiliki) ndiye anayepanga nauli itakayokatishwa siku ya safari," alisema.

Jumamosi aliambiwa nauli zimepanda hadi Sh. 33,000 na hiyo ni kutokana na uamuzi uliotolewa na mmiliki wa basi na kulazimika kulipia gharama hiyo.

"Aliniambia nauli ni Sh. 33,000 mwenye basi ametujulisha jana usiku tuuze hivyo, kama hutaweza basi nafasi tutamuuzia mtu mwingine, sisi tunafuata maelekezo ya mmiliki wetu, ametuambia zitaendelea kuongezeka tunavyokaribia sikukuu," alisema.

Tudea Michael aliyekuwa akisafiri kuelekea Iringa alisema alilazimika kuchelewa kupata basi kituoni baada ya mabasi yaliyokuwa yanaondoka asubuhi kutoza nauli ya Sh. 30,000 badala ya Sh. 24,000 iliyopangwa.

"Nimefika hapa saa 11:30 asubuhi mabasi yote ya asubuhi yanataka nauli ya Sh.30,000 wakati mimi najua nauli mpaka Iringa ni Sh. 24,000 na ndiyo niliyonayo, imenibidi nilipie basi linaloondoka saa 4: 00 asubuhi, ndio nalisubiri hapa, kwa kweli kuna haja ya serikali kuingilia kati maana huko mbele nauli zitafika Sh. 100,000," alisema Michael.

Mwanahamisi Rashidi, alilalamikia huduma ya kulipia tiketi kwa njia ya mtandao kuwa na tatizo ya kutokupokea malipo hali inayowalazimu abiria kuja kukatia tiketi katika kituo hicho na wengine kutapeliwa au kulipishwa nauli zaidi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, alisema watafuatilia kwa kina.

Alisema mtu yeyote atakayebainika anahusika na tabia hiyo ya kupandisha nauli bila kufuata utaratibu uliopangwa adhabu kali zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema huduma ya malipo kwa njia ya mtandao bado inatatizo kwa kuwa sio magari yote yaliyojisajili kupokea wateja kupitia mtandao.

Aliwasihi abiria kutumia tovuti ya LATRA ili kuangalia nauli za magari yote ya mikoani pamoja na kujiridhisha gari analotaka kupanda kama limesajiliwa na lina leseni ili kuepuka usumbufu wa kutapeliwa.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Abdallah Mohamed, alisema tabia ya kupandisha nauli inafanywa na baadhi ya mawakala wa mabasi ambao sio waaminifu.




Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal (katikati), akipokea msaada wa gari kwa Ofisa wa Kampuni ya CMC, Jenifer Gower, ili kuchangia katika mradi wa klabu hiyo wa kutoa madawati kwa shule za msingi za umma. Kushoto ni mwanachama mkongwe wa klabu hiyo na mwanahabari, Hamza Kassongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni Re/Max Omela yatoa ajira 1,470

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya RE/MAX OMELA Zanzibar imesema uwekezaji wa kigeni wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 320 umefanyika na kufanikiwa kutoa ajira za kudumu kwa watu 1,470 tangu ilipoanza kutoa huduma mwaka 2016.

Takwimu hizo zimetolewa na Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Jemes Prevost, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini, katika hafla ya uzinduzi wa ushirikiano kati ya kampuni yake na ya ubunifu wa mambo ya ndani Tanzania ya jijini Dar es Salaam, Dolson Interiors.

Prevost alisema kampuni ya RE/MAX imevutia kiwango hicho cha uwekezaji baada ya kufanikiwa kulitumia soko la Ulaya na Afrika kuvutia wawekezaji sekta ya utalii na nyumba za makazi visiwani humo.

"Mafanikio haya makubwa na yanayoonesha jinsi wafanyakazi, wateja na washirika wetu wanavyothamini kazi yetu jambo ambalo limesaidia kukuza maendeleo ya sekta ya utalii na maendeleo ya nyumba za makazi," alisisitiza.

Jemes alisema kampuni hiyo imeanzishwa mwaka 1973 nchini Marekani kabla ya kuanza kutoa huduma zake Zanzibar mwaka 2016 katika Ukanda wa Pwani wa Mashariki maeneo ya Paje, Jambiani, Bwejuu na Michamvi hasa maeneo yanayokuwa kwa kasi ya uwekezaji vitega uchumi.

Alisema sekta ya utalii na nyumba za makazi zina umuhimu mkubwa katika kuharakisha maendeleo ya Zanzibar pamoja na kuongeza ajira kwa vijana.

Kadhalika wawekezaji wengi kupitia kampuni yake ni wazungu wakichukua asilimia 54 ya jumla ya miamala ikifuatiwa na asilimia 34 kutoka Afrika, sita kutoka Mashariki ya Kati, asilimia nne kutoka Bara la Asia na asilimia mbili wakitokea Afrika ya Kaskazini.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021 nchi zinazoongoza kwa uwekezaji vitenga uchumi Zanzibar ni Tanzania asilimia 28, Poland asilimia 11 Ujerumani na Ufaransa miradi mingi ikiwa ya Hoteli za Kitalii.

Aidha, alisema tangu kampuni hiyo ilipoanza kutoa huduma Zanzibar, vijana 150 wamefundishwa kazi ya udalali na uwakala na kuwataka wajasiriamali kuanzisha vikundi ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa na kampuni hizo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya kuongeza thamani ya kazi za sanaa Tanzania ya Dolson Interiors, Jamila Hemani, alisema wameamua kuanza kutoa huduma Zanzibar kwa kushirikiana na kampuni hiyo kwa wawekezaji sekta ya utalii na wananchi wa kawaida ili kutangaza mambo ya sanaa na vifaa vya matumizi ya nyumbani vya utamaduni.

Alisema kuanza kupatikana huduma hizo Zanzibar pia kutafungua fursa kwa wajasiriamali kunufaika na mafunzo kupitia kazi za mikono pamoja na kunufaika na masoko ya uhakika yakiwamo ya ndani ya nchi pamoja na nje ya nchi.

Alisema bidhaa zinazotengenezwa na kampuni yake tangu kuanzishwa miaka 15 jijini Dar es Salaam ni mazuria, magodoro, vitambaa vya samani, karatasi za ukuta, na mambo ya usanifu katika hoteli na nyumba za makazi.

Meneja wa Kampuni ya REX/MAX OMELA, Veronica Mlega, alisema kampuni hiyo ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya sekta ya utalii na nyumba za makazi visiwani humo.

Alisema huduma za uwakala wa udalali zinazotolewa na kampuni hiyo zimezingatia ubora wa kimataifa na kuwezesha kuvutia uwekezaji wa kigeni wenye thamani ya mtaji wa Dola za Marekani milioni 320 ikiongozwa na miradi ya sekta ya utalii.

Kampuni ya RE/MAX OMELA iliyoanzishwa mwaka 1973 huko Denver, Colorado nchini Marekani imefanikiwa kuwa na ofisi 800 duniani na mawakala wa mali isiyohamishika 135,000 katika nchi 115 ikiwamo Tanzania.

# Watoto wawili wa familia moja wadaiwa kukeketwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO wawili wenye umri kati ya miaka 14 na 16 wa familia moja, wakazi wa kijiji cha Katenge, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoa wa Njombe wametajwa kukeketwa kwa kipindi cha mwishoni mwa mwaka 2021.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Maryam Muhaji, wakati wa kuhitimisha kilele cha siku 16 za kupinga ukatili.

Muhaji aliwataka wakazi wa kijiji cha hicho kuachana na mila potofu za ukeketaji ambazo zinaweza kuleta madhara ya kiafya na kisaikolojia kwa watoto wa kike. "Eneo hili la Katenge mwishoni mwa mwaka jana kulitokea ukatili wa hali ya juu sana, ukatili wa kukeketa watoto wa kike wenye umri chini ya miaka 16 katika kijiji hiki ni uchungu na kwa kweli unatuumiza sana na nasikia bado unaendelea kuna kinamama ndio kazi zao kama mpo kwenye hili kundi naomba mrudi kwa Mwenyezi Mungu," alisema Muhaji.

"Mlichokitenda kwa watoto hawa sio haki, watoto wadogo chini ya umri wa miaka 16 bado hata hawajaenda sekondari ni wadogo mno mnaendekeza ukeketaji, mila potofu ambazo zinapigwa vita na zinaendelea kukemewa na taifa letu, hili ni eneo pekee ambalo linafanya ukeketaji katika wilaya nzima kwa watoto wadogo," alisema.

Muhaji alikemea mila hiyo potofu na utamaduni wanayotumia kumwandaa mtoto wa kike kwa maisha ya ndoa, kufanya hivyo ni kumnyima haki zake.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Onesmo Lyandala, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya Lauter Kanoni, aliwataka wananchi hao kuacha mila potofu na wapige vita ukeketaji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Yusta Mwambembe, alisema mwishoni mwa mwaka 2021 kulifanyika ukeketaji kwa watoto chini ya miaka 16 wakiwa na imani kwamba wasipofanyiwa hawataolewa. "Kutokana na hivyo imekua ni lazima wawafanyiwe, lakini hivyo vitu wanavifanya kwa kificho mno, baada ya kukemea kama hata watakuwa wanafanya kwa kificho sana. Na serikali kuendelea kukemea na baadhi ya watu kuchukuliwa hatua wamekua hawafanyi labda kama wanafanya kwa kuiba sana," alisema Mwambembe.

Sara Mvehelo, anayeishi kijiji hicho, alisema kuwa mila na desturi za ukeketaji zilikuwapo zamani kipindi cha mababu, lakini hivi sasa zimeonekana kurudi.

Mwenyekiti wa kijiji cha Katenge, Hussen Nyamle, alisema wakati wanafanya sherehe za ukeketaji walimualika, lakini hakwenda.

"Ni jambo la ajabu baada ya kusikia ndio maana kuna watu walilaumu baada ya kusikia sikuonekana, jambo la ukeketaji ni baya sana, wapo watu walikuwa wanajinafasi wanasema kuwa usipokeketwa huwezi kuolewa ni vitu ambavyo vya upotofu na waliokuwa wanafanya wakaungame kabisa," alisema Nyamle.

# Davido kufunga sherehe Kombe la Dunia Qatar

**LAGOS,** Nigeria

NYOTA wa Afropop kutoka Nigeria, Davido, anatarajiwa kutumbuiza katika tamasha la kufunga mashindano ya Kombe la Dunia mwishoni mwa wiki hii nchini Qatar.

Hiyo itakuwa mara ya kwanza kabisa kwa Davido kuonekana hadharani tangu kifo cha mwanawe wa kike, Ifeanyi, aliyefariki wiki kadhaa zilizopita baada ya kuzama katika bwawa la kuogelea nyumbani kwao Lagos.

Habari za Davido kutumbuiza katika sherehe za kufunga Kombe la Dunia zilifichuliwa na rafiki yake mfanyabiashara kutoka Hong Kong, Stephen Hung.

Kumbuka kwamba nyota huyo wa muziki hapo awali alipewa kadi ya kutumbuiza kwa wimbo wa Kombe la Dunia kwenye sherehe za ufunguzi, lakini hakuweza kwenda baada ya kumpoteza mwanawe, Ifeanyi.

Kwa mujibu wa Hung, ana furaha sana kwamba Davido amethibitisha kuwa atakuwa kwenye hafla ya kufunga mashindano hayo makubwa zaidi ya soka duniani.

Aliandika: "Nimefurahi sana kaka yangu Davido alithibitisha kuwa atatumbuiza kwenye sherehe za kufunga Kombe la Dunia Qatar. Siwezi kungoja kumuona huko."





# WEMA, IRENE KUCHUANA MSANII BORA WA KIKE

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII aliyetingisha kwenye filamu ya 'Kombolela', Shamila Ndwangila' Bi Star', ametajwa kuwa mmoja wa wasanii watakaochuana katika kipengele cha msanii bora wa kike katika tuzo za filamu.

Orodha ya wateule hao ilitangazwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu, Emmanuel Ndumukwa, kwenye mkutano na waandishi wa habari.

Katika kipengele cha msanii bora wa kike waliotajwa kuchuana ni Bi Star aliyeigiza kama Mwadawa kwenye Filamu ya 'Kombolela'.

Mastaa wengine waliotajwa katika kipengele hicho ni Wema Sepetu aliyeigiza kama Malkia katika Filamu ya 'Malkia'.

Pia yupo Irene Paul aliyeigiza kama Tanasha katika Filamu ya 'Yalaiti'.

Wasanii wengine waliotajwa ni Thecla Mjata, Nyota Waziri ambaye ni mwanamuziki anayefanya vizuri kwenye uga wa uigizaji na Tunu Mbegu.

Ndumukwa amesema kuwa tuzo hizo zinatarajiwa kutolewa Jumamosi wiki hii jijini Arusha ambapo wasanii 162 watachuana huku filamu 60 zikishindanishwa.

# *Mbosso: Sina ushikaji na Harmonize*

**Na Mwandishi Wetu**

MKALI wa nyimbo za mahaba kwenye muziki wa Bongo Fleva, Mbosso, amesema kwamba, yeye hajawahi kuwa na ukaribu au ushikaji na msanii mwenzake, Harmonize.

Mbosso amesema kuwa kwenye maisha yake hajawahi kabisa kuwa na ushikaji na Harmonize, kwani kila mmoja yupo bize na ishu zake.

Katika mahojiano na kituo kimoja cha redio, Mbosso alisema hataki kumzungumzia sana Harmonize kwa sababu hakuwa 'mwana' kwake.

"Sijawahi kuwa na ushikaji na Harmonize tangu tukiwa wote kwenye Lebo ya Wasafi, hivyo siwezi sana kumzungumzia," alisema Mbosso. "Hiyo haimaanishi kwamba, nina shida naye, hapana, tumetokea tu kutokuwa washikaji wala ukaribu."



# MAELFU WAKUNWA KILELE CHA BOOMPLAY CAMPUS MWANZA

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

BOOMPLAY, app inayoongoza katika utoaji wa huduma ya kusikiliza na kupakua muziki barani Afrika kwa kushirikiana na Jukwaa la Kuwezesha Vijana la Benki ya NMB 'Go na NMB' imepeleka burudani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu jijini Mwanza kupitia tamasha kubwa la Boomplay Campus Tour.

**Tamasha hilo lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Mt. Augustino Tanzania (SAUT) jijini Mwanza Jumamosi iliyopita, lilihudhuriwa na zaidi ya wanafunzi 6,000.**

Lilianza kwa wanafunzi kushiriki katika michezo mbalimbali kama vile mechi za mpira wa miguu, Usajili wa akaunti na mashindano ya kuimba ambapo wanachuo waliweza kushindana na kuwajengea utamaduni wa kucheza michezo na kukuza vipaji vyao.

Baada ya hapo hafla hiyo ilitawaliwa na mazungumzo kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwamo timu kutoka 'Go na NMB' pamoja na Uongozi wa Chuo cha Mt. Agustino. Wadau hao walizungumza na wanafunzi jinsi ya kujitambua na kukuza vipaji vyao, elimu ya matumizi sahihi ya fedha, fursa zilizoko kwenye soko la muziki hasa wa kidijitali, lakini jinsi ya kujiandaa baada ya kuhitimu masomo yao.

Muda wa usiku wasanii kadhaa walipanda jukwaani kutoa burudani akiwamo Stamina, Meja Kunta, Moni Centrozone na baadhi ya wasanii wa jijini Mwanza walipata fursa ya kuonyesha vipaji vyao na kuwapa mashabiki burudani nzuri.

Stamina na Moni Centrozone walitoa burudani ya kuvutia kupitia ngoma zao za Hip-hop huku Meja Kunta akifanya maajabu kupitia nyimbo zake za muziki wa singeli na kuhakikisha mashabiki wote wanaburudika bila kuchoka.

Katika taarifa iliyolewa kwa vyombo vya habari, Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli, alisema: "ziara za Campus Tour zinalenga kuimarisha uhusiano kati ya Boomplay na wanafunzi wa vyuo vikuu kwani vijana ni mabalozi wazuri wa App ya Boomplay, hivyo maamuzi ya kufanya matamasha kama haya ni katika kuhakikisha wanawafikia vijana kwa kugusa vitu wanavyovipenda."

Kwa upande wa Meneja Uhusiano-Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Robert Mtimba, alisema, "Tunajivunia sana kuwa sehemu ya shughuli hii, kwa miaka mingi lengo letu limekuwa kuungana na vijana kuhakikisha tunagusa vitu wanavyovipenda. Kama taasisi, tunaahidi kuendelea kusaidia vijana huku lengo kuu likiwa ni kuwapa fursa nyingi za uwezeshaji, elimu ya kifedha pamoja na kuelewa matumizi na faida za huduma za kidijitali za benki husunan NMB Lipa Mkononi, Mshiko Fasta na NMB Pesa Wakala."



Msanii wa Hip-hop nchini, Bonventure Kabogo maarufu Stamina, akitoa burudani kwa wanafunzi jijini Mwanza kupitia Tamasha la Boomplay Campus Tour lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT) jijini humo Jumamosi iliyopita. Tamasha hilo lilihudhuriwa na wanafunzi zaidi ya 6,000 kutoka katika vyuo mbalimbali vya jiji hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPLB yakiri waamuzi bado tatizo Ligi Kuu

**Na Hadija Mngwai**

WAKATI mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukitarajiwa kuanza kutimua vumbi Alhamisi wiki hii, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Steven Mguto, amesema suala la waamuzi bado limekuwa likiwasumbua na kwamba hawajapata ufumbuzi.

TPLB imetoa tathmini ya mzunguko wa kwanza baada ya kufikia tamati kwa timu zote 16 kucheza mechi 15 za raundi ya kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Mguto alisema mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara umekwenda vizuri kutokana na kutopata malalamiko kutoka kwa wachezaji na klabu isipokuwa upande wa waamuzi kumekuwa na changamoto zinazowasumbua.

"Mzunguko wa kwanza umekwenda vizuri hatujapokea malalamiko kutoka kwa wachezaji kucheleweshewa mishahara yao wala timu kulalamikia kufika katika eneo la kituo.

"Lakini kitu ambacho tunakiona tunafeli, hatujakiweka sawasawa ni suala la 'marefarii', hili suala linatusumbua sana, kweli ni binadamu tunaamini hawakosi mapungufu, lakini binadamu wenyewe kila siku wafanye makosa?

"Tutajitahidi kukaa na 'marefarii' na kamati yao tuangalie shida ni nini haswa ili tuanze kutatua, huko ndiko kidogo tulikokwazika," alisema Mguto na kuongeza:

"Maendeleo ya ligi ni mazuri, timu inaweza kushinda popote ugenini na hakuna ile dhana kuwa lazima timu fulani ikija itafungwa, hiyo imeondoka ilikuwa ushamba fulani watu walikuwa wanalazimisha matokeo kwa hali yoyote ile lakini sasa hivi timu yoyote inashinda popote.

"Mzunguko wa pili utakuwa mgumu sana watu wameona mapungufu katika timu zao watarekebisha dirisha dogo, tutegemee kuwa mgumu".

Hadi mzunguko wa kwanza unamalizika, Yanga ndiyo iko kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 38, tatu mbele ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili na nne zaidi ya Simba iliyoko nafasi ya tatu.

Kwa upande wa tatu zilizofunga mzunguko wa kwanza kwa kuburuza mkiani Polisi Tanzania yenye pointi tisa mkiani ikifuatiwa na Ruvu Shooting na Ihefu FC zenye pointi 11kila moja katika nafasi ya 14 na 13.

# Kocha Simba atua Yanga

**Na Adam Fungamwango**

SIKU tatu chache tu baada ya kumtimua Kocha Edna Lema, Klabu ya Yanga imemteua aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastin Mkoma (pichani chini), kuwa Kocha Mkuu wa timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess.

Taarifa iliyotolea jana na klabu hiyo imeeleza kuanzia sasa kocha huyo ndiye atakayekinoa kikosi hicho ambacho kwa sasa kinajiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara Jumatano ijayo dhidi ya Mkwawa Queens kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam na huo utakuwa ni mtihani wake wa kwanza.

Akizungumza baada ya kutambulishwa, Mkoma alisema amejiunga na Yanga Princess kwa ajili ya kupata mafanikio.

"Kuna vitu vitatu ambavyo vinaweza kukufanya utamani kuifundisha Yanga Princess. Ni timu kubwa, ina kikosi kizuri na kuna uongozi imara, niko hapa kuhakikisha tunapata mafanikio," alisema kocha huyo.

Klabu ya Yanga ilimtimua Lema na kocha wake msaidizi Mohamed Hussein 'Mmachinga' baada ya mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Jumatano iliyopita dhidi ya Fountain Gate ambayo wapokea kichapo cha bao 1-0.

Mkoma aliondoka Simba Queens Oktoba mwaka huu baada ya klabu hiyo kupata kocha mpya, Charles Lukula kutoka She Corporate ya Uganda ambaye alikwenda nayo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yaliyofanyika nchini Morocco na kushika nafasi ya nne.

Mkoma ambaye alijiunga na Simba Queens Novemba mwaka jana kuchukua nafasi ya Hababuu Ally, aliiwezesha timu hiyo kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara pamoja na wa CECAFA ulioipa tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANTE ATAKIWA BARCA

KLABU ya Barcelona inaweza kumsajili kiungo wa Ufaransa, N'Golo Kante, 31, ambaye mkataba wake na Chelsea unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Sport)***

### MILAN KUMPOTEZEA ZIYECH

AC Milan inaweza kuachana na mpango wa kumsajili winga wa Chelsea, Hakim Ziyech, 29, kwa sababu ya mshahara mkubwa unaotakiwa na raia huyo wa Morocco. ***(Gazzetta Dello Sport, via Football Italia)***

### SPURS YAMTAKA DE VRIJ

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Stefan de Vrij, 30, kutoka Inter Milan Januari. Atletico Madrid pia inamwania mchezaji huyo ambaye atakuwa huru kipindi cha majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ALLISTER AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Tottenham Hotspur, Juventus, Inter Milan na Atletico Madrid zinamwania kiungo wa Brighton, Alexis Mac Allister, 23. ***(Fichajes)***

### RONALDO AANIKWA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, alikuwa tayari kumuachia fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, aondoke Agosti, lakini klabu kadhaa zilikataa kumsajili mchezaji huyo. ***(Athletic)***

### ZAHA AWANIWA ARSENAL

ARSENAL na Chelsea zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili fowadi wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 30, kutoka Crystal Palace. ***(Teamtalk)***

### SKRINIAR AWINDWA

KLABU ya Newcastle inaongoza katika mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Slovakia, Milan Skriniar, 27, kutoka Inter Milan. ***(Calciomercato)***

### BERGE KWA CHELSEA, LIVER

CHELSEA na Liverpool zote zinawania kumsajili kiungo wa Norway, Sander Berge, 24, kutoka klabu ya Sheffield United. ***(Jeunesfooteux)***

### SMALLING AFUATILIWA ITALIA

JUVENTUS imejiunga kwenye mbio moja na Inter Milan kufuatilia hali ya mlinzi wa kati wa England, Chris Smalling, 33, ambaye atakuwa huru kipindi cha majira ya joto mkataba wake utakapokuwa umemalizika kule AS Roma. ***(Sky Sports Italia)***


### MKOREA KUULA UNITED

KLABU ya Manchester United imefufua mpango wake wa kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa Napoli, Kim Min-jae, 26, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Real Madrid kwa mchezaji huyo kutoka Korea Kusini. ***(Sunday Mirror)***

### OUNAHI ANUKIA SEVILLA

KLABU ya Sevilla inawania kumsajili kiungo wa Angers, Azzedine Ounahi, 22, ambaye ameonyesha ubora wa hali ya juu akiwa na Morocco kwenye Kombe la Dunia Qatar. ***(Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KANE: NILAUMIWE MIMI KUTOLEWA KWA ENGLAND

**DOHA,** Qatar

HARRY Kane amesema kwamba yeye ndiye aliyechangia kwa kiasi kikubwa kuondolewa kwa England kwenye michuano ya Kombe la Dunia baada ya kukosa penalti yake ya dakika za lala salama.

**England iliondolewa na Ufaransa kwa mabao 2-1 Jumamosi usiku katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na Kane amesema "nalazimika kukabiliana" na makosa yangu.**

England walionekana kuwa kwenye kiwango kizuri dhidi ya Ufaransa katika mchezo huo kwenye Uwanja wa Al Bayt, huku Kane akisawazisha bao la kwanza la Aurelien Tchouameni kwa penalti, baada ya Bukayo Saka kuchezewa madhambi eneo la hatari.

Hata hivyo, Olivier Giroud alirejesha uongozi kwa kufunga bao la pili kwa Ufaransa zikiwa zimesalia dakika 12, na Kane hakuweza kufunga tena baada ya penalti ya pili dakika sita kabla ya mchezo kumalizika, akipiga juu ya lango.

Kosa hilo lilimfanya Kane kupoteza nafasi ya kumpita Wayne Rooney kama mfungaji bora wa muda wote wa England kwa bao lake la 54 la kimataifa, huku 'Simba Watatu' hao wakiondolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia kwa mara ya saba katika rekodi ya michuano hiyo.

> Kama nahodha na yule aliyekosa penalti, ninawajibika kwa hilo, siwezi kulaumu maandalizi...

Akizungumza na BBC Sport baada ya mchezo huo, Kane ambaye ni nahodha wa England alitanguliza makosa yake na kuwasifu wachezaji wenzake kwa kucheza vizuri.

"Ni vigumu kuchukua kwa ajili yangu binafsi na kwa timu," alisema. "Singeweza kujivunia vijana. Tulikuwa na vipindi bora, nafasi nzuri zaidi, lakini soka inategemea mambo madogo.

"Kama nahodha na yule aliyekosa penalti, ninawajibika kwa hilo, siwezi kulaumu maandalizi yangu au maelezo kabla ya mchezo.

"Nilijisikia kujiamini kupiga, sikuitekeleza vile nilivyotaka. Itakuwa kitu ambacho lazima niishi nacho na kwa muda mrefu.

"Timu iko katika nafasi nzuri sana na kutakuwa na hali ya juu siku za usoni. Kwa kusimama hapa sasa, tumechoka imefika mwisho kwani tulikuwa na imani kamili kwamba tunaweza kufika mbali. Tunaweza kujivunia kile tunachofanya."

Kane ndiye mchezaji wa kwanza kufunga na kukosa penalti katika mechi ya Kombe la Dunia (bila mikwaju ya penalti) tangu Michal Bilek alipoifungia Czechoslovakia dhidi ya Marekani mwaka 1990.

Amefunga penalti nyingi za Kombe la Dunia kuliko mchezaji yeyote (nne).

Kosa hilo linamfanya Kane kuwa sawa na Rooney aliyefunga mabao 53 England, na nyota huyo wa Manchester United alionyesha kumuunga mkono nahodha huyo baada ya kupoteza.

"Nimechoshwa na vijana, lakini wanajivunia jinsi walivyocheza michuano hii na wanapaswa kujivunia," aliandika Rooney kwenye Twitter. "Hongera Harry Kane kwa kusawazisha rekodi hiyo, atakuwa peke yake hivi karibuni na sikuweza kufikiria mtu yeyote bora kuchukua nafasi hiyo."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
SUNDERLAND
VERSUS
WEST BROMWICH
1 | 2.87
X | 3.21
2 | 2.38

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SANTOS HAJUTII RONALDO KUANZIA BENCHI URENO



**AL THUMAMA,** Qatar

KOCHA wa Ureno, Fernando Santos, amesema "sijutii" kwa kutomwanzisha Cristiano Ronaldo baada ya kutolewa na Morocco kwenye Kombe la Dunia hatua ya robo fainali Jumamosi.

Ronaldo aliwekwa benchi hadi dakika ya 51 wakati Ureno wakiwa wamefungwa 1-0, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, hakuweza kufanya lolote Morocco ikiwa timu ya kwanza ya Afrika kutinga nusu fainali kwenye Kombe la Dunia.

Ronaldo alionekana akitoka uwanjani na kilio mwishoni mwa mchezo huo na pia aliachwa benchi wakati Ureno ikishinda 6-1 dhidi ya Uswisi katika hatua ya 16-bora.


"Sidhani hivyo, hakuna majuto," alisema Santos. "Nadhani hii ilikuwa timu ambayo ilicheza vizuri sana dhidi ya Uswisi. Cristiano Ronaldo ni mchezaji mzuri, aliingia wakati tuliona ni muhimu, kwa hiyo hakuna majuto.

"Ikiwa tutachukua watu wawili ambao walikasirishwa zaidi ni Cristiano Ronaldo na mimi mwenyewe. Bila shaka tumekasirika, lakini hiyo ni sehemu ya kazi ya kocha na mchezaji."

Morocco ilishinda kwa bao la kichwa lililofungwa na mshambuliaji wa Sevilla, Youssef En-Nesyri kipindi cha kwanza alipomshinda kipa wa Ureno, Diogo Costa na kufunga bao la kihistoria kwa taifa lake.

Ureno waliweza kupiga mashuti matatu tu yaliyolenga lango walipokuwa wakitafuta bao la kusawazisha, na baadaye Bruno Fernandes alimkosoa sana mwamuzi wa Argentina, Facundo Tello.

"Sijui kama watatoa kikombe kwa Argentina," alisema Fernandes.



# Dalot kujifunga tena Unite

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa kulia wa Klabu ya Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Diogo Dalot, inaelezwa klabu hiyo iko kwenye hatua za mwisho za kumwongezea mkataba wa kuendelea kusalia klabuni hapo.

Beki huyo wa pembeni wa Man United ambaye alijiunga klabuni hapo mwaka 2018 ukiwa usajili wa kocha Mreno Jose Mourinho, alikuwa hapati nafasi mara kwa mara klabuni hapo kutokana na uwezo wake kutokuwaridhisha makocha waliokuwapo.

Dalot amefanikiwa kuonyesha ubora mkubwa sana tangu kuja kwa kocha mpya ndani ya Man United msimu huu, na amekuwa kwenye ubora mkubwa mpaka kufikia kumshawishi Eric Ten Hag na kumfanya kuhitaji aongezewe mkataba.

Man United ina mpan
go wa kuingia soko
kutafuta beki wa kul
ambaye atasaidiana n
beki huyo wa Kiren
kwani wana mpango w
kumuuza beki wa kul
wa timu hiyo, Aaro
Wan Bissaka kutokan
na kutomvutia Ten Hag

Dalot alikuwa n
Timu ya Taifa ya Uren
kwenye michuano y
Kombe la Dunia nchin
Qatar kabla ya kuon
dolewa juzi na Moroc
co.

CHEZA USHINDE KASINO

# MGUNDA AANIKA SABABU KIKOSI KAMILI KUIVAA EAGLE

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi mnono wa mabao 8-0, walioupata Simba dhidi ya Eagle FC juzi kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda amesema ni sehemu ya maandalizi kuelekea duru la pili la Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Simba juzi ilianza vizuri michuano ya Shirikisho kwa kufanikiwa kuibuka na ushindi huo katika mchezo huo wa hatua ya pili ya ASFC, uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam juzi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema alilazimika kuwatumia baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza katika mchezo huo dhidi ya Eagle FC kwa ajili ya kupata matokeo, lakini ni sehemu ya maandalizi ya duru la pili la Ligi Kuu.

Alisema walikuwa hawaijui Eagle FC wala hawakuwahi kuiona ikicheza hali iliyowalazimu kuanza na sehemu kubwa ya kikosi kilichozoeleka kwa kuwa ni vigumu kucheza na timu ambayo huifahamu ubora wake wala upungufu, hivyo kuamua kupanga kikosi kamili na baadaye kuingiza wale ambao hawakupata nafasi sana.

“Haya ni mashindano hutakiwi kumdharau yeyote, bahati nzuri tumecheza na timu ambayo hatuifahamu ila wanatufahamu, mchezo huu tumeuchukulia umuhimu kama mechi nyingine tulilazika kutumia wachezaji wote,” alisema Mgunda na kuongeza:

“Ukiachilia mabao tuliyopata kuna kitu ambacho nakifanyia kazi, ilikuwa mechi muhimu ya kufanyia kazi yale tuliyofanya mazoezi. Mechi hii ni sehemu ya maandalizi ya duru la pili kufanya vizuri.

“Nimelazimika kuwapa nafasi Nelson Okwa na Victor Akpan walikosa muda wa kucheza kwa sababu ya kuwa majeruhi na wamerejea na kuwapa hii mechi kuanza kuwarudisha katika kiwango chao na kuwajenga kuwa fiti.”

USHINDI...



Timu ya mpira wa miguu ya Vyombo vya Usalama ya Muheza, Tanga wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya timu ya madiwani wa Halmashauri ya Muheza katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Jitegemee. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Simba yafunguka ya Barbara

INATOKA UKURASA 32

wasiwe na mashaka wala wasiwasi, Simba itaendelea kuwa na uimara wake na ubora ule ule, haijalishi mtu bora na umuhimu wa namna gani ameondoka kwa sababu inaongozwa kwa mifumo,” alisema Ahmed.

Hata hivyo, alisema hawajizuii kusikitika kuondoka kwake kwa sababu kwa muda mfupi tu alipoiongoza Simba iliotokea kuwa tishio na klabu bora barani Afrika.

“Barbara ni mtu muhimu, bora sana, ndani ya muda mfupi aliohudumu ameisimamisha Simba kuwa klabu bora na tishio barani Afrika, lakini hakuna namna jukumu letu kama taasisi ni kukubali na kuheshimu maamuzi yake, haijalishi yanaumiza kiasi gani, kilichobaki ni kuhakikisha taasisi haiyumbi na huo ndiyo msingi wa taasisi imara. Na kwa sababu yupo kwa mwezi mmoja zaidi, kuna michakato mikubwa miwili ataisimamia hadi kufikia Januari, kwanza ni usajili wa kipindi hiki cha dirisha dogo na mchakato mzima wa uchaguzi hadi viongozi wapya watakapoingia madarakani,” alisema Meneja habari huyo.

## *Simba, Yanga mdomoni mwa Waarabu CAF*

INATOKA UKURASA 32

na USM Alger ya Algeria. Hapa Yanga inaweza kukutana na ama Pyramids, ASEC Mimosas au USM Alger.

St Eloi Lupopo ya DR Congo, Al Akhdar ya Libya, Real Bamako ya Mali, na River United ya Nigeria hizi zipo Pot namba tatu. Katika Pot hili Yanga kuna uwezekano mkubwa wa kukutana na Al Akhdar, Real Bamako ama River United.

Katika Pot namba nne zipo Diables Noirs ya Congo Brazzaville, Future ya Misri, Marumo Gallants ya Afrika Kusini na ASKO Kara ya Togo. Hapa Yanga itarajie kukutana na ama Future, Marumo Gallants au ASKO Kara.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 12/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3436 | SP. Braga U23 vs FC Vizela U23 | 2.00 | 3.51 | 3.17 |
| 14:00 | 3446 | Ihud Bnei Shfaram vs Hapoel Haifa | 6.21 | 4.47 | 1.40 |
| 14:00 | 3936 | Hapoel Qalansawe vs Bnei Sakhnin | 10.64 | 5.80 | 1.20 |
| 14:00 | 5210 | SC Tira vs Hapoel Petah Tikva | 5.81 | 4.26 | 1.44 |
| 14:00 | 5725 | Kenya Police vs Bandari | 3.16 | 2.82 | 2.33 |
| 15:00 | 2157 | Sofapaka vs AFC Leopards | 2.59 | 2.78 | 2.83 |
| 15:45 | 1088 | Ceramica Cleopatra vs Haras EL Hodood | 1.85 | 3.04 | 4.89 |
| 15:45 | 3053 | Episkopi FC vs Apollon Smyrnis | 4.00 | 2.92 | 1.97 |
| 16:00 | 1160 | Mekelakeya vs Wolkite City FC | 2.10 | 3.00 | 3.80 |
| 16:00 | 1888 | Al Fehaheel vs Kazma SC | 4.20 | 3.60 | 1.80 |
| 16:00 | 5872 | Rutsiro FC vs APR FC | 5.64 | 3.26 | 1.62 |
| 16:15 | 4125 | AEK Athens B vs Proodeftiki FC | 2.05 | 3.02 | 3.55 |
| 16:30 | 3550 | Gokulam Kerala FC vs Rajasthan United | 2.36 | 3.11 | 2.82 |
| 18:00 | 1685 | Ismaily SC vs Coca Cola | 3.45 | 2.80 | 2.34 |
| 18:00 | 2173 | Najma Manama vs Malkiya Club | 1.90 | 3.35 | 3.65 |
| 18:00 | 2819 | Al-Tadamun Buri vs Busaiteen | 5.25 | 4.67 | 1.44 |
| 18:00 | 3324 | Bouri vs Al Ittifaq Bhr | 2.82 | 3.26 | 2.28 |
| 18:00 | 5307 | Sporting CP U23 vs SC Farense U23 | 2.30 | 3.70 | 2.53 |
| 18:30 | 4850 | U Craiova SA vs Argesul Pitesti | 2.02 | 3.21 | 3.66 |
| 19:00 | 1400 | Hadiya Hosahina FC vs Adama City FC | 2.06 | 2.76 | 3.97 |
| 19:30 | 4433 | AS Douanes vs ASC Diambars | 4.09 | 2.78 | 2.02 |
| 19:30 | 5746 | NK Mura vs Domzale | 2.01 | 3.50 | 3.16 |
| 20:00 | 1285 | Pendikspor vs Sakaryaspor | 1.83 | 3.45 | 3.79 |
| 20:00 | 4406 | Nea Salamis vs Karmiotissa | 2.04 | 3.35 | 3.55 |
| 20:00 | 4510 | Al Ahly Cairo vs El Ittihad Alexandria | 1.41 | 4.38 | 7.17 |
| 20:30 | 2105 | Hapoel Akko vs Sectzya Nes Ziona | 2.51 | 3.29 | 2.51 |
| 20:30 | 3128 | Ironi Hasharon vs FC Holon Yirmiyahu | 1.48 | 4.10 | 6.40 |
| 20:30 | 4993 | FC Ashdod vs Hapoel Beer Sheva | 4.59 | 3.27 | 1.74 |
| 20:30 | 5441 | Hapoel Katamon vs Maccabi Petach Tikva | 1.68 | 3.45 | 4.66 |
| 20:30 | 5555 | Ahi Nazareth vs FC Tzofi Haifa | 1.12 | 7.36 | 13.56 |
| 20:30 | 5952 | Hapoel Rishon Lezion vs Maccabi Bney Reine | 4.29 | 3.65 | 1.69 |
| 20:45 | 1214 | Hapoel Afula vs Hapoel Tel Aviv | 4.58 | 3.46 | 1.69 |
| 20:45 | 2127 | Jong AZ Alkmaar vs Jong PSV | 2.19 | 3.45 | 2.96 |
| 21:00 | 1304 | Lommel U21 vs Lierse SK U21 | 1.86 | 4.08 | 3.16 |
| 21:00 | 1708 | Racing Club Dabidjan vs Asi D Abengourou | 2.01 | 3.01 | 3.69 |
| 21:00 | 4548 | Nazareth Ilit vs Maccabi Haifa | 21.43 | 9.74 | 1.05 |
| 21:30 | 4171 | CS Mioveni vs Universitatea Craiova | 4.84 | 3.56 | 1.69 |
| 21:30 | 4773 | Hibernians vs Floriana | 1.91 | 3.30 | 3.64 |
| 22:00 | 2593 | Zulte Waregem U21 vs KAA Gent U21 | 4.77 | 4.48 | 1.50 |
| 22:00 | 4088 | Kortrijk U21 vs Oostende U21 | 4.66 | 4.37 | 1.52 |
| 22:00 | 5534 | Mechelen U21 vs Westerlo U21 | 2.53 | 3.84 | 2.25 |
| 22:00 | 5985 | OH Leuven U21 vs RWD Molenbeek U21 | 1.80 | 4.00 | 3.41 |
| 22:30 | 1227 | Foggia vs Catanzaro | 3.25 | 3.00 | 2.33 |
| 22:30 | 1251 | Brescia vs Parma | 2.83 | 3.08 | 2.48 |
| 22:45 | 5923 | Chelmsford vs Slough Town | 1.41 | 4.27 | 6.41 |
| 23:00 | 1288 | Alaves vs Levante | 2.41 | 2.98 | 3.03 |
| 23:00 | 1662 | PEC Zwolle vs Helmond Sport | 1.30 | 5.36 | 7.74 |
| 23:00 | 4244 | Sunderland vs West Bromwich | 2.87 | 3.21 | 2.38 |
| 23:00 | 4345 | FC Martigues vs Concarneau | 3.11 | 3.11 | 2.27 |
| 23:30 | 2344 | Boavista vs Vitoria Guimaraes | 2.77 | 3.11 | 2.40 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Desemba 12, 2022

Nipashe




Kane: Nilaumiwe mimi kutolewa UKURASA 29

MAMA YANGU...



Harry Kane (katikati), akihuzunika sambamba na Jack Grealish (kushoto) na Declan Rice baada ya kukosa penalti dakika za mwisho ambayo ingeiwezesha England kubadili matokeo na kuwa mabao 2-2 kwenye mechi ya robo Fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa nchini Qatar juzi usiku. Ufaransa ilitinga nusu fainali baada ya kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Yanga mdomoni mwa Waarabu CAF leo

**Na Adam Fungamwango**

●●● Kujua wapinzani wao makundi Ligi ya Mabingwa na Shirikisho Afrika, huku wakiangukia...

DROO ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika inatarajiwa kuchezeshwa leo mchana kwenye Ofisi za Makao Makuu ya CAF jijini Cairo, Misri, ambapo klabu za Tanzania Simba na Yanga zitafahamu wapinzani wao watakaokuwa nao kundi moja.

**Droo hiyo ilikuwa ifanyike Novemba 16, lakini iliahirishwa, ambapo leo kila timu itajua iko kwenye kundi gani na imepangwa na nani.**

Simba ambayo itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, itapangwa kwenye moja ya makundi manne, ikiungana na timu zingine ambazo zimeingia na kupangwa kwa mtiririko wa viwango vyao.

Katika kila 'pot' kuna kinara wa kundi ambaye hawezi kukutana na kinara wa kundi lolote kutoka mapot mengine matatu, lakini timu zilizoko pot moja haziwezi kukutana katika hatua hii ya makundi.

Hata hivyo, kwa namna pot zilivyo, wawakilishi wa Tanzania Simba na Yanga, hawawezi kukosa kupangwa na moja kati ya timu kutoka nchi za Afrika ya Kaskazini maarufu kama nchi za Kiarabu, ambazo mara nyingi zimekuwa zikizisumbua timu kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki hususan zikiwa uwanja wao wa nyumbani.

Simba ipo kwenye Pot namba tatu, ikiwa na timu za CR Belouzidad ya Algeria na JS Kablie zote za Algeria na Al Hilal ya Sudan, ambazo haiwezi kukutana na yoyote katika kundi hilo.

Wakati katika Pot namba moja kuna timu zingine ya Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca na Raja Casablanca zote za Morocco pamoja na Esperance ya Tunisia. Katika pot hili, uwezekano mkubwa wa Simba ni kukutana na timu mojawapo kati ya Wydad Casablanca, Raja Casablanca ama Esperance.

Pot namba mbili zipo Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Zamalek ya Misri, Petro de Luanda ya Angola na Horoya ya Guinea. Hapa uwezekano mkubwa kwa Simba inaweza kukutana na ama Zamalek, Petro de Luanda au Horoya.

Katika Pot namba nne kuna timu za AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Coton Sport ya Cameroon, Al Merrikh ya Sudan na Vipers ya Uganda. Hapa uwezekano wa Simba ni kukutana na Coton Sport, Al Merrikh au Vipers.

Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga ambao ndio wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo wapo Pot namba mbili na timu za Motema Pembe ya DR Congo, Asfar ya Morocco, ambazo haziwezi kukutana nao katika hatua ya makundi.

Pot namba moja kuna timu za TP Mazembe ya DR Congo, Pyramids ya Misri, ASEC Mimosas ya Ivory Coast

INAENDELEA UK. 31

# ...Yafunguka Barbara kuondoka

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeeleza kuhuzunishwa na kusikitishwa na taarifa za kujiuzulu kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wake Barbara Gonzalez, ikisema kuwa imepoteza mtu bora na muhimu, lakini inaheshimu maamuzi yake ikimtakia kila la kheri kwenye majukumu yake mengine mapya.

Aidha, klabu hiyo imesema kwa sasa ataendelea na kazi hadi Januari mwakani, akisimamia usajili wa dirisha dogo unaotarajiwa kuanza Alhamisi wiki hii pamoja na uchaguzi mzima hadi kupatikana kwa viongozi wapya watakaoingia madarakani.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema jana kuwa Simba kama klabu imepokea kwa masikitiko makubwa kwa sababu taasisi ni kama familia akiondoka mtu bora na muhimu ni lazima waliobaki wasikitike, huku akiwatuliza wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi kwani klabu itaendelea kuwa imara.

"Tumepokea kwa masikitiko makubwa, kama taasisi au familia akiondoka mmoja mtu muhimu na bora lazima mhuzunike na msikitike, lakini Simba ni moja kati ya taasisi kubwa na imara kwa hiyo hakuna kitakachoharibika na niombe nitumie nafasi hii kuwatuliza wanachama na mashabiki

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >